CHUO KIKUU CHA KENYATTA

SHULE YA FANI NA SAYANSI ZA JAMII

IDARA YA KISWAHILI

# ATHARI YA MAZINGIRA YA KIHISTORIA NA KIJAMII KATIKA UWASILISHAJI WA MAUDHUI YA *DHIFA* (E. KEZILAHABI).

TASNIFU

YA

NASIMIYU .M. CHRISTINE

C50/24587/2013

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.

2016.

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

# IKIRARI

**Tasnifu hii ni kazi yangu asili na haijawahi kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika Chuo Kikuu kingine.**

______________________________ 28/4/2016
______________________________

**NASIMIYU M. CHRISTINE** **TAREHE**

**C50/24587/2013**

**(Mtahiniwa)**

**Wasimamizi:**

**Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa ridhaa yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta.**

______________________________ 28/4/2016
______________________________

**DAKTARI EDWIN MASINDE WANYONYI** **TAREHE**

**IDARA YAKISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

______________________________ 28/04/2016
______________________________

**DAKTARI JOSEPH GAKUO KARIUKI** **TAREHE**

**IDARA YA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA KENYATTA.**

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mwanangu mpendwa Pretty-Joy Namaemba, wazazi wangu Ben na Mary Musimbi na ndugu zangu Daisy Namurwa, Elizabeth Nelima, Millicent Nafula, Fred Wekesa, Elija Masinde, Dennis Mwasame na Gloria Namaemba.Uvumilivu, subira na nguvu mliyonipa ilinipa ari ya kukamilisha kazi hii.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa ningependa kutoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika umbali huu.

Nawashukuru wasimamizi wangu Daktari Edwin Masinde na Daktari Joseph Gakuo kwa kujitolea kuniongoza na kunijenga kwa busara na ukakamavu. Nawaombea maisha marefu ili mwafae wengine.

Nakishukuru Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kunipa fursa ya kushughulikia tasnifu hii katika Idara ya Kiswahili.

Nawashukuru wazazi wangu Ben na Mary Musimbi kwa kushughulikia masomo yangu tokea utotoni hadi sasa.

Nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili. Mafundisho yenu yalinifaa sana. Mungu awazidishie hekima na maisha marefu.

Pia nawashukuru wenzangu Midika, Onyancha, Ngugi, Odhiambo, Wanyela, Cheruiyot, Kimama, Kibet, Wamalwa, Jelimo, Khavai, Aor na wengine. Tulifaana kwa mengi kuliabiri jahazi hili la elimu hadi ufuoni. Ahsanteni sana.

Shukrani za mwisho ziwaendee aila yangu kwa uvumilivu na kunitia moyo katika safari hii. Kate Musimbi, Millicent Nafula, Gloria Namaemba, Elija Masinde na Dennis Musimbi endeleeni kupiga mbizi katika bahari ya masomo. Mungu awazidishie neema na uwezo. Kwa wote nasema Mungu awabariki.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

**Uwasilishaji**: Ni jinsi mtunzi wa kazi ya fasihi anavyowasilisha maudhui au ujumbe kwa hadhira na wasomaji.

**Maudhui**: Ni jambo kuu liongelewalo na kushughulikiwa katika kazi ya fasihi. Ule ujumbe mkuu ujitokezao kwa mujibu wa mtazamo wa msanii.

**Dhamira:** Hiki ni kiini au lengo la kutunga kazi husika.

**Jamii:** Kikundi cha watu kinachoishi pamoja katika eneo fulani la kijiografia au watu wa matabaka tofauti wanaoishi eneo moja.

**Fani:** Jumla ya nyenzo zinazotumiwa kuwasilisha maudhui.

**Mazingira:** Hali au mambo yanayomzunguka kiumbe katika sehemu au maisha yake.

# IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza athari ya mazingira ya kihistoria na kijamii katika uwasilishaji wa maudhui ya diwani ya *Dhifa* ya E. Kezilahabi (2008). Malengo yalikuwa, kubainisha maudhui yaliyowasilishwa na mtunzi wa *Dhifa*, kubainisha namna maudhui haya yalivyowasilishwa na kueleza namna maudhui haya yalivyoibua mazingira ya kijamii na kihistoria. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Uhistoria Mpya ambayo huangalia umuhimu wa muktadha katika utunzi na uhakiki wa kazi za kifasihi. Pia, huonyesha ya kwamba kadiri jamii zinavyoendelea, utamaduni hubadilika kiwakati na jambo hili huathiri utunzi, uwasilishaji na uhakiki wa kazi za kifasihi. Utafiti huu ulizingatia muundo wa kimaelezo kuhusu suala la utafiti, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti. Utafiti huu ulifanywa maktabani. Sampuli iliteuliwa kimakusudi ambapo mashairi ishirini na moja yaliteuliwa ili saba yashughulikie kipengele cha siasa, uchumi na masuala ya kijamii. Data ilikusanywa kutokana na usomaji wa kina wa mashairi teule. Uchanganuzi wa data ulizingatia uainishaji wa aina ya maudhui, uwasilishaji wake pamoja na matukio ya kihistoria. Aidha, ulizingatia chimbuko la maudhui, namna yalivyowasilishwa, dhamira na falsafa ya mtunzi. Hayo yote yalifanywa kwa kuzingatia pengo lililonuiwa kujazwa na utafiti huu kwa kuongozwa na nadharia ya utafiti. Utafiti ulibaini na kutambua kwamba, siasa ya Tanzania, baada ya Azimio la Arusha ilichukuwa mkondo mpya. Aidha, mazingira mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi yalichangia pakubwa katika kuwasilisha maudhui ya diwani ya *Dhifa*. Inatarajiwa kuwa utafiti huu utawafaa wanafunzi wa shule za upili, vyuo, watafiti wa ushairi na wakuza mitalaa. Tasnifu hii iligawanywa katika sura sita. Sura ya kwanza ilishughulikia mada ya utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, sababu za kuchagua mada na misingi ya nadharia. Sura ya pili ilichunguza historia na falsafa ya mtunzi. Sura ya tatu iliangazia maudhui ya kisiasa. Sura ya nne ilichambua maudhui ya kiuchumi. Sura ya tano iliangalia maudhui ya kijamii. Sura ya sita ilijumuisha muhtasari, hitimisho,matokeo ya utafiti na mapendekezo.

# YALIYOMO

MADA ... i
IKIRARI ... ii
TABARUKU ... iii
SHUKRANI ... iv
UFAFANUZI WA ISTILAHI ... v
IKISIRI ... vi
YALIYOMO ... vii
SURA YA KWANZA ... 1
1.0 Utangulizi ... 1
1.1 Usuli wa Mada ... 1
1.2 Suala la Utafiti ... 3
1.3 Maswali ya Utafiti ... 4
1.4 Malengo ya Utafiti ... 4
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ... 5
1.6 Upeo na Mipaka ... 6
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ... 6
1.8.0 Msingi wa Nadharia ... 11
1.8.1 Nadharia ya Uhistoria Mpya ... 11
1.8.2 Mbinu za Utafiti ... 14
1.8.3 Muundo wa Utafiti ... 14
1.8.4 Mahali pa Utafiti ... 14
1.8.5 Sampuli na Mbinu za Uteuzi Wake ... 14
1.8.6 Mbinu za Kukusanya Data ... 15
1.8.7 Uchanganuzi wa Data ... 15
1.8.8 Uwasilishaji wa Matokeo ... 15
1.9 Muhtasari ... 16
SURA YA PILI ... 17
Historia, Mazingira na Falsafa ya Mtunzi ... 17
2.0 Utangulizi ... 17
2.1 Mazingira ya Msanii ... 17

2.2 Wakati wa Ukoloni ........ 20
2.3 Kabla na baada ya Azimio la Arusha ........ 25
2.4 Mashairi katika Kipindi cha Uhuru na Azimio la Arusha ........ 30
2.5 Kumhusu Mtunzi Euphrase Kezilahabi ........ 34
2.6 Muhtasari ........ 38
SURA YA TATU ........ 39
Maudhui ya Kisiasa ........ 39
3.0 Utangulizi ........ 39
3.1 Shairi: 'Dhifa' ........ 39
3.2 Shairi: 'Madomo Mapana' ........ 43
3.3 Shairi: 'Jibwa' ........ 47
3.4 Shairi: 'Cha Watu' ........ 51
3.5 Shairi: 'Bonde' ........ 53
3.6 Shairi: 'Ulingoni' ........ 55
3.7 Shairi: 'Mafuriko' ........ 56
3.8 Muhtasari ........ 58
SURA YA NNE ........ 59
Maudhui ya Kiuchumi ........ 59
4.0 Utangulizi ........ 59
4.1 Shairi: 'Maendeleo si Ndwele' ........ 59
4.2 Shairi: 'Njia Tulopitishwa' ........ 61
4.3 Shairi: 'Ukweli Koko' ........ 64
4.4 Shairi: 'Alalaye' ........ 67
4.5 Shairi: 'Maskini 2' ........ 68
4.6 Shairi: 'Maskini 3' ........ 70
4.7 Shairi: 'Zimwi' ........ 71
4.8 Muhtasari ........ 73
SURA YA TANO ........ 74
Maudhui ya Kijamii ........ 74
5.0 Utangulizi ........ 74
5.1 Shairi: 'Mke wa Waziri' ........ 74

5.2 Shairi: 'Marahaba' ..... 77
5.3 Shairi: 'Wimbo wa Unyago' ..... 79
5.4. Shairi: 'Makaburini' ..... 81
5.5 Shairi: 'Hoja' ..... 83
5.6 Shairi: 'Namagondo iii' ..... 85
5.7 Shairi: 'Msamaha' ..... 86
5.8 Muhtasari ..... 88
SURA YA SITA ..... 89
Hitimisho, Matokeo na Mapendekezo ya Utafiti ..... 89
6.1 Muhtasari ..... 89
6.2 Matokeo ya Utafiti ..... 92
6.3 Changamoto za Utafiti ..... 96
6.4 Umuhimu wa Matokeo ya Utafiti ..... 96
6.5 Mapendekezo ..... 97
MAREJELEO ..... 98
Kiambatisho: Mashairi Teule ..... 104

# SURA YA KWANZA

## Msingi wa Utafiti

### 1.0 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia usuli wa mada ya utafiti, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti. Vilevile, sababu za kuchagua mada na umuhimu wake, upeo wa utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi wa nadharia na mbinu zilizotumiwa katika utafiti: muundo wa utafiti, sampuli iliyotumiwa, njia za kukusanya data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo.

### 1.1 Usuli wa Mada

Mazingira ya kihistoria na kijamii huathiri utunzi wa msanii kifani na kimaudhui. Kila utungo wa fasihi una chanzo chake katika maisha ya binadamu. Hazina kubwa ya msanii wa fasihi ni jumla ya maisha yanayopatikana katika mazingira yake ya kihistoria na ya kijamii. Hivyo, msanii kwa mara nyingi huzoa mawazo kutoka katika jamii yake.

Mshairi wa Kiswahili ana sababu nyingi zinazomfanya atunge mashairi. Ni mtu aliye macho daima. Ni nadra kumwona amenyamaa panapotukia jambo fulani katika mazingira yake anamoishi. Akiona jamii au taifa lake linaelekea kombo anatahadharisha na kulizindua. Hupenda kukashifu uongozi wa nchi yake. Kwa jumla lengo muhimu la shairi ni kuhifadhi matukio ya kihistoria na utamaduni wa jamii (Masinde, 1992).

Washairi wa Kiswahili, kama walivyo wasanii wengine katika jamii yoyote ile ni zao la jamii hiyo. Wasanii huishi katika jamii zao na tukio lolote la kijamii au kihistoria huwaathiri kwa njia moja au nyingine. Athari hizi hujenga tajriba zao. Kutokana na

tajriba hizo, watunzi hupata ilhamu au mguso wa kutunga kazi za kifasihi kubainisha namna walivyoathiriwa na matukio hayo. Kwa kiwango kikubwa, kazi za kifasihi huakisi yale yanayotendeka katika mazingira maalum ya kijamii na kihistoria kwa mujibu wa wakati. Hivyo, yale wanayoyashughulikia na namna wanavyoyashughulikia huendana na athari walizopata pamoja na viwango binafsi vya ubunifu wa watunzi husika. Mabadiliko yatokeayo katika nyanja zote za maisha kama vile kiuchumi, kisiasa na kijamii huathiri namna watunzi wanavyoshughulikia kazi zao (Masinde, 1992).

Maisha ya mtunzi wa shairi na mazingira yake humpa tajriba ya namna anavyoitunga kazi yake kwa sababu namna anavyowasilisha kazi yake hutegemea itikadi na falsafa yake kama mtu binafsi. Kwa hivyo, historia ya maisha ya watunzi ni muhimu katika kueleza chimbuko la maudhui na namna yanavyowasilishwa. Hadhira anayolenga msanii pia huathiri namna anavyotunga kazi yake. (Masinde, 1992).

Madumulla (1988) anaeleza, katika kila kipindi cha maisha kuna matukio fulani ambayo hujitokeza zaidi kuliko mengine. Baadhi yanaweza kuigusa jamii kwa uzuri au kwa ubaya kwa mujibu wa kipindi maalum cha kihistoria. Aidha, tukio linapokuwa hivi, huwa mada kuu na muhimu kwa jamii inayohusika na hukumbukwa kwa miaka mingi baadaye.

Kulingana na Mlacha (1984) historia ya kipindi fulani cha utunzi ni muhimu katika utunzi wa kazi za kifasihi ukiwemo ushairi. Kwa mfano, katika utafiti huu ilibainika kwamba sera zilizobuniwa baada ya uhuru Tanzania na hasa Azimio la Arusha la 1967 lililolenga kuvunja mifumo ya ubepari na kujenga ujamaa, kuondoa utabaka, kuijenga Tanzania Bara kiuchumi na kisiasa na kukomesha unyonyaji, uonevu na umaskini

ziliathiri ulimwengu wa watunzi wa Tanzania kihulka kwa kuwa katika miaka ya 1970 na kuendelea, watunzi walitunga kazi zao kwa njia ya kuhakiki na kutathmini iwapo malengo ya Azimio la Arusha yalifaulu.

Washairi wa Kiswahili wana nafasi mbalimbali katika jamii kama vile kukashifu uovu. Wametambua kuwa maisha si jana na leo tu, bali pia kuna kesho ambayo lazima ifanyiwe matayarisho yake kwa kutumia leo. Hamu ya mtunzi ni kuiumba jamii mpya kufuatana na jinsi anavyoyaona matatizo yanayoikabili jamii yake. Kwa vile fasihi ni kama kioo cha jamii na ushairi kama picha au vivuli vyetu kwenye kioo hicho, utunzi humulika ule urazini wa jamii husika katika kipindi husika. Mlacha, (1984).

Namna watunzi hushughulikia kazi zao huathiriwa na mambo kadha wa kadha. Miongoni ni kama vile, viwango vyao vya ubunifu, hadhira lengwa, tajriba ya mtunzi, falsafa ya mtunzi na itikadi yake kuhusiana na suala analoshughulikia.Kutokana na maelezo ya hapo juu, ni dhahiri kwamba kulikuwa na haja ya kufanya utafiti kuhusu diwani ya *Dhifa* kuhusu chimbuko la maudhui,namna yalivyowasilishwa na mazingira ya kijamii na kihistoria yaliobua maudhui husika.

**1.2 Suala la Utafiti**

Utafiti huu ulichunguza athari ya mazingira ya kihistoria na kijamii katika uwasilishaji wa maudhui ya *Dhifa.* Mtafiti amechochewa na sababu kwamba utungo wa fasihi una chanzo chake katika maisha ya binadamu katika mazingira yake maalum ya kihistoria, kiuchumi na kijamii. Hazina kubwa ya msanii wa fasihi ni jumla ya maisha yanayopatikana katika mazingira yake ya kijamii na ya kihistoria. Hivyo, msanii hupata

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

tajriba na mawazo ya kushughulikia katika utungo wake kutokana na yale anayoyashuhudia, kusikia, na kukumbana nayo.

Nchi ya Tanzania ilipitia mabadiliko mbalimbali ya kijamii na kihistoria wakati wa ukoloni na baada ya uhuru. Mabadiliko hayo yaliathiri utunzi wa mashairi kifani na kimaudhui. Ni kwa misingi hii ambapo utafiti ulifanywa. Kadri mtafiti ajuavyo, utafiti unaofuata mkabala huu haujafanywa.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

a) Ni maudhui gani yamewasilishwa na mtunzi wa diwani ya *Dhifa*?

b) Maudhui hayo yamewasilishwa vipi?

c) Mazingira gani ya kihistoria, kiuchumi na kijamii yaliibuwa maudhui hayo?

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu ni:

a) Kubainisha maudhui yaliyowasilishwa katika diwani ya *Dhifa.*

b) Kueleza namna maudhui ya *Dhifa* yalivyowasilishwa.

c) Kubainisha mazingira ya kihistoria, kiuchumi na kijamii yaliyoibua maudhui haya.

**1.5 Sababu za Kuchagua Mada**

Mada hii ilichaguliwa ikizingatiwa kwamba ni kupitia kwa maudhui na namna yalivyowasilishwa ndipo mtunzi huwasilisha dhamira kwa hadhira na wasomaji. Ushairi ulichaguliwa kwa sababu utanzu huu umewahi kutungiwa maswala mbalimbali katika mazingira ya watunzi na ndio umetumikia jamii zaidi ya tanzu zingine za fasihi.

Mazingira maalum ya kijamii na kihistoria huwa malighafi ya mtunzi kifani na kimaudhui. Hivyo, huwa ni chimbuko la maudhui na lugha inayotumika kuwasilishia ujumbe. Kihistoria, utanzu huu umepitia mabadiliko mengi kifani na kimaudhui kufikia hali yake ya sasa. Hii ina maana ya kwamba mshairi wa Kiswahili amekuwa na uhusiano wa aina mbalimbali na jamii yake kwa kueleza hisia, mahitaji na matarajio ya jamii katika nyakati tofauti za kihistoria (Senkoro, 1988 na Abdalla, 1978).

Kuna maudhui mbalimbali ambayo yameshughulikiwa na Kezilahabi. Kwa hivyo, kulikuwa na umuhimu wa kufanya utafiti ili kubaini maudhui hayo. Aidha, Kezilahabi ni mtunzi anayeshughulikia masuala ya jamii ya sasa katika mazingira na kipindi cha sasa cha historia kuwasilisha ujumbe wake. Hii ina maana ya kwamba ilikuwa muhimu kubainisha maudhui aliyoshughulikia na namna alivyoyashughulikia katika *Dhifa*.

Utafiti huu umetarajiwa kuwa na manufaa kwa wanafunzi, watafiti, wahakiki, na wakuza mitaala. Wanafunzi watakuwa na uelewa kuhusu uhakiki wa maudhui na jinsi yanavyowasilishwa. Wakuza mitaala nao wataweza kuteua vipengele vya ufunzaji na ujifunzaji wa ushairi. Wahakiki watanufaika na mbinu za uhakiki kwa kuzingatia namna uhakiki wa maudhui na dhamira hushughulikiwa.

## 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu ulijikita katika utanzu wa ushairi wa Kiswahili. Ulimwangazia Kezilahabi kwa sababu mtunzi huyu ni miongoni mwa watunzi maarufu katika taaluma ya ushairi wa Kiswahili. Vilevile, anashughulikia masuala ya kisasa kwa kutumia mitindo ya kisasa katika mazingira ya kisasa kiwakati.

Utafiti uliangazia maudhui kwa sababu ni kupitia kwayo ambapo tunapata lengo na mafunzo ya mtunzi kwa hadhira na wasomaji. Aidha, namna anavyowasilisha maudhui ni muhimu katika utunzi wa kifasihi kwa sababu ndiyo njia anayoitumia mtunzi kuiathiri jamii kupitia kuzindua, kutahadharisha, kukashifu, kuelekeza na kwa jumla kuelimisha. Maudhui ambayo yalishughulikiwa ni yale yanayohusu masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Mtafiti alishughulikia mashairi ishirini na moja yenye maudhui ya siasa, uchumi na jamii, namna yalivyowasilshwa na utendakazi wake ili kupata data toshelevu, saba kwa kila kipengele husika. Kezilahabi ametunga diwani kadha kama vile *Kichomi* na *karibu ndani.* Hata hivyo, mtafiti alichagua *Dhifa* kwa sababu haijashughulikiwa kadiri ajuavyo kwa kuzingatia mkabala wa utafiti huu.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Swala la maudhui limeshughulikiwa na waandishi, wahakiki na watafiti wengi. Kezilahabi (1974) anasema kwamba, ushairi ni tukio, hali au wazo ambalo limeonyeshwa kwetu kutokana na upangaji mzuri wa maneno fasaha yenye mizani kwa ufupi. Maneno haya yanalenga kuonyesha ukweli fulani wa maisha. Kauli hii imeshadidiwa na Mulokozi na Kahigi (1979) kuwa ushairi ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalum wa maneno fasaha na yenye muwala, kwa lugha ya mkato, picha, sitiari, ishara, usemi

maandishi na mahadhi ya nyimbo. Ushairi hueleza mawazo, kufunza, kueleza tukio au hisi fulani kuhusu maisha au mazingira ya jamii kwa njia inayogusa moyo. Kazi hizi zilituchochea kufanyia utafiti diwani ya *Dhifa* ili kubaini namna lugha ilivyotumiwa kisanaa kuibua ujumbe wa mtunzi. Aidha, maelezo yao yalisaidia kuchunguza dhamira ya Kezilahabi katika uwasilishaji wa maudhui mbalimbali kwa kuongozwa na malengo mahsusi.

Diwani ya *Sauti ya Dhiki* yake Abdilatif ilichunguzwa na Matteru (1975) katika kiwango cha maudhui, muundo na matumizi ya lugha. Kazi hii ilitufaa kujua jinsi lugha huibua maudhui ya kazi ya fasihi. Ingawa inafanana kwa kiasi kikubwa na utafiti huu, yeye alisisitiza matumizi ya lahaja ya Kimvita na uwezo wake wa kutumia tamathali za usemi. Utafiti wa Matteru unatofautiana na huu kwa sababu utafiti wake ulijikita katika lahaja ya Kimvita na uwezo wake wa kutumia tamathali za usemi. Utafiti wetu ulijikita katika diwani ya *Dhifa* na ulishughulikia athari ya mazingira ya kijamii na kihistoria katika uwasilishaji wa maudhuina namna maudhui haya yalivyowasilishwa.

Utafiti kuhusu ushairi wa Abdilatif katika kiwango cha maudhui ulifanywa na Chacha (1987) akizingatia *Sauti ya Dhiki*. Alichukua mtazamo wa Kimaksi na kuhakiki vipengele vya kimtindo, kwani mtindo ni nyenzo kuu ya kuwasilisha maudhui ya mwandishi. Utafiti huu uliufaa utafiti wetu katika kujua jinsi maudhui huibuka na kuwasilishwa kwa hadhira na wasomaji. Tafiti hizi zinatofautiana katika nadharia, watunzi, mazingira ya watunzi, malengo ya utafiti na matini.

Senkoro (1988) amekariri kwamba, kinachofanya maudhui kuwa muhimu katika ushairi ni uwasilishaji wake kupitia kwa ishara mahususi za lugha ambazo hujengeka katika tamathali za usemi. Alibainisha kuwa, mtindo ni namna ambayo msanii huipa kazi ya fasihi sura ya kifani na kimaudhui kwa njia ambayo msanii asingeweza kuipa hata kama jambo linalozungumziwa na wasanii hawa ni lilelile. Kauli yake imeendelezwa na Massamba (2003). Kwa ujumla, sanaa hiyo iko katika uteuzi na mpangilio maalum wa maneno na viwango tofauti vya wasanii. Kutokana na matumizi mahsusi ya lugha na mbinu za uwasilishaji, ushairi huweza kujenga mazingira ya kuathiri na kuigusa mioyo ya hadhira. Kauli zao zilitusaidia kulenga vipengele hivyo kwa ujumla.Utafiti wetu unatofautiana na kazi yao katika kiwango cha nadharia, tofauti katika vipindi vya historia, watunzi, tajriba zao na mazingira yao.

Masinde (1992) alishughulikia mtindo na dhamira katika mashairi huru ya Kiswahili kwa lengo la kuonyesha kuwa dhamira na mtindo ni uti wa mgongo wa shairi na hudhihirika katika kazi moja. Alibainisha kuwa shairi lina sifa za kipekee na kuwa umbo la ndani la shairi ndilo muhimu zaidi katika kubainsha utanzu huu kwa kuongozwa na nadharia ya kimtindo. Katika mwaka wa 2003 alishughulikia ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na mabadiliko ya maudhui akiongozwa na nadharia ya uhistoria mpya ambayo ndiyo iliongoza utafiti huu. Kazi yake ilisaidia katika kuelewa vipengele vya kijamii na kihistoria vinavyoweza kuibua na kuleta mabadiliko katika kuwasilisha maudhui ya mtunzi husika. Alipata kwamba kila kipindi maalum cha kihistoria huathiri utunzi wa mashairi kwa njia moja au nyingine. Aidha, uhakiki wa kihistoria ni njia faafu zaidi ya

kuweza kuuelewa na kuutathmini vyema zaidi ushairi wa Kiswahili. Utafiti wake unatofautiana na huu katika malengo, maswali, watunzi wa kazi husika na matini.

King'ei (2000: XV) anasema kwamba kila fasihi nzuri ni ile yenye kuhimiza, kuboresha, au kuimarisha ujenzi wa jamii imara yenye uadilifu, usawa na haki. Maudhui ya fasihi yoyote huzalika kutokana na hali ya jamii ilivyo na kwa wakati wake. Kazi yake ilitusaidia kuimarisha swala la utafiti. Amegusia vipengele muhimu kwa kijumla vinavyohusiana na utafiti huu. Tofauti na kazi yake, utafiti huu uliongozwa na nadharia, pamoja na malengo mahususi kwa kuzingatia diwani teule.

Wamitila (2003) anasema kuwa, maudhui ni neno linalotumiwa kujumulisha yaliyomo katika kazi ya kifasihi. Katika uchambuzi wa maudhui, msomaji anapaswa kuangalia dhamira, ujumbe na falsafa ya mshairi. Kazi hii inahusiana na utafiti wetu katika kipengele cha maudhui. Inagusia dhana ya maudhui na kupendekeza yanayopaswa kuzingatiwa katika uchambuzi wake. Tofauti na utafiti huu ni kwamba, Wamitila ametoa ufasiri wa kipengele cha maudhui na namna ya kuchambuliwa. Utafiti wetu ulijikita katika uchunguzi mahsusi wa kazi teule kwa kuzingatia uwasilishaji wa kipengele cha maudhui na utendakazi wake. Vilevile, utafiti huu pia uliongozwa na nadharia ya uhakiki na malengo mahsusi.

Gicuku (2011) alishughulikia usawiri wa maudhui ya ndoa katika ushairi wa Kezilahabi na Mberia kwa lengo la kubainisha jinsi watunzi hawa walivyoyasawiri haya maudhui na changamoto zinazobainika katika asasi hii. Utafiti huu ulikuwa wa manufaa kwetu. Ulitufaa katika kudhihirisha maudhui mbalimbali yaliyowasilishwa na mtunzi wa *Dhifa.* Tofauti na utafiti wake, wetu ulishughulikia jinsi mazingira huathiri utunzi. Pia, yeye

alitumia nadharia ya umuundo –utekelezi na huu uliongozwa na nadharia ya uhistoria mpya.

Mutiiria (2014) alishughulikia mchango wa kimaudhui wa watunzi wa kike katika ushairi wa Kiswahili akiongozwa na nadharia ya maadili kwa malengo ya kubainisha mchango wa watunzi wa kike katika maendeleo ya utunzi wa ushairi .

Ojenge (2014) alishughulikia maudhui yanayohusiana na maswala ibuka katika ushairi huru wa Kiswahili. Alilenga kubainisha chanzo cha maswala ibuka, athari ya maswala hayo katika jamii na namna yalivyosawiriwa, akiongozwa na nadharia ya maadili. Utafiti wake unahusiana na wetu kwa kuwa yeye pia aliangazia maudhui.Tofauti ni kwamba utafiti huu una malengo na nadharia tofauti.

Utafiti kuhusu changamoto za uchanganuzi na ufasiri wa ushairi katika shule za upili nchini Kenya ulifanywa na Gakuo (2014). Lengo lake lilikuwa kutathmini jinsi muktadha wa kitamaduni na mazingira ya mtunzi yanavyoakisi mawasiliano katika tungo za ushairi. Pia, alichunguza athari za muktadha wa kitamaduni na mazingira yanayomzunguka mtunzi katika uwasilishaji wa maudhui yake. Aliongozwa na nadharia za ki-hemenitiki na ya uhistoria mpya ambayo ndiyo iliongoza utafiti wetu. Kazi yake ilitufaa katika kueleza namna mazingira ya mtunzi kwa ujumla wake huathiri utunzi, uhakiki na uwasilishaji wa kazi husika. Utafiti wake ulitufaa pia katika kuelewa na kutumikiza nadharia ya uhistoria mpya kwani swala la muktadha haliwezi kutenganishwa na kazi za kifasihi. Utafiti wake unatofautiana na wetu katika malengo, matini na watunzi. Wetu ulimwangazia mtunzi Kezilahabi na ulijikita katika diwani teule.

Tafiti zilifanywa na vitabu kuandikwa kuhusu ama fani au dhamira na maudhui katika mashairi ya Kiswahili kwa malengo mbalimbali. Hata hivyo, hazijazingatia mazingira, historia na falsafa ya watunzi wa kazi husika katika vipindi tofauti vya historia. Utafiti huu ulichunguza athari ya mazingira ya kihistoria na kijamii katika uwasilishaji wa maudhui. Pia, ulibainisha namna falsafa ya mtunzi na kiwango chake cha ubunifu huathiri namna anavyowasilisha kazi yake. Kadri mtafiti ajuavyo utafiti unaofuata mkabala huu haujafanywa. Hali hii ni ishara tosha kwamba palikuwa na pengo ambalo utafiti huu ulijaza.

## 1.8.0 Msingi wa Nadharia

### 1.8.1 Nadharia ya Uhistoria Mpya

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhistoria Mpya. Nadharia hii inahusishwa na shule ya wahakiki wa Kimarekani. Wanatambua umuhimu wa muktadha wa kihistoria katika uteuzi, usomaji na uhakiki wa kazi za kifasihi.Nadharia hii ina misingi yake katika mawazo yao Raymond (1977) na Foucault (1972, 1977, 1997).

Mawazo makuu ya nadharia hii ni kwamba, kila tukio la kielezi au kisimulizi hutegemezwa kwenye hali changamano ya matukio ya kiyakinifu. Tukio lolote la kufichua, kuhakiki, kukosoa na hata kupinga huishia kuzitumia mbinu anazozipinga mhakiki. Aidha, kazi za kifasihi na zisizo za kifasihi huingiliana kimzunguko na hamna usemi wowote wa kiubunifu unaoweza kuelekeza kwenye ukweli usiobadilika au unaoelekezea hali ya kibinadamu isiyoweza kubadilishwa.

Mtindo wa kuhakiki kwa lugha inayoakifu huelezea utamaduni unaopatikana katika jamii inayorejelewa. Njogu na Chimera (1999) wanaeleza kuwa fasihi huchipuka kutokana na

tajriba ya maisha ya wanajamii na mtagusano wao kijamii, kisiasa na kichumi. Jamii ndiyo hujenga mazingira ambayo ni nguzo kuu ya msomaji wa kazi ya fasihi na uhakiki wake.

Wana-Uhistoria Mpya wanatofautiana na wana-Uhistoria Jadi katika masuala kama utopendeleo na udumaji. Wao wanajihusisha na kutafuta mbinu mpya za kusawiri matukio ya wakati uliopita katika muktadha wa wakati uliopo lakini siyo kusawiri historia au wakati uliopita. Maelezo haya yalifaa katika utafiti huu kwa sababu haujihusishi na kuweka maudhui yaliyoibuka katika diwani ya *Dhifa* kwenye muktadha wa kihistoria, bali ni kuyachanganua yanavyoibuka wakati huu ili kuakisi ukweli mbalimbali na wa maana kifasihi. (Gakuo, 2014).

Kulingana na wana-Uhistoria Mpya, mwingiliano matini uliopo unapatikana kwa kuitazama jamii pamoja na utamaduni wala siyo sharti mhakiki wa fasihi kujifunga kwenye kipengele fulani maalum cha kazi hizi. Ni makosa kuitenga kazi ya fasihi na muktadha wa kijamii kwani fasihi ni zao la jamii na jamii ndiyo huipa uhai.Wanachosema ni kwamba fasihi ipo kwa sababu jamii ipo lakini siyo kinyume chake. Akiendeleza kauli hii, Wamitila (2002) anasema kuwa huwezi kuihakiki fasihi kama tukio huru na jamii kwani haitoki katika ombwe tupu.Fasihi ni tajriba ya maisha ya wanajamii na mtagusano wao kijamii, kisiasa na kiuchumi. Jamii ndiyo hujenga mazingira ambayo ni nguzo kuu ya msomaji wa kazi ya fasihi na uhakiki wake.

Nadharia hii ina mihimili ifuatayo ambayo iliongoza utafiti huu:

1) Kazi za kifasihi ni matokeo ya uhusiano changamano wa kimwingiliano matini na wala sio kazi zinazotokana na ubunifu wa mwandishi peke yake. Mhimili huu ulitufaa katika kuchanganua utungo wa fasihi kama zao la jumuiya fulani ambapo utamaduni na maendeleo ya fasihi pamoja na mambo ya kijamii na kihistoria huchangamana ili kuupa utungo fulani mfumo wake maalum.Vilevile, ulitusaidia kuelewa *Dhifa* ilitungwa katika mazingira yapi ya kihistoria na kijamii.
2) Kila kazi za kubuni zina muktadha wa kijamii na zina mahusiano yanayoingiliana.Mhimili huu ulifaa katika kuchunguza jinsi jamii halisi za mwandishi zinavyozalisha fasihi katika mahali na wakati maalum kihistoria. Ulitusaidia kutafuta data inayohusiana na chimbuko la maudhui ya *Dhifa.*
3) Dhamira ya waandishi huathiri maendeleo ya historia ya kazi ya fasihi inayohakikiwa pamoja na jamii husika. Mhimili huu ulitusaidia kuchunguza matakwa na matarajio ya kijamii na ya kisiasa yanavyoathiri utunzi na upokezi wa kazi ya fasihi, kutokana na dhamira na maudhui ya mtunzi (Greenblatt, 1980).
4) Muktadha wa chimbuko la kazi ya fasihi husika huathiri uhakiki na ufasili wa matini ya kifasihi. Mhimili huu ulitufaa katika kuangalia chimbuko la maudhui na athari yake katika jamii.
5) Kazi yoyote ya fasihi haina budi kubadilika. Mhimili huu ulitusaidia kuangalia mifumo ya uongozi nchini Tanzania katika nyakati tofauti za kihistoria na namna mifumo hiyo tofauti ilivyoathiri maudhui na uwasilishaji wake.

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

### 1.8.2 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti zinahusu jinsi muundo wa utafiti utakavyotekelezwa na namna utafiti wote utakavyofanyika. Mbinu itumikayo huamua uzito wa data inayotarajiwa kukusanywa na kuchanganuliwa (Kombo na Tromp, 2006). Sehemu hii ilishughulikia: muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, sampuli lengwa, njia za kukusanya data, uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo.

### 1.8.3 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti ndio mwongozo wa utafiti wowote. Muundo ndio mpango na nguzo inayoelekeza mtafiti kuhusu namna atakavyokusanya data yake. Kwa mantiki hii, muundo wa utafiti unarejelea aina ya utafiti utakaofanywa (Kombo na Tromp, 2006). Utafiti huu ulichukua muundo wa kimaelezo. Mbinu ya kimaelezo ilitumika kueleza miktadha ambamo jamii ya Tanzania imepitia kihistoria pamoja na athari zake kwa utunzi. Kadhalika, mbinu hii ilitumika katika ukusanyaji, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti.

### 1.8.4 Mahali pa Utafiti

Utafiti ulifanywa maktabani.Mtafiti alisoma kazi na makala yaliyompa data ya msingi iliyohusiana na mada ya utafiti, suala la utafiti, nadharia teule pamoja na maelezo ya jumla kuhusu yaliyondikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti.

### 1.8.5 Sampuli na Mbinu za Uteuzi Wake

Data iliyohitajika ilitokana na mashairi ya *Dhifa* yaliyoteuliwa kutumia mbinu kusudio. Mashairi ishirini na moja yaliyohusu maudhui ya uchumi, siasa na jamii yaliteuliwa kutumia mbinu kusudio ili kumwezesha mtafiti kupata data toshelevu ya kutimiza

mahitaji ya utafiti huu. Mashairi saba kwa kila kipengele. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006) usampulishaji kusudio hutumiwa pale ambapo mtafiti hulenga kimakusudi kundi fulani analoonelea kuwa lina uwezo wa kuzalisha data zenye sifa na habari anazozihitaji. Orodho (2005) anashadidia kwa kusema kwamba, usampulishaji kusudio ni uamuzi wa mtafiti wa kuteua moja kwa moja idadi ndogo iliyo na uwezo wa kudhihirisha tabia zinazohitajika na utafiti wake. Hivyo, kumwezesha mtafiti kufanya uteuzi wa moja kwa moja ili kupata sampuli itakayowakilisha idadi yote kwa kutoa habari muhimu anayohitaji. Jumla ya mashairi ishirini na moja yalizingatiwa.

### 1.8.6 Mbinu za Kukusanya Data

Data ya utafiti huu ilikusanywa kutokana na usomaji wa kina wa mashairi teule ya diwani ya *Dhifa.* Mtafiti alichagua sehemu za mashairi yenye data iliyohitajika kutosheleza mahitaji ya utafiti. Alinukuu mifano mbalimbali ya mashairi yaliyokuwa na maudhui ya uchumi, siasa na jamii ili kueleza namna ujumbe ulivyowasilishwa.

### 1.8.7 Uchanganuzi wa Data

Katika hatua ya mwanzo kabisa, data iliainishwa kwa kuzingatia aina ya maudhui, uwasilishaji wake na matukio ya kihistoria. Kisha uchanganuzi ukafanywa kwa kuonyesha chimbuko la maudhui, namna yalivyowasilishwa, dhamira ya mtunzi na falsafa yake. Aidha, uchanganuzi uliongozwa na malengo, pengo lililonuiwa kujazwa na mihimili ya nadharia.

### 1.8.8 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo ya kinathari. Mifano mwafaka ya maudhui, namna yalivyowasilishwa na ubainishaji wa mazingira ya kijamii

na kihistoria yaliyoibua utunzi husika ilitolewa. Uwasilishaji ulifanywa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia ya utafiti.

## 1.9 Muhtasari

Masuala yaliyojadiliwa katika sura ni ya kikaida na yalihusu msingi wa utafiti. Haya ni pamoja na utangulizi wa sura yenyewe, usuli wa utafiti, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka ya utafiti. Sura hii pia iliangazia yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti pamoja na msingi wa nadharia. Istoshe, ilishughulikia mbinu za utafiti zilizotumiwa katika kutekeleza na kufanikisha utafiti huu. Sura hii ni muhimu kwa kuwa ilitujengea msingi na muktadha ambamo utatifi wote ulifanywa. Sura inayofuata ilihusu historia, mazingira na falsafa ya mtunzi.

# SURA YA PILI

## Historia, Mazingira na Falsafa ya Mtunzi

### 2.0 Utangulizi

Sura hii iliangalia historia na mazingira ya mtunzi pamoja na falsafa yake kwa lengo la kuelewa msingi, muktadha na chimbuko la mashairi ya diwani ya *Dhifa*. Jambo hili linatokana na sababu kwamba mazingira ya msanii katika ujumla wake pamoja na falsafa yake huathiri namna anavyotunga kazi yake, mwelekeo wake na dhamira pia. Hali hii imebainika kupitia mashairi yaliyoshughulikia masuala ya uchumi, siasa na jamii. Vipengele hivi viwili huupa utunzi mwelekeo na mkondo maalum.

Mazingira ya kihistoria na kijamii huathiri utunzi wa msanii kifani na kimaudhui pamoja na kuupa utungo mwelekeo. Sura hii ilijadili mazingira ya kihistoria na kijamii nchini Tanzania wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni na zaidi sana kuzaliwa kwa Azimio la Arusha kwa matarajio kwamba ulinganishi wa vipindi hivi vitatu katika historia ya Watanzania umetuwezesha kueleza kwa utondoti maudhui na dhamira ya mtunzi na hivyo kutuwezesha kueleza athari ya mazingira ya kijamii na kihistoria katika uwasilishaji wa maudhui ya *Dhifa*.

### 2.1 Mazingira ya Msanii

Mshairi wa Kiswahili, kama alivyo msanii mwingine katika jamii yoyote ile ni zao la jamii hiyo. Mabadiliko yatokeayo katika nyanja zote za maisha kama vile ya kiuchumi, kisiasa na kijamii humwathiri. Masinde (1992). Athari hizi ndizo humpa mshairi hamu ya kutunga kuhusu jambo linalomchoma moyo. Kwa hivyo, wasanii wote ni zao la

kihistoria. Isitoshe mshairi kama mwajamii hawezi kuepuka kuathiriwa na mikinzano ya kitabaka inayojidhihirisha katika jamii hiyo.

Anaendelea kusema kwamba, mwadishi yeyote hawezi kujiepusha kamwe na masuala ya kijamii yaliyomzunguka anapoitunga kazi yake. Hii ni kwa sababu mwandishi ni mwanajamii na anaathiriwa kwa kiasi kikubwa na mambo yale anayopitia maishani, yale anayoambiwa, kuyasoma au kuyashuhudia yakiwakumba wanajamii wenzake. Jambo hili humpa msukumo wa kuyatungia maswala ya kijamii yanayompendeza au hata kumchukiza.

Waandishi wengi hasa wa tenzi huwa wanavutiwa sana kueleza visa vya kihistoria. Tenzi hizi ni pamoja na *Utenzi wa Uhuru wa Tanganyika* na Mwinyihatibu, *Utenzi wa Jamhuri ya Tanzania* na R. Mwaruka, *Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar* na M.S Khatibu, Utenzi wa *Vita vya Uhuru* wake Shaaban Robert miongoni mwa wengine. Karibu waandishi wengi waliotajwa hapo juu na wengineo wameangalia historia nzima ya Tanzania na kutupa picha halisi ya vipindi vyote ambavyo Tanzania imepitia, yaani tangu ukoloni mkongwe wa Kiarabu, Kijerumani na Kiingereza hadi Uhuru na Azimio.

Watunzi hawa wanaonyesha malalamishi yao ambayo kama watunzi na waandishi wengine wa Kiafrika wanaoandika baada ya uhuru wanatupa picha halisi ya mkoloni kama mtu mbaya, mdhalimu, mnyonyaji, mkandamizaji na muoneaji. Nao wanaonyesha madhambi waliyoyatenda wakoloni kutuchukua utumwa na kuuzwa kama wanyama sokoni, kutupiga vita, kutuchomea mashamba, kutulimisha na mambo kama hayo ya kidhalimu. Maneno yenye hisia hizo na historia za watu mashujaa waliopinga udhalimu

huo pia yanapatikana katika kazi za ushairi za waandishi wa siku hizi kama Kezilahabi. Ni dharihi kuwa mashujaa hawa walishindwa na wanahistoria hawana budi kuukubali ukweli huo. Kwa hivyo, ni vigumu kwa wasanii wetu kuubadili ukweli huo wa kihistora, lakini wao huueleza ukweli huo kwa njia ya sanaa.

Hata baaada ya uhuru, waandishi na watunzi wengi walizidi kuonyesha matukio mahsusi ya kihistoria. Waandishi na watunzi walianza kueleza maana ya uhuru, wakaanza kumwangalia mkoloni kwa jicho jipya. Mkoloni ambaye mwanzoni alikuwa baba na mlezi sasa amegeuka kuwa adui na muuaji (Mmbaga, 1978).

Kazi hii ilishughulikia sera ya kikoloni na zile zilizobuniwa baada ya uhuru na Azimio la Arusha la 1967. Ukoloni ulivunja mifumo ya kijamii ya jadi ya Watanzania. Baadhi ya mifumo na sera hizi zilihifadhiwa na kuathiri sera katika Tanzania huru. Azimio la Arusha lilidhamiria kurekebisha na kuondoa athari za kikoloni na hii ilikuwa hatua muhimu sana katika historia ya Watanzania kama ilivyodhihirika katika mashairi teule ya *Dhifa.*

Tuliangalia maisha na falsafa ya mtunzi tuliyemchaghua kumfanyia utafiti. Hii ni kwa sababu tajriba ya mtunzi huathiri mwelekeo wake. Kwa hivyo, historia ya maisha ya mtunzi ni muhimu katika kueleza athari ya kihistoria nakijamii katika uwasilishaji wa maudhui katika utunzi wake. Sura hii ililenga kuonyesha kuwa utunzi wa fasihi, ushairi ukiwemo ni kama kioo cha jamii ulimotungiwa.

## 2.2 Wakati wa Ukoloni

Kipindi hiki katika historia ya siasa ya Afrika Mashariki kinaweza kuwekwa katika mihula mitatu maalum. Muhula wa kwanza, kama asemavyo Ogot katika Anene (1966:438) kinaweza kuitwa 'Enzi ya Uhifadhi' hasa 1886-1914. Katika kipindi hiki, koloni za Afrika Mashariki zilizochukuliwa kama msingi wa fahari ya taifa na umuhimu wao ulithaminiwa katika mkabala wa mng'ang'ano wa kisiasa baina ya mataifa makubwa. Uingereza na Ujerumani ni mataifa yaliyochukuliwa kwamba kazi yao ya kwanza ni kuhifadhi sehemu zao za utawala dhidi ya vitisho kutoka nje.

Muhula wa pili ulikuwa kati ya 1918-1939. Hiki ni kipindi kilichoshuhudia wakoloni wa Uingereza wakiwatumia Waafrika katika utawala wao. Pia, kulitokea uhusianowa karibu kati ya mataifa ya Afrika Mashariki. Maongozi ya sera ya utawala wa Waingereza yalikuwa ya mabadiliko ya polepole. Muhula wa tatu ulikuwepo kati ya 1945-1962, hasa baada ya vita vikuu ya pili ya dunia. Wakati huu unajulikana kama 'kipindi cha uhuru'. Waafrika walipigania uhuru.

Katika kipindi cha ukoloni, wakoloni polepole walitumia hila zao ili kuwafanya Waafrika wapuuze na kudunisha utamaduni wa Kiafrika. Kwa upande mwingine, wakoloni walifanya Waafrika kuutukuza utamaduni wa kikoloni, hivyo kuzamisha mirija ya kuendelea kuwategemea hadi sasa. Fanon (1963:261).

Utawala wa kikoloni uliathiri kwa njia mbalimbali utawala wa kiasili. Kwa mfano, jamii za kiasili zilizotawaliwa na wafalme na ambazo hazikupinga utawala wa kikoloni zilihifadhi sehemu kubwa ya utawala huo. Wakoloni pia walianzisha vituo vya kifalme

mahali ambapo havikuwepo ili kuwatuza vibaraka wao wa Kiafrika, mfano ufalme wa Sukuma kaskazini mwa Tanzania.

Wale waliopinga utawala wa kikoloni kama Wahehe na Wanyamwezi walipoteza himaya zao. Gray katika Anene (1966) atuarifu kuwa upinzani mkuu ulitokea kusini mwa Tanzania ambapo Wayao wakiongozwa na Abushiri na Wahehe wakiongozwa na Mkwawa walipinga utawala wa kikoloni. Hali hii ilimfanya Kezilahabi kutunga shairi la 'Mkwava' ili kusifu juhudi za kizalendo za Mkwava wa Uhehe aliyepigania uhuru hadi mwisho.

Athari nyingine ya utawala wa kikloni ilikuwa kwamba watu wa asili tofauti walijumuishwa pamoja ili kufanya utawala wa kikoloni kuwa rahisi. Hili lilihujumu utawala wa kiasili. Katika hali kama hii, watunzi walitunga mashairi kulilia utamaduni wa Kiafrika uliosahaulika.

Kulitokea sera mpya ya kikoloni ambapo kulikuwa na mahakama ya wakoloni na nyingine ya Waafrika. Sheria za wakoloni zilikuwa kali kwa wenyeji na zilijaa maonevu ambapo Waafrika walihangaishwa bila sababu kwa kutumia polisi. Hali hii iliwaathiri watunzi kiasi kwamba walitunga mashairi kulalamika kuhusu utawala katili na wenye mabavu. Mfano, shairi la 'Upepo wa Wakati' katika *Kichomi*. Mtunzi anasema:

Hivyo ndivyo ulimwengu ulivyo
Na hivyo maisha ya binadamu
Wanapanda na kushuka
Wakisukumwa na upepo wa wakati.
Tazama wanapojinyakulia madaraka

Kama mzamaji, mguu wa rafikiye, ashikavyo!
Wanavyoshika pesa kama mtoto
Na picha ya bandia
Au askari mwehu na bunduki yake
Na kutunyamazisha!

Viongozi Waafrika walioteuliwa katika utawala wa kikoloni walikuja kuwa vifaa vya utawalawa kikoloni. Walihitajika kutekeleza kila kitu kwa utii bila kusaili matendo yao. Kwa mfano, kukusanya kodi, kutoa chakula, kutoa watu wa kufanya kazi za shokoa na wengine kuingizwa katika jeshi la kikoloni. Machifu wa kikoloni waliathiri utaratibu wa kiasili kuhusu siasa, uchumi na hata maisha ya kijamii kwa jumla. Hawakuwa na huruma katika utekelezaji wao, lao lilikuwa ni kuridhisha na kufuruhisha 'mabwana' zao. (Rodney, 1972).

Nchini Tanzania, Wajerumani walitawala koloni yao kupitia Maakida waliotuzwa kwa kupewa sehemu ya kodi waliokusanya, mshahara kila mwezi, kupewa mashamba na kuruhusiwa anasa fulani. Jambo jingine kuhusu utawala huu ni unyonyaji kiuchumi. Walianzisha mashamba makubwa ya mimea kama vile pamba na mkonge. Pia, walihimiza upataji wa wafanyakazi kwa urahisi na wakati mwingine kwa kuwalazimisha. Hawakuheshimu utu wa mwafrika. Utawala huo ulitwaa kwa nguvu mashamba ya Waafrika yenye rutuba na kuwalazimisha kwenda kwenye 'risavu' ambapo ardhi haikuwa na rutuba. Isitoshe, Waafrika wengi walilazimishwa kuwa maskwata katika ardhi yao. Licha ya haya, walitozwa kodi na mateso. Jambo hili liliwasukuma kufanya kazi katika mashamba ya wazungu.

Waafrika walilazimishwa kufanya kazi ya ujenzi wa barabara na reli. Watunzi walilalamikia hali kama hizi kupitia utunzi wa mashairi. Pesa zilizoletwa katika koloni ya Tanganyika ziliwalazimu Waafrika kutupilia mbali njia zao asili za uchumi. Mishahara waliyopewa ilikuwa habamno kiasi cha kutowawezesha kukimu mahitaji ya familia zao. Hali hii iliwafanya vijana kughuria mijinina katika mashamba ya Wajerumani kutafuta kazi. Hali hii iliathiri mapato ya kilimo katika sehemu za mashambani. Ubinafsi ulizuka na kuvunja maisha ya ujima ya Watanzania. Hali ni wazi katika shairi 'Enzi za Mapambano' katika *Kunga za Ushairi*. Mulokozi anasema:

Ndugu ajuayena wewe usiyejua
Shida zimepanda bei
Maisha yananunuliwa na mauti pia
Hivyo ni vibaya lakini ni vizuri
Ni mwito wa mapambano.

Uchumi wa kikoloni uliwaathiri Waafrika kwa njia mbalimbali. Ulihimiza ubinafsi ambao uliambatana na unyonyaji usiojali utu. Ubepari ambao uliambatana na ulimbikizi wa mali kwa kuwanyonya waliozalisha mali hiyo ulizuka. Pia, mabepari walitumia hila ili kuwazugazuga wanyonge na kuamwa jasho lao. Hali hii ya ubinafsi ilivunja hali ya kiutu ambayo Waafrika walikuwa nayo katika ujima. Hali hii inadhihirika katika shairi la 'Maombolezo ya Mtu Maskini' katika diwani ya *Malenga wa Bara* ifuatavyo:

….simba wa ubepari anapachika makucha,
Na kunitia mashimo mifukoni
Nami nabakia kutangatanga
Na kupepesuka kama utete tufanini

....shubiri ya ufakiri imezimua sukari yangu ya maisha
Na miiba ya dhuluma imeitoboa mikono yangu nisiweze kujikimu
Nimekuwa mtumwa katika dunia huru
Fakiri katika jumuia ya tajiri
Na chungwa la kuswagwaswagwa
Kama sarakasi katika uzi!

Kijamii, utamaduni wa Waafrika ulipuuzwa na kudunishwa. Shughuli zote za kimila zilipigwa marufuku. Kwa mfano, kuabudu miungu, kuoa wake wengi, elimu ya kienyeji, vyote vilipuuzwa kwa manufaa ya utamaduni wa kizungu ambao ndio chanzo cha ukoloni mamboleo.

Kulingana na Ogot (1974) na Ilife (1969), maasi ya Maji-Maji ya mwaka 1905 yalikuwa utesi dhidi ya unyonyaji na unyang'anyaji wa Kijerumani. Maasi haya yalisambaa katika sehemu nyingi. Japo yalizimwa mwaka 1907, yalikuwa na ishara ya kuwaunganisha Waafrika dhidi ya sera ya kikoloni yenye udhalimu na unyanyasaji. Brett (1973:11). Wakoloni walivamia Waafrika wakawafanya watumwa na kuwaweka chini ya utawala wao. Kadhalika, walinyakua mali yao kwa kuwaua, kuwatesa na kuwahadaa. Anaendelea kueleza kuwa, ukoloni ndio uliozorotesha kustawi kwa Afrika nzima. Maendeleo yangepatikana tu kupitia kujikomboa kutoka kwa mfumo wa kibepari ili kuleta mfumo wa kijamaa. Ameumulika ubepari kama mnaso usio na utu na ambao unaharibu uhuru na kujitosheleza. Ni katika mtazamo kama huu ambapo shairi la 'Kifo cha Mende Wekundu'katika *Karibu ndani* lilitungwa. Kezilahabi anasema:

Kifo cha mende sharti miguu juu.

Kichwa ukikanyage kipasuke usikie.

Na kisha wengine usiku mchana uwasake.

Mpaka watakapokwisha. Usiseme nao.

Ubepari, ubwanyenye na umwinyi vimeshutumiwa na kupigwa vita na Kezilahabi. Waliopigania uhuru walitarajia kuwa mifumo ya kikoloni ingebadilishwa uhuru upatikanapo lakini hawakufaulu. Kilichobaki ni kuzinduka na kujikomboa.

**2.3 Kabla na baada ya Azimio la Arusha**

Tanzania ilipojipatia uhuru, ilikuwa muhimu kwamba iwena sera mpya kisiasa, kijamii na kitamaduni ili malengo yake ya kupigania uhuru yatimizwe. Lakini sera za Tanzania huru kabla ya Azimio hazikufanikiwa. Khatib (1987) anasema kuwa, washairi wengi wamazungumzia Azimio la Arusha kwa kulitafsiri katika mielekeo mbalimbali. Mashairi mengi yaliandikwa kuhusu Azimio la Arusha lakini kabla ya kutaja mifano hiyo ni vyema tuone sababu za msingi zilizosababisha Azimio la Arusha kuzaliwa. Baadhi ya sababu hizo ni za ndani ya nchi na zingine ni za nje ya nchi. Mosi, kulikuwa na nguvu na mivutano ya kijamii iliyopevusha mimba ya Azimio la Arusha. Hii ni mikinzano ya kitabaka iliyokuwepo Tanzania bara mara tu baada ya uhuru. Anaendelea kusema kuwa, walikuwepo wachache ambao waliitwa 'naizesheni'au 'wabenzi' dhidi ya kundi kubwa la 'akina kabwela'. Mikinzano hii iliwavunja moyo 'akina kabwela.' Baada ya uhuru waliopigania wote dhidi ya mkoloni ukiwa sasa unafaidi wachache.

Sera ya Tanzania-huru pia haikufanikiwa kutokana na sababu za nje. Kulikuwepo na nguvu nyingine, hasa katika 'medani' ya biashara ya kimataifa. Khatibu (1987) anaendelea kusema kuwa, katika kipindi kifupi cha uhuru serikali ilishindwa kuleta

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

maendeleo ya haraka kwa watu wake baada ya kukosa misaada iliyotarajiwa kutoka nje. Bei ya mazao ya pamba, korosho na mkonge iliporomoka ghafla katika soko la kimataifa. Wakati huo, malighafi na vitu vilivyotengenezwa viwandani kutoka nje ambavyo vilihitajika vilikuwa ghali mno. Mabepari chwara kama awaitavyo Khatib, walikuwa wakitia fora nchini kwa msaada wa mfumo wa ukoloni mamboleo. Ukoloni mamboleo ulizamisha mirija yake nchini katika kuhodhi faida ya uchumi kama vile mabenki, viwanda, machimbo ya madini, mashamba makubwa na biashara ya nje na ndani.

Kilio cha Watanzania walipoona kuwa nchi yao ilikuwa imesalitiwa kinabainika katika mashairi kama vile 'Mgomba', 'Hatumuoni' ya Kezilahabi katika *Kichomi* kama ifuatavyo:

> …mti wa mji umelala chini: hauna faida tena,
> Baada ya kukatwa na wafanya kazi
> Wa bustani kwa kusita
> Chumbani hakuna kitu
> Isipokuwa upepo fulani wenye huzuni utingishao
> Wenye hila waliokizunguka kitanda na kulia
> Machozi yenye matumaini yapiga
> Mbiu hatari ya magovi nyumbani
> Magovi…

Mashairi ya aina hii yanaonesha tanzia ya uhuru uliosalitiwa na baadhi ya viongozi ambao walijitenga na kuwasahau wananchi waliopigania uhuru wao. Badala yake, walishiriki katika mfumo wa kinyonyaji wa ukoloni mamboleo kuzidi kuwanyonya na kuwakandamiza wananchi wa tabaka la chini.

Mabadiliko yaliyotokea Zanzibar chini ya Abeid Karume katika kipindi kifupi baada ya uhuru ambapo wananchi wa Zanzibar walishuhudia mapinduzi kisiwani. Vilevile, walikuwa tayari wamepatiwa huduma za bure za kiafya, elimu, maji na nyumba. Pia, njia kuu za uchumi kama vile mabenki, viwanda, ardhi na mashamba zilikuwa mali ya umma. Mwelekeo wa sera ya itikadi ya serikali na chama chake cha Afro-Shirazi vilionyesha nia ya ujenzi wa taifa la usawa, haki na ujamaa.

Baada ya Tanzania kujipatia uhuru wake mwaka wa 1961 kutoka kwa Waingereza, nchi hii ilifuata mfumo wa uchumi wa kibepari. Matokeo ya mfumo huo hayakuwafurahisha viongozi wa Tanzania, (Boesen, 1977:14). Chama cha TANU kilichotawala Tanzania bara kilionelea kwamba kulikuwa na haja yakuanzishwa siasa mpya ya ujamaa ambayo ingeleta maongozi tofauti na yale ya hapo awali.

Katika mapambazuko ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha, washairi wengi walilipokea Azimio hili kwa shangwe, hoihoi, na nderemo. Ilitarajiwa kuwa Azimio lingeleta matumaini kwa wanyonge. Azimio lilitarajiwa kuwa mwokozi wa wavuja-jasho. Mulokozi na Kahigi, washairi wachanga katika uwanja huu wakati huo walilifananisha Azimio na jua ambalo lingemulika njia na kuwa ngazi ya kupandia wanyonge:

Nimeona Jua la Dhahabu
Katika mji wa Arusha
Likamulika njia
Nisiweze kujikwaa (*Malenga wa Bara*, Uk.18: 1976).

Katika mwaka 1967, Azimio la Arusha lilitangazwa. Huo ndio ukawa mwanzo wa siasa mpya ya ujamaa katika historia ya Tanzania. Siasa hiyo ilidhamiria kuwafaa watu waishi pamoja katika vijiji na kufanya kazi pamoja na manufaa ya wote. Kadhalika, siasa hiyo ilikusudia kuleta usawa wa kiuchumi miongoni mwa wananchi na kuondoa kila aina ya unyonyaji na unyanyasaji. Kulikuwepo na matarajio makuu ya ufanisi kiuchumi, kisiasa na kitamaduni.

Azimio lilidhamiria kuonyesha kwamba uhuru unamaanisha kujitegemea. Kwa hivyo, maendeleo ya nchi huletwa na watu wake. Nguzo zake ni watu, mashamba, mashauri mema na uongozi bora. Elimu ambayo ingetolewa ingeenda sambamba na matakwa ya nchi pamoja na malengo ya kijamii. Ilinuiwa kujenga Tanzania huruyenye usawa na heshima kwa ubinadamu kwenye misingi ya Kiafrika (Rodney, 1972:262).

> Muundo wa elimu katika mfumo wa elimu
> ya jadi ya Kiafrika ulikuwa unazifaa jamii
> hizo katika kupambana na mazingira yao.

Mwandishi anaeleza kuwa, elimu hiyo ilitokana na mfumo wa kiuchumi, kisiasa, na kijamii wa jamii husika. Ingezuia majaribu ya usodawi au usafihi ambao huwafanya walioelimika kuwapuuza wale walio chini yao kwa kuwaona duni. Kwa mfano shairi la 'Sima na Mayayi' katika *Malenga wa Bara.* Mulokozi anasema:

> Kumbuka zama hizo
> Tulipoishi mimi na wewe
> Mama yako na wadogo zako

Je tulikoga mara ngapi kwa juma

Unakumbuka?...

Hata hivyo, utekelezaji wa wa siasa hiyo haukuwa rahisi. Kulikuwa na matatizo mengi yaliyoukumba mpango huo kama asemavyo Boesen (1977) kuwa baadhi ya viongozi mikoani hawakujua malengo ya siasa hiyo. Viongozi hawa hawakuchaghuliwa kwa madhumuni ya kutekeleza mpango huo. Kwa hivyo, uongozi katika utekelezaji wa siasa ya ujamaa waonekana kutokuwa na mwelekeo mzuri. Mfano huu ni wazi katika shairi la 'Uliza Wanaojua' katika *Kichomi.* Kezilahabi anasema:

Wako wapi waliokuwa viongozi zamani
Waliotoa hotuba ujamaa kuupigania?
Sasa wamestaafu ndio wafuga kuku
Ndio wenye majumba ubepari kurithisha!
Kama wewe hujui, uliza wanaojua
Ukweli watakwambia.
Au hujaona makabila wenye mashamba.
Matrekta yanafukuta na vumbi kutimuliwa!
Zungumza juu ya vijiji watakuonyesha kidole
'Pilipili usiyoila yakuwashiani!'...

Tangu Azimio litangazwe washairi wengi akiwemo Kezilahabi wamelizungumzia katika nyanja tofauti na walikuwepo katika zile awamu tatu za mabadiliko ya kisiasa tokea kabla ya uhuru, baada ya uhuru na baada ya kuzaliwa kwa Azimio la Arusha. Ni bayana kuwa, tatizo kuu la Tanzania huru lilikuwa kule kuwepo kwa matabaka ya wanyonyao na wanyonywao. Hali hii ilisababisha Azimio la Arusha kama ilivyotajwa hapo juu. Kisha kukawa na shangwe katika kulikaribisha Azimio, halafu kukatokea udhaifu fulani katika

harakati za utekelezaji wa itikadi ya siasa ya ujamaa pamoja na kuzihusisha sehemu muhimu za uchumi wa nchi. Kwa hivyo, ubepari uliendelea, unyonyaji na unyanyasaji pia. Hivyo, kuna kutoridhika na kukata tamaa. Hali hii inajitokeza katika utunzi wa Kezilahabi kama itavyobainika baadaye.

**2.4 Mashairi katika Kipindi cha Uhuru na Azimio la Arusha**

Kipindi hiki kinaanza mwaka wa 1961 na kuendelea. Katika kipindi hiki, mashairi mengi yalikuwa ya kushangilia uhuru na kuwapongeza wapigania uhuru kwa kazi yao nzuri. Mashairi ya aina hiyo yanaonekana katika mashairi marefu kama vile; *Utenzi wa uhuru wa Tanganyika (1967)* ulioandikwa na Mwinyihatibu Mohamed Amiri, *Utenzi wa Jamuhuri ya Tanganyika (*1967) ulioandikwa na Ramadhani Mwaruka, *Utenzi wa Uhuru wa Kenya* (1972) ulioandikwa na Salim A.Kibao.

Mwaka wa 1967, Azimio la Arusha lililoambatana na siasa ya ujamaa na kujitegemea lilitangazwa na hivyo kuleta sura mpya ya ushairi wa Kiswahili. Mashairi ya kijamaa yaliyosifia Azimio la Arusha na siasa ya ujamaa na kujitegemea yaliibuka. Miongoni mwa mashairi hayo ni *Mashairi ya Azimio la Arusha* (1971) yaliyohaririwa na Grant Kamenju na Farouk Topan. Fani na mtindo mpya wa ushairi wa kimajibizano ulianzishwa ambao ulipewa jina ngonjera. Mfano mzuri wa ushairi huo wa kimajibizano unaonekana katika Ngonjera za *UKUTA* za Mnyampala 1970. Ngonjera hizi zilitumiwa sana na wanasiasa kueneza siasa ya ujamaa na kujitegemea. Hata hivyo, Mmbaga katika makala yake iitwayo '*Ngonjera: Historia yake Simulizi hadi Andishi* iliyopo kwenye jarida la Kiswahili anaeleza kuwa fani hii ya ngonjera imekuwepo katika jamii mbalimbali hata kabla ya wakati huo.

Mmbaga anathibitisha kuwa ushairi andishi wa Kiswahili unachimbuka katika ushairi simulizi wa Kibantu uliokuwepo tangu kale. Hoja yetu hapa ni kuwa, hata kama ngonjera simulizi zimekuwepo kwa muda mrefu ngonjera andishi zilianza kuonekana katika wakati huu. Ushairi mwingi wa wakati huu ulikuwa wa kikasuku.

Kasuku ni ndege mwenye tabia ya kuiga kila sauti anayoisikia bila kujua maana yake na madhara yake. Hivyo, kusema mashairi ya kikasuku tunamaanisha kwamba mashairi yaliyosifia kila jambo lililosemwa na wanasiasa bila kudhihirisha kufaa kwake.

**a) Kipindi cha Vita vya Kagera na Ugumu wa Maisha**

Katika kipindi hiki, palianza kuibuka hali ya kukata tamaa miongoni mwa watu kutokana na matamanio na matarajio yao baada ya uhuru kutotimizwa. Baada ya uhuru, watu waliamini kwamba maisha yao yangekuwa mazuri zaidi na kungekuwa na neema zaidi lakini hali haikuwa hivyo. Hapa ndipo ulipoibuka ushairi wa kihakiki ambao uliikosoa jamii.

Ushairi wa kipindi hicho ulionesha hali halisi ya jamii katika nyanja mbalimbali kama vile hali ya kisiasa, hususan hali ya uongozi mbaya, ukiritimba, kujilimbikizia mali, uhujumu, uchumi na kadhalika. Washairi pia walianza kutathmini upya kuhusu Azimio la Arusha na siasa ya ujamaa na kujitegemea kama vilikuwa na maana yoyote. Hapa ndipo palipoibuka mashairi kama vile

'*Miaka Kumi Baada ya Azimio la Arusha*' (1977) yaliyohaririwa na Abdilatif Abdalla. Mashairi hayo yanaonyesha jinsi hali ya kiuchumi na kijamii ilivyokuwa mbaya. Yanaonyesha jinsi wananchi walivyokuwa wanapata taabu kupata mahitaji muhimu.

Mashairi mengine ya mkondo huu ni ya Kezilahabi (1974) *Kichomi*, (1988) *Karibu Ndani* ya Kahigi na Mulokozi (1976) *Malenga wa Bara* na ya Mohamed Seif Khatib (1988).

Watunzi hawa walipendekeza mbinu mbalimbali za kuondokana na matatizo hayo ikiwa ni pamoja na kuwahimiza wananchi kuungana ili kutatua matatizo yao na kuchukua hatua. Aidha, yalipendekeza pia viongozi kuwajibika ama kuwajibishwa ili kuepusha matatizo zaidi. Hali hiyo inaonekana katika mashairi ya *Fungate ya Uhuru* (1988) na ya Mochiwa (1988) *Mvumilivu Hula Mbivu*. Mochiwa anasisitiza kwamba huu si wakati wa wananchi kuwavumilia viongozi wasiofaa maana mvumilivu hula mbivu.

Kwa ujumla, watunzi hawa wanataka ujenzi wa jamii mpya ambayo itakuwa na haki, uchumi imara, jamii iliyojikomboa kiutamaduni, yenye watu wazalendo, yenye umoja, usawa na utu na ambayo ina viongozi bora. Kwa mfano, Kezilahabi katika diwani yake ya *Karibu Ndani* shairi lake la kwanza kabisa liitwalo '*Chai ya Jioni*' anabainisha maovu haya ya viongozi. Katika shairi hili, mshairi anaonyesha jinsi viongozi wanavyojisahau wakiwa madarakani. Katika kujisahau kwao hawajui ya kwamba kuanguka kwao kwaja. Anasema:

> Wakati tunywapo chai hapa upenuni
> Na kuwatazama watoto wetu
> Wakicheza bembea kwa furaha
> Tujue kamba ya bembea yetu
> Imeshalika na imeanza kuoza
> Na bado kidogo tutaporomoka…

Hivyo, anawaasa kuwa ni vyema wahakikishe kwamba kabla hawajaondoka madarakani wafanye mambo yanayokubalika katika jamii. Mashairi mengine ya mkondo huu katika diwani hii ni pamoja na shairi la pili kitabuni '*Mkesho*', la tatu '*Matumaini*' na mengineyo mengi. Katika shairi la '*Mkesho*' mwandishi anabainisha kwamba wakati watu wanateseka wakisubiri maendeleo viongozi wanaishi maisha ya kifahari.

Katika shairi la '*Matumaini*' mtunzi anabainisha jinsi Waafrika waliokuwa na matumaini makubwa wakati nchi zao zilipopata uhuru kuwa viongozi wa Kiafrika wangewaletea maendeleo, walivyokata tamaa na kukosa matumaini kabisa. Kwa ujumla, mshairi huyu amesawiri sana hali ya kukata tamaa iliyokuwepo wakati huo. Hata hivyo, izingatiwe kuwa, mashairi haya yanaweza kuchambuliwa kwa namna nyingine na kupewa dhamira nyingine.

Ngonjera za *UKUTA* zina mashairi ambayo msanii ameweka safu maalum yenye mashairi yanayohusu elimu na utamaduni. Katika safu hii, ametunga mashairi mengi ambayo yanahimiza ukombozi wa kiutamaduni. Miongoni mwa mashairi hayo ni pamoja na '*Utamaduni Kitu Gani* na '*Kiingereza Lugha Nzuri?*' Katika shairi la '*Utamaduni Kitu Gani*'msanii anaielimisha jamii kuhusu suala nzima la utamaduni wa Kiafrika na kuwataka wauheshimu utamaduni wao maana ni bora. Katika shairi la '*Kiingereza Lugha Nzuri*' msanii anahoji uzuri wa lugha ya Kiingereza. Katika shairi hilo, anawakejeli wanajamii wanaoona kwamba kujua Kiingereza ndiyo usomi na ujuzi wa mambo na kuwakumbusha kuwa Kiswahili ni lugha inayojitosheleza na lugha ya usomi pia. Kwa kusema hivyo, msanii alikusudia kuikomboa jamii kutokana na ukoloni.

**2.5 Kumhusu Mtunzi Euphrase Kezilahabi**

Euphrase Kezilahabi alizaliwa katika kijiji cha Namagondo katika kisiwa cha Ukerewe tarehe 13-4-1943. Alielimishwa katika seminari ya kikatoliki ya Nyagezi Junior kutoka darasa la kwanza hadi la kumi na nne. Alijifunza falsafa za kinadhifu za dini, lugha ya kilatini mbali na masomo mengine. Baada ya kidato cha sita, alitoka seminari kwa sababu tayari kaka yake alikuwa padre hivyo wazazi wakamshauri asifuate mkondo wa kakake. Alijiunga na chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo alisomea ualimu, lugha na fasihi. Alipohitimu Chuo kikuu mwaka 1970, aliajiriwa katika shule ya sekondari ya Mzumbe na baadaye huko Mkwawa mwaka wa 1971. Baada ya muda, Kezilahabi alijiunga na Chuo Kikuu cha Wisconsin Marekani, ambapo alifuzu kwa shahada za uzamili na uzamifu. Tasnifu yake ya uzamili ilihusu riwaya za Shaaban Robert. Shahada ya uzamifu ilihusu fasihi ya Kiafrika na fasihi linganishi. Masomo haya yalipanua ufahamu wake wa maisha pamoja na maswala ya kifasihi ya kilimwengu.

Baba yake alikuwa mkuu wa kijiji ambaye alikuwa akitoa ushauri na kuamua kesi zilizohusu maisha ya wanakijiji, mbali na kufanya juhudi za kuleta maendeleo kijijini. Kazi muhimu ya kijijini mwao ilikuwa ukulima na ufugaji. Hali hii imemwathiri kiasi kwamba hujishughulisha na maisha ya shamba katika uandishi wake. Anawatazama wasomi jinsi wanavyohusiana na wanajamii wengine. Licha ya kuwa msomi, yeye hupenda kushirikiana na wanakijiji nyumbani katika shughuli na sherehe zao anapojikuta huko. Haya yote yanadhihirika katika uandishi wake.

Maisha ya mwanadamu ni swala alilojishughulisha nalo sana mwandishi huyu katika kazi zake za kisanaa. Analiangalia swala hili katika mikabala miwili, wa mtu binafsi na wa

jamii. Anamchunguza mtu katika hatua zote kama vile kuzaliwa, ujana, malezi, ndoa, uzee hadi kifo huku akijaribu kufumbua fumbo lililoko katika kila mojawapo ya hatua hizi.

Kama asemavyo Mulokozi (1983) mtu hupata utu wake katika jamii, hivyo hawezi kuishi katika upweke pasi na binadamu wengine. Akiendeleza wazo hili Mulokozi anasema:-

> Jamii ina vikwazo miiko na masharti yake yanayoiongoza na kudumisha kanuni za jamii wakati mwigine humfunga mtu binafsi au kuingilia matakwa yake na shughuli zake za kujinuifanisha, kujiendeleza na kujitafutia furaha. Je, wakati utashi wa mtu binafsi unapogongana na utashi wa jamii yake, mtu binafsi anao uhuru na hiari kiasi gani? Kipi kikuu mtu au jamii? Kwa jumla maisha au matendo ya jamii au (tabaka za jamii ) na ya mtu binafsi yana sababu, kusudi au maana gani kwa jamii na kwa mtu binafsi?

Kezilahabi ameshughulikia maswala ya utamaushi, falsafa ambayo imemwathiri kwa kiwango kikubwa katika mtazamo wake wa maisha na uandishi wake. Mengi kuhusu falsafa hii alijifunza akiwa chuoni ambapo aling'amua kwamba jamii ina vikwazo, miiko na masharti yake yanayoiongoza na kuidumisha.

Wahakiki wengi wa kazi za sanaa za Kezilahabi wanaafikiana kwamba kuna maswala kadha yanayojitokeza katika kazi hizo. Wahakiki hawa ni kama vile, Mulokozi (1983). Maswala yenyewe ni, maisha hasa ni nini na yana maana gani? Ni nini hasa umuhimu wa maisha ya binadamu ikiwa hatima yake ni kifo? Maana ya uhuru ni nini? Mtu binafsi ana uhuru ganina ipi mipaka ya uhuru huo? Kuna uhusiano gani kati ya mwanajamii na jamii

yake? Ni ipi tafsiri ya mapenzi na kuna uhusiano gani baina ya mwanamume na mwanamke kimwili na kindoa? Ni nini shida za watu wenye vyeo namadaraka na upotofu wao kikazi na kimapenzi? Ni mikinzano na mgogoro gani ya kitamaduni ipo baina ya ujadi unaofifia na usasa unaochomoza vijijini na mijini? Malezi ya watoto yana matokeo yapi? Mbona kuna uzazi na ugumba? Elimu ya kimagharibi ina athari zipi kwa msomi?

Ni kwa mantiki hii ambapo tulishughulikia namna ameyawasilisha maudhui yake katika mashairi teule ambayo tuliyachambua katika diwani ya *Dhifa.* Katika utunzi wake, Kezilahabi amebainisha kwamba mazingira ya kihistoria na ya kijamii ndiyo yanayounda hulka ya mtu. Mtunzi pia ametaja athari zilizoletwa na elimu ya kikoloni kuwa zenye kutumikia uchumi wa kibepari, kujisahau, kujidharau, kutamani uzungu, kujichukia, kujidunisha, kuchukia chochote cha Kiafrika na kumfanya Mwafrika mtumwa.

Hali kadhalika, Kezilahabi anashughulikia swala la maana ya maisha katika utunzi wake. Ameyadhihirisha kama adhabu kali, yasiyo na furaha ila huzuni tu. Ameonyesha kwamba binadamu hana chochote cha kujivunia. Maisha ya binadamu yamejaa ghururi. Kwa hivyo, hayatakuwa shwari. Anahimiza kwamba dunia ni kitu ambacho mwanadamu hapaswi kukitegemea kwani ni kitu kisicho na maana.

Kuhusu uhuru wa mtu binafsi katika jamii, mtunzi anaonyesha katika kazi zake kuwa mtu hana uhuru wa kufanya lile alitakalo na vile apendavyo ikiwa jambo hilo linakinzana na matakwa ya na matarajio ya jamii yake na pale ambapo matakwa ya mtu binafsi yanafarikiana na ya jamii basi mtu ndiye huumia. Pia, anaonyesha kwamba mtu binafsi

hawi huru pale matakwa yake yanapopingana na yale ya jamii yake. Hili ni wazi pale ambapo mtunzi huyu alikuwa Seminari akiwa anaishi chini ya sheria ambazo zilimnyima uhuru wa kibinafsi wa kufanya mambo alivyotaka. Hali hii ya kunyimwa uhuru ilimfanya akatoka Seminari.

Kuhusu furaha, mtuzi ameonyesha kwamba mwanadamu hawezi kupata furaha kamili hapa duniani, kwa sababu hiyo anawashauri wanadamu kuyaishi maisha kama yalivyo kwani kuitafuta furaha ni sawa na kupoteza wakati.

Mtunzi vilevile ameshughulikia swala la ndoa ambapo ameonya kwamba hakuna matumaini katika ndoa za wasomi. Amebainisha kwamba ndoa za kiasili zilifaulu kwa sababu ya heshima, furaha na kuridhiana. Anasuta kule kuandama sera ya maisha ya kigeni ambapo hapana uaminifu katika maisha ya ndoa. Kuna uozo mwingi na ukiukaji wa haki. Kwa mafano shairi la 'Wimbo wa Kunguni', 'Mlima wa Kimombo' na Kitu Nisichokitaka'. Adagala (1980) anaeleza haya kuhusiana na jambo hili:-

> Umalaya aghalabu huwa ni zao la mfumo wa kibepari
> wanawake ambao hawana njia nyingine ya kiuchumi
> hujiuza ili wajipatie pesa za kuendesha maisha yao.

Kinachodhihirika katika dondoo hili ni kwamba, mfumo wa kibepari umeathiri hali ya uchumi. Wanawake ambao hawana ajira wameamua kuiuza miili yao ili wapate pesa za kuendesha maisha yao na familia zao. Hawana njia mbadala ya kujitafutia pato na kujikimu maishani hali ambayo inawasukuma kufanya mambo kama haya. Mwandishi

anasuta malezi mabaya ya wazazi. Vilevile, ameonyesha kuwa dini imeibuka kutokana na kushindwa kwa mwanadamu kupata furaha duniani.

## 2.6 Muhtasari

Sura hii ilibainisha ya kwamba vipindi tofauti vya historia ya jamii huwa chimbuko la kazi za utunzi na vilevile huathiri fani na maudhui ya watunzi. Ilionyesha ya kwamba watunzi wakiwa wanajamii, huathiriwa na matukio katika mazingira yao kwa mujibu wa wakati.

Mazingira huwapa tajriba watunzi na huwa malighafi yao. Namna mtunzi anavyotunga kazi yake hutokana na namna alivyoathiriwa na matukio ya jamii yake, dhamira yake, falsafa yake na imani yake kuhusu suala analolishughulikia na walengwa wake. Sura inayofuata ilishughulikia maudhui ya kisiasa.

Nadharia ya Uhistoria Mpya ilitusaidia katika kuangalia historia ya jamii iliyo chimbuko la diwani ya *Dhifa*. Ilituongoza kuangalia maisha ya mtunzi mwenyewe na namna maisha hayo yalivyo na mchango katika mtazamo na utunzi wake kwa jumla. Hivyo, suala la muktadha wa utunzi limeweza kubainika.

# SURA YA TATU

## Maudhui ya Kisiasa

### 3.0 Utangulizi

Sura hii ilichunguza maudhui ya kisiasa katika diwani ya *Dhifa*. Iliangalia namna mtunzi alivyowasilisha maudhui ya kisiasa na muktadha ulioibua maudhui hayo. Katika kufanya hivyo, sura hii iliongozwa na mihimili ya nadharia ya uhistoria mpya isemayo kwamba muktadha wa utunzi ni muhimu katika kuielewa kazi husika. Kazi ya kifasihi haichimbuki katika ombwe tupu bali huchipuka kutoka kwa tajriba ya maisha ya wanajamii na mtagusano wao kijamii, kisiasa na kiuchumi. (Gakuo, 2014). Isitoshe, jamii ndiyo hujenga mazingira ambayo ni nguzo kuu ya msomaji wa kazi ya fasihina uhakiki wake kwa jumla. Kazi ya fasihi haitenganishwi na historia ya jamii husika.

Sura hii pia ilionyesha kwamba kila fasihi nzuri ni ile yenye kuhimiza, kuboresha au kuimarishwa ujenzi wa jamii imara yenye uadilifu, usawa na haki. Aidha, maudhui ya fasihi yoyote huzalika kutokana na hali ya jamii ilivyo na kwa wakati wake. Sura hii iliangazia dhima ya ushairi katika kuundwa kwa jamii bora nchini Tanzania kwa kuibua hali halisi ya mazingira ya kisiasa.

### 3.1 Shairi: 'Dhifa'

Maudhui ya kisiasa katika diwani ya *Dhifa* yanaweza kuangaliwa kwa kuzingatia harakati za ujenzi wa jamii mpya nchini Tanzania, hasa baada ya Azimio la Arusha. Katika shairi hili, mtunzi anajaribu kuhakiki utekelezaji na kufaulu kwa Azimio la Arusha. Wakati tunapojadili dhamira ya ujenzi wa jamii mpya, ni muhimu kuzingatia na kukumbuka kuwa diwani ya *Dhifa* ilitungwa na kuchapishwa katika awamu ya pili ya

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

uongozi wa serikali ya Jamhuri ya Tanzania. Kwa misingi hii, mawazo yanayojitokeza katika diwani hii, hususan, katika kuzingatia kipengele cha kisiasa, yalihusishwa na hali hiyo.

Shairi hili la *Dhifa* limetungwa juu ya uongozi katika Afrika, hasa Tanzania huru. Kezilahabi anazungumzia wakati wa ukoloni ambapo Wazungu na Waarabu waling'ang'ania na kuligawa bara la Afrika na namna wao walivyosherehekea hali hii.

Kichwa cha hili shairi ni jazanda, mshairi anasema *'Dhifa.'* Hii ni jazanda inayoonyesha kusherehekea kwa mkoloni kwa kufaulu kuzinyakua na kuzitawala nchi mbalimbali za Kiafrika. Mtunzi anasema kwamba ni 'Chakula cha mchana.' Mchana unaashiria kuwa mambo ni dhahiri na yanaonekana waziwazi. Anaendelea kusema kuwa 'Walanchi wameshafika'. Hii ni taswira inayoonyesha kwamba hawa ni wale wakoloni waliokuja kugawana rasilmali za nchi za bara la Afrika na kila mtu amejigawa sehemu yake.

Mtunzi anaendelea kusema:

> Puani mwa Bwana mkubwa
> Kamasi jeupe la chungulia
> Waonao hawaoni
> Ila nzi atuae pale
> Siyo tu kuliona
> Bali kulila kabisa
> Kwa mbwembwe achezesha mbawaze.

Hapa, 'Bwana mkubwa' ni taashira ya kiongozi au tabaka la wale wanaotawala kwa unafiki na 'Kamasi' ni taswira inayoashiria uchafu. Uchafu unaozungumziwa ni dhuluma dhidi ya watawaliwa, uonevu, ukandamizaji, ubaguzi wa rangi, unyonyaji na unyang'anyi wa rasilmali zao. Kimsingi, mfumo wa uongozi ulihakikisha kwamba mataifa ya kikoloni yananufaika kwa vyovyote vile. Kwa njia hii, Waafrika walitumiwa kama vifaa vya kuendeleza mbinu za unyonyaji wa rasilmali zao kwa manufaa ya wakoloni.

Kama njia ya kubainisha uozo huo, Waafrika hawakushirikishwa katika maamuzi muhimu kuhusu uongozi wa bara hili. Kwa mfano, walinyimwa haki ya uraia katika mataifa yao, mifumo yao ya uongozi na uzalishaji mali ikaharibiwa, na himaya zao kuratibiwa upya kama maeneo ya kutoa malighafi kwa viwanda vya ulaya.

Kusema kuwa 'Waonao hawaoni' ni kinaya kwamba hata watu wapaswao kugundua hayo maovu hawayaoni. Wale wanaokaribia na kushiriki mfumo huo wa kibepari wanaukumbatia na kuufurahia. Hii ndiyo sababu mtunzi anasema kuwa 'Nzi atua pale na kulila kamasi'. Inamaanisha hali ya viongozi kufurahia matunda ya uongo wao, kushabikia unafiki wao na kuhongera tija yao. Hili ni wazi mtunzi asemapo 'Kwa mbwembwe achezesha mbawaze.'

Kwa kawaida, nzi hupenda kula uchafu mithili ya kamasi linalozungumziwa katika shairi hili. Kezilahabi anabainisha wale wanaonufaika na mfumo huo. Hawa ni pamoja na mawaziri ambao hupata pesa nyingi, wabunge wanaopewa magari nawaandishi waliopewa kazi. Wakati haya yote yanapoendelea, wanaotawaliwa nao wameketi tu wakitazama kwa kuwa mfumo wa kidhalimu hauwapi fursa ya kuitetea haki yao.

Ilivyo ni kwamba taathira za mfumo wa kikoloni zinajitokeza katika mfumo wa sasa katika umbo la ukoloni mamboleo. Jambo hili linabainika mtunzi anapoeleza kuwa 'Huku matajiri wakisherehekea, maskini wamejikalia tu'. Anasema kuwa 'Wacheza ngoma ni wakulima' kwa maana ya kwamba, miongoni mwa watu walionyonywa ni wakulima na kundi hili la wakulima ndilo linatumika kuwaburudisha na kuwahudumia matajiri. Ni kinaya kwamba wale ambao wanawawezesha viongozi kuendeleza zile shamrashamra ili dhifa inoge ni wananchi wa kawaida.

Kezilahabi anasema kuwa hawa wanyonyaji wameketi kwa starehe na kusherehekea kutokana na shibe waliyo nayo huku watu wa kawaida wakiendelea kuumia. Kwa kusema 'Wapiga picha mso kibali pigeni, mpaambe nzi na kamasi'. Mtunzi anamaanisha kwamba angependa taswira za dhifa hii zijulikane kwa umma, hasa za hawa wanyonyaji na uchafuwake. Kile ambacho mtunzi anataka ni kufahamisha umma kuhusu madhila wanayofanyiwa wanyonge katika mfumo wa kibepari usiojali utu wala haki za kibinadamu. Huku matajiri wanapostarehe, hawawajali maslahi ya wale wanaowawezesha kupata zile starehe na utulivu.

Akiwa kama mwalimu wa jamii, Kezilahabi anawazindua watu wayaone maovu ya ukoloni mamboleo. Anataka watu waone taswira na uovu wa mfumo huo dhalimu. Ufafanuzi unaotolewa katika shairi hili ni kwamba mambo muhimu yaliyotakiwa yatekelezwe hayakutekelezwa kutokana na kujisahau, ubinafsi na mfumo wa kibepari usiojali utu.

Taswira ya viongozi pia inaashiria kule kutotambua kuwa maisha ni mafupi. Kwa hivyo, katika kule kushiba kwao, viongozi, matajiri na wanasisasa wanaishi kwa raha mstarehe katika mfumo wa kitabaka na wanapuuza maslahi yakimsingi ya walio wengi ambao ni wa tabaka la chini.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni mfumo wa kihistoria wa utabaka na ubepari wa kikoloni usiojali maslahi ya walio wengi. Aidha, ni mfumo unaoashiria uzungu weusi. Kwa jinsi hii, kuna hali ya juhudi kabambe kufanywa ili walio wengi wapate kuzinduka na kuzidisha mapambano ili kutetea haki zao.

### 3.2 Shairi: 'Madomo Mapana'

Shairi hili linachora hali ya kusikitisha ya wanyonge kutokana na kuwepo kwa viongozi ambao wanajifikiria wao wenyewe bila kujali maslahi ya raia na nchi wanazotawala. Kwa njia hii, raia wanateseka kutokana na madhila mbalimbali ya viongozi wa mfumo wa kibepari. Mfumo huu kwa kawaida husheheni uonevu, upendeleo, unyonyaji, ukandamizaji na dhuluma. Katika mfumo huu pia, viongozi huhodhi njia zote za uzalishaji mali. Kwa hivyo, walio wengi na ambao ni watawaliwa wananyonywana kukamuliwa jasho lao. Hawafurahii matunda ya jasho lao wala uhuru uliopatikana kwa shida.

Mtunzi anasema kuwa 'Nitafukuzwa mbinguni kwa ushairi wangu mbaya.' Anamaanisha kuwa hata akiteswa kwa kusema ukweli katika ushairi wake, yeye hataogopa. Mbinguni ni pahala panapoaminiwa kuwa penye utulivu, maisha mazuri na yenye tumaini. Kwa

hivyo, mtunzi ametumia mbinguni kuashiria maisha yenye tunu, raha, starehe na kila aina ya uzuri.

Anaendelea kusema kuwa 'Lakini hata motoninitaimba.' Ana maana ya kwamba, hata katika mateso mengi kiasi gani mithili ya yale yapatikanayo motoni au jehanamu, yeye atazidi kusema ukweli. Akiwa mtunzi, amejitolea kuwa mtetezi wa wanyonge ambao wamenyimwa haki na kudhulumiwa na maongozi dhalimu.

Kufuatia uhuru wa kisiasa uliopatikana, mtunzi anaonyesha ya kwamba kulihitajika mabadiliko ya uongozi ili kuwafaidi Waafrika. Kezilahabi amejitokeza kama mwalimu kuwaelekeza wananchi ili wachukue nafasi zao vilivyo. Miongoni mwa hatua za kimsingi ni kupitia mapambano ya kidemokrasia, haki za kijamii, uongozi huru, haki za kibinadamu, uajibikaji na uhuru wa kushiriki katika maamuzi ya uongozi wanchi na utawala mzuri.

Anatumia tashbihi ya wanasiasa kuwa 'kama jizi' kumaanisha ya kwamba viongozi husika ni wezi kupita mwizi wa kawaida. Hii inaashiria kwamba kiwango chao cha wizi kimepita kiasi. Kutokana na uongozi wa ubinafsi na tamaa kupita kiasi, mtunzi anabainisha kuwa mtu akiongozwa na ubinafsi, hajali hata haki za msingi za wanyonge. Haya yanabainika mtunzi asemapo kwamba wana hiari kutumia hila bila kuona haya. Anasema:

> Wanasiasa ni kama jizi
> Lililosukuma mtoto pembeni
> Na kunyonya ziwa la mama

Wakati amelala usingizi usiku.

Kitendo cha kumsukuma mtoto pembeni kinaashiria ya kwamba wanasiasa hawana hisia za kiutu. Kwa kawaida, mtoto hupaswa kulindwa na kunyonyeshwa na mamake. Ni kinaya kwamba wanasiasa hawajali hali ya mtoto. Badala yake wanajali maslahi yao ndiposa wananyonya titi la mama badala kumwachia mtoto anyonye ili asiathirike kiafya. Hii ni taswira ya dhuluma katika jamii. Wanyonge wananyimwa haki yao kwa sababu ya ubahili na inda.

Kumsukuma mtoto pembeni kunamaanisha kuwa viongozi ni katili. Mtoto anafaa kuhurumiwa, kutunzwa vyema na kulindwa. Kitendo cha wanasiasa ni sawa na kuangamiza. Hivyo ndivyo wanavyotendewa raia katika mfumo usiojali haki na utu.

Kumnyonya mama akiwa usingizini ni ishara ya mbinu na hila zinazotumiwa na wanasiasa kuendeleza maslahi yao. Wanasiasa hufanya mambo yao kisirisiri kwa lengo la kujinufainisha. Wao ni walafi na ndiyo sababu mtunzi anatumia 'Madomo Mapana' kama kichwa na kiini cha shairi. Tabia hii ya wanasiasa inaashiria kwamba wanasiasa wamekuwa vikwazo kwa wananchi kwa sababu wanawadhulumu walio wengi kwa kuwanyima haki yao.

Mtunzi vilevile anaashiria kwamba, kifo cha wanasiasa kitatoa suluhu kwa walio wengi kupata afueni. Wananchi pia watajikomboa kutokana na mfumo dhalilishi na nyonyaji. Hii ndiyo maana mtunzi anasema:

> Tumejikomboa na domo
>
> Moja pana…

Dondoo hili linamaanisha ya kwamba wanasiasa ni miongoni mwa vizingiti vikuu vinavyozuia haki na maisha mazuri ya walio wengi. Ni matumaini yake kwamba maongozi mabaya ya wanasiasa yazikwe katika kaburi la sahau. Yeye ni miongoni mwa wengi ambao wamechoshwa na mfumo usiojali haki. Mshairi amejichukulia kuwa miongoni mwa watawaliwa wanaoteseka. Katika harakati za kujenga taifa jipya, anaashiria kwamba watunzi, kama walimu, wana nafasi muhimu katika kuzindua umma kupitia kuelimisha jamii.Wanazindua jamii kutokana na maovu wanayotendewa na viongozi.

Wito ni kuwa watu wajielewe, waelewe wajibu wao na kuchukua nafasi zao katika kurekebisha jamii ili iwe nzuri na yenye maadili mema. Hii ndiyo maana anawapa changamoto wasomaji kuona mbali, la sivyo, hakuna haja ya kushika tama na kujihurumia. Mtunzi anaendelea kushauri kuwa, ikiwa hawana maono ya mbali, hakuna haja ya kukuna vichwa. Yafaa tufikirie na kuchukua hatua katika kurekebisha jamii yetu.

Mtunzi anahitimisha kwa kusema ya kwamba nchi imekamuliwa na Wazungu na Waarabu. Raia sasa wananyonywa kupita kiasi. Baada ya kunyonywa, kilichobaki ni umaskini. Kwa hivyo, mtunzi anatoa wito kuwa yeyeametekeleza wajibu wake kwa kumulika maovu yanayokumba jamii kutokana na maongozi mabaya. Kinachofuatia sasa ni wajibu na jukumu la raia wenyewe kuchukua hatua mwafaka ili kujenga jamii mpya yenye maendeleo, haki na usawa kufuatia Azimio la Arusha.

Uchambuzi wa shairi hili ulikita katika muktadha wa Azimio la Arusha ambalo lilikuwa tukio kuu la kihistoria katika nchi ya Tanzania. Kulikuwa na nguvu na mivutano ya

kitabaka Tanzania bara mara tu baada ya uhuru. Kushadidia hili, Khatib (1987:37) anasema ya kuwa walikuwepo wachache ambao waliitwa 'naizesheni' au 'wabenzi' dhidi ya kundi kubwa la 'akina kabwela'. Uhuru sasa ulikuwa unawafaidi wachache. Kwa sababu hii, mshairi ametunga mashairi kutoa wito wa ujenzi wa jamii mpya na kudhihirisha maana ya uhuru.

Lengo kuu la Azimio lilikuwa kujenga Tanzania mpya yenye haki, usawa na isiyo ya kitabaka. Hili ni shairi ambalo ni kielelezo bora cha jitihada za kutaka Watanzania kujenga ujamaa na kuufyeka mfumo wa kinyonyaji wa kibepari. Mtunzi amebainisha kwamba upo umuhimu wa kuzindua na kuwa macho ili kuleta mabadiliko yoyote.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni viongozi na wanasiasa ambao wanawakandamiza watu wanyonge bila kujali haki zao. Wao wanaangamiza hata kiini cha uhai. Hiki ni kinyume na matarajio ya wanyonge waliodhani kuwa Azimio la Arusha lingekuwa mwokozi wao na kidato cha kupandia ngazi maishani.

### 3.3 Shairi: 'Jibwa'

Anwani ya shairi hili inaashiria hali isiyo ya kawaida ya mhusika. Mtunzi ametumia lugha ya kukejeli kiongozi ambaye amelinganishwa na jibwa. Mtunzi ametumia dhihaka anapozungumzia mienendo ya viongozi.

Anasema:

> Jibwa likitoka jikoni
> Ulimi lajilamba
> Piga, limekuiba piga:

Jibwa likishika hatamu
Haliwezi kuacha utamu.

Jibwa litokapo jikoni likiwa lajilamba ulimi huwa limeiba. Hii inaashiria ya kwamba, mhusika anayezungumziwa atakuwa na alama za mabaki ya chakula alichoiba. Mtu kama huyu akipewa nafasi ya kuongoza, ataendeleza hali hiyo. Ni muhimu kutahadhari na kuhakikisha ya kwamba watu ambao ni mazao ya mfumo wa kibepari hawafai kamwe kupewa hatamu za uongozi, hasa baada ya Azimio la Arusha ili kuwepo na mabadiliko yaliyodhamiriwa.

Wito wa mtunzi ni kwamba, ni muhimu kupambana na viongozi wanaoendeleza hulka za kikoloni ili kuwaangamiza kabisa! Hii ndiyo sababu mtunzi anasisitiza wito wa 'Kupiga kichwa, kulimwagia petroli, kulifunga kamba shingoni na kuliburuzwa hadi jalalani'. Haya ni mapambano yanayohusu mabadiliko ya mfumo wa maisha ya jamii ambayo kwayo kwa kipindi hicho yalitakiwa jamii yenye kumiliki njia kuu za uchumi, jamii yenye haki sawa na jamii isiyonyonywa wala kunyonya. Kufanikisha yote hayo kulihitaji mapambano ambayo hayakuwa yamefanikiwa mara tu baada ya uhuru na kabla ya Azimio la Arusha. Haya ni wazi Kezilahabi asemapo:

Dawa ya jibwa ni shoka.
Subiri litakapolala,
Na ndoto za kwiba likiota
Piga kichwa piga.
Life,
Life bila ukemi
Majirani wasichingulie.

Kisha Kamba shingoni funga
Haraka haraka liburuze
Jalalani…

Kwa kawaida, jikoni ni mahala pa lishe na shibe. Ni asili ya kufukuza njaa na kiu. Ni taathira ya maongozi ya kibepari yaliyotokana na mfumo wa kikoloni. Kwa hivyo, yanatamanisha kwa wale walionufaika na ukoloni kwa sababu maongozi hayo ni ya ukiritimba, anasa na kujitakia makuu. Tamaa hii inatokana na ukuu na utamu wamamlaka. Anaeleza kuwa viongozi wenye tamaa wakiwa uongozini tamaa yao huongezeka na hawatosheki wala kujali utu na maslahi ya wengine.

Mtunzi anaendelea kusisitiza kuwa, viongozi ni wezi. Anaeleza ya kwamba, jibwa likianza kuiba huwa na mazoea ya kuendelea kuiba na huanza na mayai(vitu vidogovidogo). Kezilahabi anaendelea kusema kuwa:

Kesho litakula kitovu
Cha mtoto wako pekee
Jibwa jizi fisi.

Kula kitovu cha mtoto ni sawa na kula kiini cha maisha yake. Hii ina maana ya kwamba viongozi kama hawa wanaweza kuangamiza chemchemi za maisha ya walio wengi. Kinachobainishwa hapa ni ubinafsi. Pia, wanaongozwa na ulafi. Kwa hivyo, ni walafi, hawatosheki na wanaangamiza hata kiini cha maisha ya mtu. Kwa kuwa, wao ni katili.

Mshairi anaendelea kusema kuwa viongozi wetu hawana adabu kwa sababu ya kulewa mamlaka na wana kiburi. Viongozi wana cheche za matusi na maneno mengi yasiyo na

msingi. Wanapenda starehe, anasa na kulala kivulini lakini mtu wa kawaida anayeumia hubebeshwa mizigo ya kila aina. Kezilahabi anadhihirisha hili anaposema, 'Litalala kivulini wewe ukichumia juani'.

Mshairi anasema kuwa:

> Jibwa liloshika hatamu
>
> Litatumia kila hila
>
> Kila vitisho na unyama
>
> Litakacho likipate
>
> Na meno nje litatoa
>
> Kwa kivuli kipitacho.

Katika ubeti huu, mtunzi anaonyesha kuwa viongozi na wanasiasa hutumia kila hila, unafiki na ujanja. Maongozi yao ni ya vitisho na dhuluma. Wao hutumia kila mbinu ili wapate kile wanachokitaka. Kwa kusema kuwa 'Meno litatoa nje.' Mshairi anamaanisha kuwa wanatumia maongozi ya vitisho. Makosa ya wanasiasa huwafanya kila mara wakififikiria ya kwamba wameonekana kwa sababu hii, wanapigana tu na vivuli bali ni si watu halisi kwani wanatumia visingizio.

Mtunzi anaendelea kusema kuwa dawa yao ni shoka. Hapa, shoka inaashiria kuangamizwa kabisa! Kwa hivyo, anatoa wito ya kwamba huwezi kupigana nao ana kwa ana. Ni muhimu kuwapangia mikakati ya kuwaangamiza kisiasa. Anasema kuwa mikakati mwafaka ni 'kusubiri linapolala.' Hapa anasema kuwa watu wabuni njia mwafaka na njia mojawapo ni upigaji mzuri wa kura. Vilevile, kugundua hila

wanazotumia na kukabiliana nazo kupitia njia za ukombozi. Lazima wajue kiini na kumaliza ugonjwa huo kabisa. Anakariri kwamba, 'life bila ukemi.'

Njia nyingine ya kumaliza uovu ni kukataa hongo na kupiga kura kwa njia iliyo wazi na yenye haki. Anapendekeza mikakati ya kuangamiza viongozi hawa. Mikakati hii ni pamoja na kunyongwa, kupigwa risasi, kumwagiwa petroli na kuchomwa. Hapa anashauri watu wawe jasiri na kukataa hila za viongozi na kutumia njia hizi kuwamaliza kabisa.

Katika ubeti wa mwisho, mtunzi anatoa changamoto ya kwamba viongozi wabaya wanaishi miongoni mwetu. Suluhu ni kukataa ukabila na kufanya haki kwa kujenga jamii mpya. Shairi hili liliibuliwa na mazingira ambayo viongozi wamejisahau na kuanza kuwaibia watawala badala ya kuwaletea maendeleo na usawa katika jamii.

**3.4 Shairi: 'Cha Watu'**

Katika shairi hili, mshairi anazungumza kuhusu wale wazee ambao walipigania uhuru. Anawashtumu wazee hawa kwa kupoteza mwelekeo baada ya uhuru. Mtunzi anasema kwamba 'Wazee wa uhuru wamepoteza miwani.' Hawa wazee wamepoteza mwelekeo kwa kuwa na sera mbaya, maono sahili na itikadi mbovu. Wazee hawa hufikiria wao pekee ndio wanastahiki. Kulingana nao, hakuna mwingine anayefaa.

Huu mtazamo finyu wa kijamii ni kizuizi kikubwa kwa demokrasia katika mataifa huru ya Kiafrika. Huchangia kutengwa kwa baadhi ya watu katika maongozi ya nchi. Hivyo, ni njia mojawapo ya kuendeleza ukoloni mamboleo na mfumo wa kitabaka.

Miongoni mwa vikwazo vinavyotinga maendeleo ya Afrika ni ubarakala na ukaragosi wa kisiasa, kujitakia makuu na ufisadi. Kwa njia hii, mataifa ya Kiafrika ikiwemo Tanzania wakati wa uhuru yalirithi makosa ya kisera. Sera hizo ziliundwa kimakusudi kuwanufaisha viongozi kama hao kwa lengo la kunyonya na kujinufaisha wao wenyewe pamoja na walioshirikiana nao.

Kwa jinsi hiyo, taifa kama la Tanzania baada ya uhuru lilirithi mfumo ambao haukufaa mazingira ya Tanzania. Mifano ya viongozi waliotajwa hapo juu hawangetoa fursa kwa uongozi wenye uwazi, uajibikaji na kushirikisha wengine. Mifumo ya maongozi ya kiuchumi haingeruhusu wengine kufurahia matunda ya uhuru. Viongozi kama hao hawangeruhusu mabadiliko yoyote. Hiyyo, maongozi yao yalijaa michakato na harakati za kujiendeleza na kujilimbikizia mali.

'Wazee' ambao ni ishara ya viongozi waliopigania ukombozi wana kiburi na maringo na hawakubali kushauriwa wala kukosolewa. Walipigania uhuru, basi wanachukulia kuwa nchi ni yao. Kwa misingi hiyo, vijana huambiwa wao ni viongozi wa kesho. Wazee hawa ni wahifadhikiasi cha kutobadili maono, sera na mbinu zao za kuongoza. Lengo lao kuu ni kukimbilia makombo (mabaki) na nafasi zilizoachwa na wakoloni.

Mtunzi anasema kuwa 'Watoto wawasomea kinyumenyume.' Hapa, kulingana na viongozi hawa, yale maarifa ambayo vijana wamepata kupitia elimu yao ni kinyume na matarajio ya uhuru wa Afrika. Wazee hawa wanaona vijana hawana lolote la maana la kusema kuhusiana na dhamira za uhuru uliopiganiwa. Kwa njia hii, wazee wanajiona

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

wao ndio wenye nia nzuri kwa taifa na wenye mwelekeo unaofaa kulingana na malengo ya uhuru. Wao wanawaona vijana wana nia mbaya ya kuvuruga nchi.

Mshairi anaendelea kueleza kuwa katika kufanya hivi, hawa wazee wana tamaa ya mali. Mtunzi anasema kuwa 'Udenda wao umedondokea chakula.' Anamaanisha kuwa, kwa sababu ya tamaa yao ya kupita kiasiwao wamekula rasilmali yote ya taifa. Anasema kuwa wazee wamekula minofu yote kuashiria zile rasilmali za taifa.

Kwa ambavyo wamefilisi nchi, mtunzi anasema 'Sasa wajaribu hata mifupa', anaashiria kuwa wanang'ang'ania chochote kile wanachokiona. Ni muhimu watu waamke ili kuokoa jamii na taifa lao. Katika kuamka huku, mtunzi anataka vijana wachukue hatamu za uongozi leo, wasingoje kesho kwa sababu nguvu na maono wanazo.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni uhifadhi. Wazee au viongozi waliopigania uhuru hawataki kukosolewa, kupewa wosia wala kubadili maono yao kuhusu uongozi wa nchi. Wanawaona vijana kama watu wasio na malengo mazuri, hivyo hawafai kuongoza. Wazee hawa bado wanashikilia mawazo yao sahili na kuwanyima vijana nafasi za uongozi.

**3.5 Shairi: 'Bonde'**

Mtunzi anaongea kuhusu giza lililokuwepo hapo awali. Anasema kuwa 'Hapo zamani za kale palikuwa na giza.' Giza linaashiria maisha mabaya yasiyo na tumaini. Ni mfumo wa uongozi wa kidhalimu na mambo maovu yanayotakana na uongozi usiojali utu. Anaendelea kusema kuwa:

> Halafu kutoka mlima Kilimanjaro jua likachomoza.

Mazingira haya yapo karibu na mji wa Arusha na kuchomoza kwa jua kunaashiria matumaini ya watu wanchi ya Tanzania kulingana na tangazo la Azimio la Arusha na jua hilo likang'ara juu ya nchi kwa tabasamu. Kauli hii inamaanisha kwamba, Azimio la Arusha liliwapa Watanzania matumaini ya maisha bora. Lilinuiwa kujenga Tanzania huru yenye usawa, heshima na isiyo ya kitabaka.

Tabasamu hili linaashiria kule kukumbatia Azimio la Arusha. Mshairi anaendelea kusema kuwa 'Halafu kutoka mlimani maneno makubwa yalijiviringisha kwa nguvu za wazo'. Hapa mtunzi anamaanisha kule kutangazwa kwa Azimio la Arusha. Maneno haya yalidhamiria kuleta mapinduzi na wale ambao maslahi yao yalitishwa wakawa 'wamekimya' kwa kuwa walishtuliwa na mawazo ya kimapinduzi.

Hapa mtunzi anasema kuwa 'Wakatumbukia kwenye bonde la fikra.' Anamaanisha kuwa hawa ambao maslahi yao yalitishwa walianza kufikiri kwa kina wasijue nini cha kufanya. Huku wakiwa katika hali hiyo kukawa na 'Mwanga.' Mabepari walipokuwa katika hali ile ya 'kimya', wachochole wakawa na tumaini la kuona vidato vya kupandia ngazi kimaisha. Baada ya giza, hawa waliokimya walifikiria mbinu mpya za kujiendeleza. Katika hali hiyo, wenye matumaini waliendelea kusherehekea.

Wale walio na matumaini wakawa na fikra pevu ya kuziba mianya ya kuendeleza ubepari. Kezilahabi anaonyesha kuwa ili Azimio la Arusha liwe na maana, kuna umuhimu wa utekelezaji kutimizwa vilivyo. Kufaulu kwa Azimio pia kutatokana na kutathmini kwa nini kipindi mara tu baada ya uhuru na kabla ya Azimio hakikuleta

mabadiliko wala kufaulu kutimiza matarajio ya uhuru. Ilikuwa muhimu kuelewa hatua mwafaka za kuchukuliwa kuleta mabadiliko ya kweli ndipo malengo ya Azimio yatimie.

Katika ubeti wa mwisho mshairi anasema kuwa:

> Sasa twaimba nyimbo za matunda ya mwanga
> Na fikra pevu, tukifukia mashimo
> Yaliyoachwa nyuma

Watu wana matumaini ya kuwa Azimio lingefaulu. Hatua hii ilihitaji fikra pevu. Ni muhimu watu kutathmini ni nini kilifanya Azimio la Arusha kutofaulu ikizingatiwa kwamba diwani hii ilitungwa kutathmini iwapo malengo ya Azimio la Arusha yalitimia. Anaonyesha kuwa mashimo yanaashiria udhaifu ulioachwa wazi. Suluhisho litatokana na kuyaziba mashimo hayo ili waimbe wimbo wa matunda ya mwanga (ufanisi wa Azimio la Arusha). Ili matunda ya Azimio yapatikane na malengo kufaulu, ni lazima watu hawa wajitafiti na wajielewe ndipo watambue usawa na haki.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni uongozi wa nchi uliokuwa dhaifu na wa kutetereka. Kulikuwa na uzembe wa viongozi kutowajibika, utekelezaji mbaya wa malengo ya Azimio na hali ya utabaka na ubinafsi kuendelea kuwepo hata baada ya Azimio la Arusha.

### 3.6 Shairi: 'Ulingoni'

Kezilahabi anazungumza kuhusu mchezo uleule ambao wanasiasa wameuzoea. Wanawachezea wananchi watawaliwa. Anaonyesha kuwa wanasiasa hujifanya kujua kila

kitu. Katika kufanya hivi, wanawaudhi watawala ambao wanaelewa kile kinachofaa kufanywa.

Anasema kuwa:

Bila kubadilisha uwanja
Mwondoko ni uleule
Kilichobaki ni kuanzisha kiufundi
Mduara mpya mwenye mzingo mpana.....

Katika ubeti huu, anasema kuwa raia wamechoka na ule mkondo mmoja wa utawala. Mtunzi anazungumzia mbinu mpya za uongozi ambazo yafaa watawala wabuni. Wale wanaotumia mfumo mmoja wa utawala hawana chao sasa kwa sababu wananchi wamechoka na mkondo huu mmoja wa uongozi na polepole, wanauhama. Anawambia wanasiasa wabadili mbinu za uongozi kwa kubadili mkondo ili wananchi wasihame katika mfumo huo.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni mfumo wa uongozi ambao haukubadili hata baada ya uhuru. Licha ya miaka mingi ya uhuru hakuna chochote kipya ambacho kilionyesha matunda ya uhuru na Azimio la Arusha. Hivyo, mtunzi alikuwa akihakiki uongozi wanchi kwa kuzingatia malengo ya uhuru na Azimio la Arusha. Amebainisha ya kwamba hata baada ya miaka mingi ya uhuru, ukoloni mamboleo na ubepari ni vitu ambavyo vilihitaji kushughulikiwa kwa kutumia mbinu na mikakati mipya.

### 3.7 Shairi: 'Mafuriko'

Katika shairi hili, mtunzi anawahamasisha wananchi kotekote kuhusu uchaguzi bora wa viongozi. Anabainisha ya kwamba ni kutokana na uchaguzi bora tu ambapo viongozi wa

zamani wataweza kuondolewa mamlakani. Kwa jinsi hii, wananchi sasa watawachagua tu viongozi wenye maono. Huu utakuwa wakati wa mapinduzi. Mtunzi anasema:

> Ninaandika wimbo juu ya mbawa za nzi
> Utoe muziki zirukapo wausikie walio wengi
> Ushairi wa jalalani utaimbwa
> Juu ya vidonda vya wakulima
> Na usaha ulio jasho lao.

Kezilahabi anaonyesha kwamba atatumia mbinu ya ushairi kuwajuza na kuwahamasisha watu kuhusu wajibu wao katika kupigania ukombozi wa pili. Miongoni mwa vitu atakavyozingatia ni utetezi wa haki za wakulima na jasho lao.

Wanyonge katika jamii kama vile wakulima wananyonywa,wanaonewa, wanakandamizwa na wanadhulumiwa. Hawafurahii matunda ya jasho lao. Kilimo ndicho tegemeo na nguzo ya walio wengi katika jamii. Kutotendewa haki kuna maana ya kwamba walio wengi wanadhulumiwa na kunyanyaswa. Hali yao ni duni na wanadumu katika umaskini.

Anasema ya kwamba nguvu za mapinduzi zitavunjilia mbali maongozi ya zamani na kutakuwa na kishindo kikuu. Uongozi mbaya utang'olewa kutokea shinani na nyenzo zote zinazoendeleza mfumo wa zamani pia zitaangamizwa. Uongozi usiojali utu utazikwa katika kaburi la sahau na hautakuwa na nafasi tena. Mazingira yaliyoibua utunzi huu ni mwamko mpya Tanzania na dunia nzima. Kwa njia hii, mapokeo yote yakiwemo masuala ya uongozi, yatakataliwa na wananchi.

### 3.8 Muhtasari

Katika sura hii, utafiti ulishughulikia utathmini wa malengo ya kupigania uhuru na Azimio la Arusha. Umeonyesha kwamba malengo ya uhuru na Azimio la Arusha hayakutimizwa kwa sababu ya ubinafsi, uongozi mbaya na utekelezaji mbaya. Hivyo, ukoloni mamboleo unadhihirika miaka mingi baada ya uhuru. Suluhisho ni wananchikuhamasishwa ipasavyo na kuchukua hatua ifaayo ili kuleta mapinduzi ya maana. Jambo hili linahitaji mapambano. Sura inayofuata ilishughulikia maudhui ya kiuchumi.

# SURA YA NNE

## Maudhui ya Kiuchumi

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii, utafiti ulidhihirisha kwamba utunzi huakisi uyakinifu na uhalisia wa mazingira ya mtunzi kwa kuzingatia matukio ya kihistoria ya wakati wake. Sura hii pia, ilibainisha kwamba Kezilahabi, kama mtunzi anaielewa jamii yake barabara. Utunzi wake unaonyesha jinsi msimamo wake ulivyo kuhusu jamii. Anajitokeza kama mwanafalsafa anayezungumzia ujenzi wa jamii mpya hasa kiuchumi baada ya uhuru.

Mtunzi anaelekeza silaha zake dhidi ya mfumo wa kibepari ambao ndio adui wa mataifa changa ya Kiafrika. Anachambua hali halisi ya Tanzania baada ya kutangazwa kwa Azimo la Arusha la mwaka 1967. Uhakiki ulizingatia malengo ya Azimio kama mhimili wa kuielekeza jamii ya Tanzania kuelekea maisha bora ya ufanisi na maendeleo.

Mihimili ya nadharia ambayo ilioongoza utafiti katika sura hii ni ile inayoangalia miktadha ya utunzi, urejeleaji wa matukio ya kihistoria pamoja na uelewa wa mazingira na maisha ya mtunzi kwa ujumla.

### 4.1 Shairi: 'Maendeleo si Ndwele'

Katika shairi hili, mtunzi ametumia jazanda ya 'Panya' kuonyesha namna mataifa machanga ya Kiafrika yanavyonyonywa. Anatumia neno 'Jiko benki' kuonyesha jinsi rasilmali za nchi zinavyotumika vibaya. Hii ndiyo maana anasemakuwa chakula hakipikiki kikaiva. Anaashiria sera na malengo ya Azimio la Arusha. Kutopikika

kunaashiria kutotimizwa kwa malengo ya Azimio na kuwa kuna vikwazo vilivyotinga utekelezaji wa Azimio.

Kiuchumi Azimio lililenga kuleta usawa wa kiuchumi, kuondoa utabaka, unyonyaji, ubinafsi, ukupe na ukiritimba. Hata baada ya kutangazwa kwa Azimio, kulikuwa na pingamizi kutoka kwa wale walioendeleza mfumo wa kibepari. Hali hii katika jamii ya Tanzania ilitinga kufaulu kwa Azimio la Arusha na malengo ya kupigania uhuru.

Mshairi anasema 'Watoto wagongana wao kwa wao.' Hapa, anamaanisha kuwa hata wale waliokuwa na mawazo mazuribaada ya uhuru na Azimio badala ya kuyaendeleza, wao pia wameathiriwa na mfumo wa kikoloni wa kupigania kipato. Hii ndiyo maana anasema 'Wanatoana meno'. Hii inaashiria kuwa watu wanapigana katika hali ya kujilimbikizia mali.

Mtunzi anasema kuwa 'Baba atoka chumbani na bunduki akiyumba'. Hili linaashiria kwa kukosa mwelekeo, kiongozi wa taifa anatoka na kauli kali ya kuangamiza maovu, lakini pia anayumbayumba kwa kukosa msimamo thabiti. Inamaanisha kuwa yeyepia ameathirika. Bunduki hutumika kuangamiza watu. Kezilahabi anasema, 'Akiimba wimbo wa taifa wa Afrika.' Anaashirira kuwa wao ni wamoja kama taifa moja la Afrika. Kinaya ni kwamba hawamaanishi wanayosema. Wimbo huu ni ishara ya unafiki ilhali wanadanganya watawaliwa kuwa wako pamoja. Ukweli ni kwamba wao wanaendeleza maslahi ya kibinafsi.

Mshairi anaposema 'Alioutunga ndotoni.' Ni ishara ya mambo mazuri anayowaza tu lakini hatendi. Hii ndio maana anasema 'Panya anapita dirisha lilowazi nje' kwa maana

ya kuwa wanyonyaji hawanaswi kwa kuwa hakuna mikakati mahsusi ya utekelezaji wa maazimio yanayotarajiwa kuleta usawa.

Kezilahabi anasema 'Mtoto bubu anawatazama akicheka.' Hii ni kuashiria wale ambao walikuwa na nia ya kutekeleza malengo ya Azimio hawana sauti na uwezo kwa kuwa mfumo wa kibepari hauwapi fursa ya kuteleza wanacheka tu bila kuelewa cha kufanya. Anasema 'Kitoto kichanga kinalia.' Katika muktadha huu, ni kuwa wale wanaoelewa kile kinachofaa kufanywa wanaumizwa na mfumo dhalilishi na kandamizi.

'Bundi anamshika panya gizani.' Hii inaashiria kuwa, shughuli za kuipora nchi na rasilmali yake huendeshwa chini kwa chini ndio maana ametumia shughuli za gizani. Katika kufanya hivyo ndiyo mataifa ya Afrika yameangamia kiuchumi kutokana na hila na ulaghai unaofanywa na viongozi. Hii ndio maana ya maendeleo yamepiga chenga Afrika. Mifumo kandamizi imefanya rasilmali zote kuporwa.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni mfumo wa kibepari ulioendelea hata baada ya Azimio na uliendelea kuwakandamiza wanyonge katika jamii. Tabaka tawala lilitumia mbinu na hila mbalimbali kulinda na kudumisha maslahi yao. Hali hii imebainika miaka kadhaa hata baada ya Azimio la Arusha.

**4.2 Shairi: 'Njia Tulopitishwa'**

Katika shairi hili, mtunzi anaashiria athari za mfumo wa kikoloni wa ubepari. Anaeleza kwamba, ile njia au mfumo wa kibepari imekita mizizi hata katika jamii ya sasa. Kwa sababu ya ile njia ya kikoloni, si rahisi kuondoa athari za ukoloni. Hii ndiyo sababu mtunzi anasema:

Sasa wakokota tongotongo nzito machoni kwa mswaki kuukuu.

Mswaki kuukuu ni ishara ya mbinu ambazo zinatumika kuondoa athari za mfumo wa kikoloni na ambazo hazina nguvu tena ya kukabiliana na uozo ambao upo katika jamii. Hata wale tunaotegemea kuleta mabadiliko ni mazao ya mfumo ule. Anasema 'Aa kusafisha meno ya njano.' Kuashiria athari ya ukoloni imekita mizizi zaidi na kwa sababu hiyo, tunaona kwamba wahusika wanafanya mambo yao kisiri ndio mtunzi anasema 'Kisha wanacheka gizani kwa mawi yatokeayo' kwa maana ya kwamba wanaendesha mambo yao gizani kama vile ulaghai na wanafurahia tendo hilo.

Tunaona ya kwamba, katika kufanya mambo haya wanaishia kuvutana kwa sababu ya rasilmali. Katika huku kung'ang'ania kipato wanatenga wale wanaozalisha mali. Anasema 'Walijigonga kwenye kichuguu walichokiumba na kuukimbia mchwa.'

Uongozi wa nchi unatoa mwongozo usiotegemewa na haufai. Hii ndiyo maana anasema 'Mlima unatoa cheche hafifu kileleni, zisotosha kuonyesha njia'. Haya ni maongozi yasiyofaa kukabiliana na maovu yanayokumba umma. Anaendelea kusema kuwa 'Nzige waloanguliwa jangwani'. Hii ni jazanda kwa kuwa nzige yaweza kumaanisha waporaji. Wanachukuwa chochote watakachopata katika nchi isiyo yao. Jangwa ni taashira ya hali ngumu ya maisha na umaskini. Hawa ni walaji ambao asili yao ni ya ulitima. 'Sasa walala juu ya majani'. Hii inaashiria kuwa hao maskini sasa wanalalia vinono, wao wamelalia hizo nafasi. Watu hao wanashikilia hatamu za uongozi na sasa nchi haina rasilmali kutokana nao. Anasema kuwa 'Yadaiwa mito na visiwa vimekauka.'

Mtunzi anasema kuwa 'Watetezi wapiga madebe shinda'. Kumaanisha wale wanaotetea haki sasa maneno yao hayana athari. Ni 'Ndege waoga tu washtukaao'. Hii inaashiria wale wanaonufaika na ule mfumo wa unyonyaji ndio wanashtuka lakini vigogo wenyewe hawashtuki.

Mtunzi anaonyesha kuzorota kwa uchumi ndiyo anatumia maswali ya balagha kuwa wananchi wanajiuliza, 'Kesho tutakula nini, swali la kitoto'na wale walokomaa ni wazee. 'Sasa tufe hivihivi, swali la watu wazima.' Mtunzi anawazindua watu wachukue nafasi zao katika kupigania haki.

Anaendelea kuonyesha hali ya kiuchumi ambayo ni ya kusikitisha na ndiposa analilia mizizi ya kikoloni iliyokita na kuiharibu jamii yake. Anasema kuwa 'Twasubiri mvua ya haki.' Hii ni kumaanisha kuwa tumaini lililoko ni haki kutendwa. Mtunzi anasema kuwa 'Tukisawazishe na kwa majembe makali'. Anaashiria juhudi mahsusi za kujenga mikakati ya kuleta usawa na haki.

Kezilahabi anasema kuwa 'Na kukandika nyumba mpya.' Anamaanisha kuna umuhimu wa harakati za kujenga jamii mpya ili kuondoa mfumo wa awali. Anasema kuwa 'Na kuchomamoto malkia wa askari.' Askari anaashiria dhuluma katika jamii za Kiafrika. Sasa kwa kuchoma moto anamaanisha kwamba kuna haja ya kuangamiza kiini cha dhuluma katika jamii kwa hivyo, ndio haki itapatikana katika rasilmali kwa kusema kuwa 'Penye haki vichuguu na milima hulala'.

Katika ubeti wa nne, mtunzi anaashiria kuwa ufisadi uliopo ni rasmi na kwa hivyo kutokana na hili, taifa limepata aibu. Hata hivyo, umoja wa wale wenye haki utapepea

daima na daima hawa watu watakuwa na wapo. Haya yatatimizwa ikiwa wenye haki watakuwa na umoja thabiti na nguvu sawa. Machozi ya moto inaashiria nguvu, katika kule kulilia pamoja, washikane na wawe imara watashinda katika umoja huo. Rasilmali ambazo zimeibwa zitarejeshwa na mapinduzi yatapatikana tu kukiwa na umoja.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni utabaka. Kwamba, licha ya kuwepo kwa malengo mazuri ya Azimio la Arusha, utekelezaji wake ulikuwa na matatizo. Utabaka uliendelea, unyonyaji ukadumishwa na walio wengi kukosa kufurahia matunda ya uhuru. Waliokuwa na maono mazuri hawakuweza kuyaafikia kwa sababu ya vikwazo vya mfumo wa uongozi. Hivyo, mfumo wa kibepari ukaendelea. Athari za mfumo huu zimekita mizizi na watawaliwa wanaumia sana. Hawana zana za kupigania haki zao kulingana na Azimio la Arusha na bado wananchi wanateseka kutokana na mfumo mbaya wa uongozi.

### 4.3 Shairi: 'Ukweli Koko'

Mshairi anaanza kwa kusema kuwa amekuja kusema uwongo. Katika maongozi ya Kiafrika, kuna wingi wa unafiki na ulaghai miongoni mwa viongozi wetu. Katika shairi hili, mtunzi anasema kuwa 'Watawala wanapenda demokrasia'. Hapa anadhihaki kauli au matamshi ya viongozi wetu kuwa wanapenda demokrasia na huku hawatekelezi wajibu wao na kusema kuwa 'Umaskini ni kujitakia'. Hapa si ukweli, mfumo uliopo wa kitabaka wa kibepari umejaa unyonyaji na ukandamizaji kuwa umaskini si wa kujitakia na kuwa wafanyi kazi si wavivu bali ni ule mfumo dhalilishi ndio unawaumiza na kuwafanya walimao wasivune mazao ya jasho lao.

Jasho la wakulima linaamwa na wengine. Wakulima wana mateso mengi kwa sababu ya kunyanyaswa na mfumo uliopo. Mawazo ya kidemokrasia ni matamshi tu bali si vitendo. Mfumo wa kibepari wenye ukiritimba unawanyonya wafanyakazi na kuwasingizia kuwa wavivu. Kwa kusema kuwa ardhi, madini na nafaka ni mali ya umma si ukweli kwa sababu ni mali ya walio wachache au mali ya umma lakini kwa manufaa ya walio wachache.

Mtunzi anaonyesha ya kwamba Kiingereza na Kifaranza ni funguo za maisha. Hali hii inatokana na sababu kwamba katika jamii husika kuna kutukuza lugha za kigeni. Hii ni ishara kwamba wahusika wamekengeuka na wanaamini kwamba lugha na tamaduni za kigeni ndizo ustaarabu. Kuhusiana na hili, Ngugi wa Thiongo (1977:14) anasema:

> Mfumo wa kikoloni ulizaa aina ya elimu ambayo
> ilikuza utii, kujichukia na kutojiamini
> uliwazaa watu ambao walong'olewa kutokana na
> asili zao, na ndiyo mwanzo wa uozo wa
> wasomi waliojitenga na jamii zao.

Utunzi wa Kezilahabi unabainisha ya kwamba mazingira ya kijamii ndiyo yanayoiunda hulka na shaksia ya mtu. Pia, anabainisha athari zilizoletwa na elimu ya kikoloni kuwa zenye kutumikia uchumi wa kibepari, kujisahau, kujidharau, kutojiamini, kuthamini na kutamani Uzungu, kujichukia na vilevile kuchukia chochote cha Kiafrika na kumfanya Mwafrika mtumwa katika mazingira yake. Katika mfumo wa kisasa kuna kuabudu vitu vya kigeni kama vile lugha hizi na tamaduni zake. Kwa misingi hii, anaonyesha kuna

utumwa wa kuabudu mambo ya kigeni tukipuuza ya kiasili. Kuwa lugha za Kiafrika ni lugha za mitaani ni kuonyesha jinsi tumezidharau lugha zetu asili za Kiafrika na tumekuwa watumwa wa uchumi wa kigeni na kupuuza wetu. Watu hawana uhalisi maishani mwao.

Imani ya Waafrika kama inavyodhihirika katika shairi hili ni njia moja ya kuwa watumwa wa utamaduni wa kigeni. Ni njia ya kuendeleza ukoloni mamboleo. Uchumi wa kikoloni uliwaathiri Waafrika kwa njia mbalimbali. Kama shairi linavyoonyesha, uchumi huu ulihimiza ubinafsi ambao uliambatana na unyonyaji usiojali utu. Kulikuwa na ubepari ambao uliambatanishwa na ulimbikizi wa mali. Hali hii pia iliathiri mfumo wa Kiafrika ambapo utamaduni wa Kiafrika ulipuuzwa na kudunishwa. Elimu ya kienyeji ilipuuzwa kwa manufaa ya utamaduni wa Kizungu. Maoni haya yameshadidiwa na Wanjala (1980:15) anaposema kuwa:

> Mwafrika aliyesoma aliona vigumu kuhifadhi
> miiko na ibada zilizowaunganisha watu wake pamoja...
> alitenganishwa na sherehe za kuimba, kupiga ngoma.....

Ni katika misingi hii ambapo Kezilahabi ametunga shairi hili kufokea ukoloni mamboleo na kudhihirisha madhara yatokanayo na kuabudu utamaduni wa kigeni. Ni kupitia imani potofu kama hizo ambapo imekuwa vigumu kutekeleza malengo ya kupigania uhuru na Azimio la Arusha.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni uongozi mbaya. Viongozi sasa ni mazao ya mfumo wa kibepari kupitia aina ya elimu waliyopata. Hivyo, inakuwa vigumu kuleta mabadiliko

kisera kuwiana na mahitaji ya uhalisia wa mazingira ya Kiafrika. Wamekengeuka na hawana heshima na chochote cha Kiafrika. Viongozi hawa wanakuwa kikwazo katika kuleta mapinduzi na maongozi mapya.

**4.4 Shairi: 'Alalaye'**

Shairi hili ni mfano wa dhiki zinazowakumba wakulima na wavuvi. Kama tulivyotaja, mtunzi alizaliwa katika mazingira ya ukulima na uvuvi. Anasema, huku wakulima na wavuvi wakiendelea kuumia, wale wanaofaa kuwaokoa hawajali. Mtunzi anasema 'Mafuriko yaliyotokea.' Kinachoashiriwa na mafuriko ni kile kitu ambacho kimeharibu masoko ya ulimwengu. Bei zilizotangazwa zimeathiri wakulima na wavuvi.

Masoko ya ulimwengu yaliwanyanyasa Waafrika kutokana na bei duni kwa mazao yao. Bei iliamuliwa ng'ambo. Aidha, Waafrika hawakuwa na sauti ikawa kwamba mazao yao yananunuliwa kwa bei rahisi lakini waliyazalisha kwa gharama ya juu na kazi ngumu. Mfumo wa kibepari unatumiwa kunyanyasa wakulima. Hii ndio maana ya kusota kimya na kuimba kimoyomoyo. Wanaumia katika umaskini wao bila usemi wowote.

Mtunzi anaendelea kusema kwamba:

> Tumeona mifupa ya kuku jalalani.

Kauli hii inaashiria kwamba wakulima na wafugaji wameshuhudia ishara kwamba kumekuwepo na manufaa yanayotokana na jasho lao lakini hawakushirikishwa katika uhondo huo. Hii ina maana ya kwamba jasho lao linawafaidi wengine. Mabaki ya mifupa huwepo baada ya kusherehekea na mifupa hutupwa kwenye jaa la taka. Hivyo, wakulima na wafugaji hupata tu masalio au masaso ya kile ambacho kimewafaa viongozi.

Wakulima na wafugaji wameona mabaki ya nguvu zao japo waliumia kuzalisha mali, hawajapata lolote ila wanaonufaika ni wengine.

Kauli hii imeendelezwa na Kezilahabi anaposema kwamba 'Tumeona vyombo vikisafishwa jikoni'. Kwa mtunzi kusema kuwa 'Alalaye simwamshe.' Anamaanisha kila mtu ana haki ya kufurahia matunda ya jasho lake na baadaye hata mjinga pia huerevuka kuonyesha kuwa kuna mabadiliko na wale waliodhulumiwa walizinduka na sasa wanajua haki zao na wanazitetea.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni mfumo wa uongozi ambao unawakandamiza wananchi kwa kuwasingizia kuwa wao ni wavivu na ndio maana hawana maendeleo. Pia, viongozi wanawahadaa watawaliwa kuwa wanapenda demokrasia. Haya ni maneno matupu, vitendo vyao havionyeshi kuwa wana nia njema kwa wale wanaowatawala.

**4.5 Shairi: 'Maskini 2'**

Katika shairi hili, mtunzi anatuchorea hali duni ya maskini katika mfumo wa kitabaka. Mhusika ambaye ni maskini anasema hafurahii maisha yake kutokana na mfumo dhalimu. Katika hali yake ya kusononeka, anaangukia chochote kinachoweza kumuauni. Mtunzi anasema:

> Maskini amechinja maelfu ya sisimizi
> Chajio cha mwisho.

'Sisimizi' ni wadudu wadogo sana na hawafai hata kuwa chakula cha binadamu. Lakini kwa sababu ya ulitima, basi mhusika anachinja kiasi kingi cha sisimizi ili ale kama

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

chajio. Na kwa sababu ya mahangaiko na mateso anayoyapata katika hali yake ya umaskini analazimishwa kuwameza wazima bila kutafuna.

Vilevile, mtunzi anaashiria hali ya mhusika ambayo imedhoofika na kuwa mhusika hajiwezi kabisa. Hali hii inaelekea kumletea kifo kwa sababu ya kukosa lishe. Hili linadhihirika pale ambapo mtunzi anasema kuwa 'Mdomowe ukiwa wazi.' Istoshe, kwa sababu ya umaskini wake, amepuuzwa na wanajamii wengine. Hapati msaada kwa sababu ya hali yake duni.

Mtunzi anasema:

> Alikufa juzi kwa njaa
> Kila mpita njia atupia jani bichi
> Kuepuka laana.

Mtunzi ametumia kinaya kwamba, mhusika alipokufa juzi kutokana na njaa, kila mpita njia alimtupia majani kama desturi ya jamii yake ili wasipate laana. Hawa waliotupa majani wasipate laana walikuwa katika nafasi ya kumwokoa mhusika asife kutokana na njaa. Pia, maskini huyo ameachwa palepale badala ya kupewa mazishi na la kusikitisha ni kwamba, 'Atazikwa na halmashauri ya jiji bila jina.' Hii inaonyesha kuwa, mhusika atakokotwa na kuzikwa bila heshima yoyote kwa kuwa yeye ni maskini.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni mfumo dhalimu wa kitabaka ambapo tabaka la juu linadhulumu tabaka la chini bila kujali lolote. Maskini wanaendelea kukandamizwa hadi kufa kutokana na mfumo dhalimu usiojali watu wanaoishi katika ulitima.

**4.6 Shairi: 'Maskini 3'**

Katika shairi hili, mhusika ni maskini. Si kwamba alitaka kuwa katika hali hiyo bali alilazimishwa na wale walio tajiri. Kulingana na mtunzi, mhusika huyu ni mkulima au mfugaji. Anaongea kuhusu unyonge wao ambao mfumo wa uongozi unawanyanyasa kwa kuwa yeye na wengine walio katika tabaka kama lake wananyonywa.

Kwa upande mmoja, mhusika huyu ananyonywa na tabaka na kwa upande wa pili, hali hii ya umaskini imemsababishia njaa. Kwa jinsi hii, anaona kwamba pale ambapo atasukumwa kufikia mwisho na akonde kama siafu atachukua hatua. Mtunzi anasema:

> Wakati nimekondeana kama siafu
> Nitaingia ndani ya sikio la tajiri
> Ukali mumumo nitang'ata
> Sikio lilokataa kusikia kilio changu
> ….hadi karne kama ndege.

Siafu ni mdudu aumae kwa uchungu. Mtunzi anaashiria kuwa, watu wa tabaka kama la mhusika watachukua hatua ya kupigania haki yao. Hatua hiyo itamzindua tajiri. Anaposema kuwa 'Kwa ukali atang'ata' ina maana kuwa mapambano kati yao na tajiri yatakuwa makali hadi yule tajiri (dhalimu) asikie, akome ukandamizaji wa wakulima na wafugaji. Wale wanaopuuza malalamishi ya wanyonge watakiona. Mhusika analalamika kuwa hali kama hii ni ya zamani wakati wa ukoloni na hata baada ya uhuru hali hiyo bado ingalipo.

Mtunzi anaendelea kusema kwamba, kwa sababu ya dhuluma zilizoko, watu kama hawa wamekuwa kama viziwi. Kuashiria kuwa wamenyamazishwa na hawajapewa nafasi ya kupigania haki zao kwa muda mrefu. Na kwa sababu ya kukosa sauti, 'Wanakunywa maji ya mvua yalobaki juu ya jani la mti.' Hii ina maana kwamba, baada ya watu hawa kufanya kazi yao kwa bidii, wao hupata tu masalio.

Wanategea masalio, watu wa tabaka la juu nao wanaogelea katika utajiri unaotiririka kama mto. Vilevile, anasisitiza kuhusu hali ya 'Utajiri unaoyoyoma maziwani na baharini.' Huu utajiri mkubwa unawaendea watu ambao wamestarehe kwa jasho la wanyonge na wanyonge nao wamebakia kutegea masalio tu. Wakulima ndio wapo kwenye ulitima hata baada ya kuzalisha mazao. Wanapotetea haki zao, wanaambiwa hawaeleweki. Kilio cha wanyonge kinachukuliwa kama kelele. Wanapojitetea tabaka dhalimu linadhani hawajui wanachosema kwa sababu tajiri haoni kwa nini maskini alalamike.

Mazingira yaliyoibua utunzi huu ni utabaka na udhalimu. Wale wanaozalisha mali wanaishia kuumia na mali yao kunufaisha watu wa tabaka la juu ambao wanawakandamiza. Pindi wanapojaribu kulalamika, hakuna anayewasikia. Malalamiko yao yanaoneka na kuchukuliwa tu kama kelele.

### 4.7 Shairi: 'Zimwi'

Katika shairi hili, mtunzi anaonyesha hali geni au usasa ambao umeathiri jamii. Sera hii ya kigeni imeelezwa kwa kutumia sitiari ya 'Zimwi linaloweza kuwaangamiza'. Ugeni huu umewaathiri na kuwameza wanakijiji. Zimwi hili ni ishara ya utamaduni wa kigeni,

sera au elimu geni. Sera hii imekengeusha vijana na athari yake imesambaa. Wanakijiji wanajaribu kuambaa athari hizo na kukadiria kama kuna njia ya kuwaokoa vijana.

Wazazi wanalia katika kule kukengeuka hasa wanapokumbuka uchungu waliopitia kuwalea vijana. Mtunzi anaeleza masikitiko ya wazazi kuhusu hali ya sasa ya maisha ambapo vijana wamemezwa na ubinafsi na kuwasahau wazazi wao hasa kiuchumi.

Kwa sababu ya kuelewa misingi ya jamii, hali ya usasa inaangamiza zaidi vijana wanapojitenga na kusahau jamii zao kabisa. Katika hali ya sasa watu wamejitenga na wanajishughulisha tu na masuala ya kibinafsi bali hawasaidii na kuendeleza uchumi kwa pamoja. Kwa sababu ya kupuuza wazazi na wanajamii, utabaka umezuka. Kuna watu wenye uwezo wa kiuchumi na wale wasio nao. 'Udende nzi wakitambalia.' Hili linamaanisha kuwa matajiri wamedorora katika hali ya anasa ambayo imewafanya washinde wakihesabu mali na kufikiria pale pa 'Kutoboa'. Hii inaashiria kuwa, kutokana na mfumo wa sasa wa kiuchumi, kizazi kipya kilichozaliwa katika mfumo huu hakijali tena jamii yao bali wao hujilimbikizia tu mali.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni ubinafsi na utabaka ambapo jamii inajitenga kwa misingi ya uzalishaji mali. Hata vijana ambao uchumi wa kesho unawategemea sasa wamekuwa na ubinafsi na hawajali maslahi ya wengine. Kila mmoja hufikiriajinsi atajiendeleza kiuchumi bila kujali mwenziwe au hata jamaa yake.

### 4.8 Muhtasari

Katika sura hii, Kezilahabi anadhihirisha ya kwamba utunzi huakisi uyakinifu na uhalisia wa mazingira ya mtunzi kwa kuzingatia mazingira ya kihistoria. Anaelekeza silaha zake dhidi ya mfumo wa kibepari ambao ni adui wa mataifa changa ya Kiafrika. Anamulika hali halisi ya Tanzania baada ya kutangazwa kwa Azimio na kuonyesha athari za mfumo wa kikoloni ambao umekita mizizi kwa jamii ya sasa na kuathiri uchumi wa nchi ambao umezorota kutokana na uongozi usiotegemewa.

# SURA YA TANO

## Maudhui ya Kijamii

### 5.0 Utangulizi

Sura hii iliangazia masuala yanayoikumba jamii ya sasa.Ilimulika maudhui yanayohusiana na hali za watu zinazoashiria mabadiliko ya wanajamii hasa wanapofanikiwa na kutoka katika hali duni. Unyanyasaji wa wanyonge, kama vile yatima na maskini unadhihirika. Zaidi sana ujenzi wa jamii yenye uadilifu na utu kutokana na kuomba msamaha.

### 5.1 Shairi: 'Mke wa Waziri'

Katika shairi hili, mtunzi anaanza kwa kuonyesha picha ya mhusika Monika aliyekuwa mke wa Waziri. Amesawiriwa kama kielelezo cha watu wanaobainisha wimbo wa maisha unaohusisha mabadiliko hasa mtu anapotoka katika tabaka duni na kufanikiwa. Pia, kukiona kinyume na kinaya kinachotawala katika maisha.

Kinaya kinachozungumziwa kinatokana na watu ambao wanabadilika na kujitenga na wenzao baada ya hali zao kubadilika kutoka uduni hadi ufanisi. Haya ni mabadiliko ambayo yanawafanya baadhi ya watu kuikana jana yaona kujisahau haraka kama anavyofanya Monika katika shairi hili. Kwa njia hiyo, jana inayodhihirishwa katika shairi hili inaashiria maisha ya unyonge au uduni.

Katika hali yake ya awali, mtunzi ameonyesha kwamba Monika alitoka kwao bila ushanga kiunoni na kamakumbikumbi asiye na mbawa. Taswira hii inasaidia kuelewa hali ya unyonge na umaskini aliokuwemo Monika. Kukosa ushanga kiunoni kunaashiria

hali ya juu ya umaskini. Tashbihi ya kumbikumbi asiye na mbawa inaashiria kukosa uwezo wa kuruka. Hali hii inasaidia kuelewa hali yake duni kimaisha. Monika alibadilika alipofika mjini na kuolewa na waziri. Tukio hilo lilimwathiri Monika kitabia, kimtazamo na kimwenendo. Ni mwepesi wa kusahau alikotoka. Ni kinaya kwamba sasa anataka watu aliokuwa akishiriki nao awali wasimame barabarani kumshangilia apitapo. Mtunzi anasema kuwa:

> …upitapo wainua kipua juu
> Chogo limechongeka kama senene
> Na kutusanifu kwa mawani meusi
> Kama nyani achezaye sarakasi

Hii ni ishara ya maringo, kiburi, na dharau baada ya hali ya Monika kubadilika kuwa nzuri. 'Kuinua kipua juu' ni kejeli ambayo mtunzi anatumia kuwazindua watu wanaobadili mienendo yao wanapofanikiwa. Anaendelea kudhihaki mienendo ya watu kwa kusema kuwa wanakaa kamab 'Nyani achezaye sarakasi'. Maelezo haya yanayoonyesha uigizaji wa mienendo isiyo halisi, kwamba kule kuwa bibi wa waziri kumemvimbisha kichwa na amaenza hulka isiyo halisi. Kwa kejeli, mtunzi anamshutumu Monika kwa vituko na mienendo iliyobadilika. Mtunzi alikuwa na ufahamu wa kina kuhusu maisha ya Waziri. Anasema:

> Yule mumeo anatoka kijiji jirani
> Tulimwona akilambwa na mbwa
> Alipomaliza kujisaidia.

Kezilahabi anamaanisha kuwa anamtambua mumewe Monika ndani nanje. Walitoka vijiji jirani na mtunzi alimwona nyakati zile mumewe Monika akiwa katika hali duni. Hii ni

taswira inayoonyesha ya kwamba hata mume wa Monika alitoka katika familia maskini na hali yake ya mwanzoni ilikuwa duni.

Kufahamikiana kwa mtunzi na mumewe Monika kunaendelea kwa kauli hii. 'Na alikimbia siku ya tohara'. Hili lina maana kuwa mumewe Monika alikuwa mwoga. Mtunzi anaendelea kumshutumu mumewe Monika kwa kiburi chake. Anatumia tashbihi kuonyesha mienendo yao ilivyo ya ujeuri, maringo na kujiamini kama beberu, tayari kupigana. Anampa changamoto aweze kuzingatia ukweli wa mambo na kukumbatia uhalisia wa maisha bila kusahau alikotoka.

Kulingana na mtunzi, mienendo ya watu kama Monika ni bandia. Anamshauri Monika kusikiliza ushauri wa nasaha kuhusu uhalisia wa maisha ya wanawake wa mashambani. Anatumia maswali balagha kumzindua Monika aone na kukumbatia ukweli wa mambo. Kuwa mambo ya ukuu ni ya muda tu na yakiisha, mtu hurudi pale alipokuwa.

Funzo ni kwamba kiburi cha madaraka huzaa ubeberu. Maisha yetu ni safari ndefu na binadamu awapo kwenye safari ya maisha yake ulimwenguni, anapaswa kuichunguza maisha yake kwa jicho la upembuzi kama mtembeaji mzuri anayeifahamu njia anayoitumia. Uchunguzi huo unamdhihirishia hali iliyomo ulimwenguni. Kinaya ni kwamba watu wengi baada ya kunyookewa na maisha huwa wepesi wa kujisahau na pia kusahau walikotoka.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni hali ya binadamu kujisahau hasa wanapotoka katika tabaka la chini na kuanza kuwaona walioshiriki nao kama watu duni. Hali ya ukengeushi na kusahau kwa haraka inadhihirika wazi.

## 5.2 Shairi: 'Marahaba'

Katika shairi hili, falsafa ya mtunzi ni kuhusu maana hasa ya maisha. Jambo kuu ni umuhimu wa kujiandaa ili kuyakabili maisha vilivyo. Wito hapa ni kwa binadamu kujichunguza na kujielewa ili kujijua, kujitambua na kujirekebisha vilivyo. Kezilahabi anaeleza kuwa sote tuliumbwa na Mungu ambaye ni mfadhili wetu na ndiyo maana anasema 'Sote tumwasilishie malalamiko yetu.'

Anaendelea kuonyesha kwamba kadri watu wanavyozeeka ndivyo matatizo yao ya maisha yanavyoongezeka. Hii ina maana kwamba ni muhimu watu kupanga maisha yao ya baadaye kama wangali na nguvu. Mtu asiyefanya hivyo huishia kujuta. Hii ndiyo maana akasema:

> Yaelekea kadiri tunavyozeeka
> Na matatizo ya maisha kuongezeka
> Twazidi kuyakumbuka maksia
> Tuliyotundika ukutani ujanani.

Shairi hili linaonyesha kwamba vijana wana nafasi muhimu katika jamii. Wana nguvu na wanaweza kutekeleza mambo mengi katika jamii. Mshairi anatafakari kuhusu maisha mazuri waliyoyapitia wakiwa vijana. Anatumia taswira ya 'makasia' kueleza kuwa mambo mengi maishani hufanywa katika ujana kwa sababu wana nguvu na maono. Yale tuyafanyayo ujanani tutayakumbuka uzeeni. Makasia hutumiwa katika kuendesha chombo mbele ili usafiri ufanikiwe baharini. Hivyo, maisha ya mtu uzeeni hutegemea jinsi alivyoishi akiwa kijana.

Jamii yaweza kuendelea tu kukiwa na uelewano kati ya wanajamii. Anatoa wito ya kwamba ni muhimu 'Kuziba matundu ya mtumbwi wetu'.Mtumbwi unaashiria asasi ya jamii au nchi. Ni muhimu kuondoa vikwazo vinavyoweza kuikwamisha na kuirudisha jamii nyuma. Vikwazo vya kijamii ambavyo vimeashiriwa kwa matunduni pamoja naukabila, ufisadi, upendeleo, uonevu, chuki, kukosa maono na mipangilio mahsusi ya maisha ya baadaye.

Kulingana na mtunzi, ni muhimu kujiandaa kutenda mema. Tukitenda wema, hatima yetu itakuwa nzuri. Anasema:

> Tuzibe matundu ya mtumbwi wetu
> Na tupige makasia tuelekee
> Kwenye kisiwa cha uzima wa milele
> ...hapa duniani tu wasafiri.

Mtumbwi hauwezi kwenda mbele bila wapiga makasia kushirikana pamoja. Kwa hivyo, ni muhimu wapiga makasia kuelewana na kuwa kitu kimoja ili nguvu zao zizalishe matunda na mtumbwi uwafikishe wasafiri ufuoni. Iwapo waendesha mtumbwi hawatavuta pamoja, mtumbwi hautaweza kuendelea. Utazama kabla ya kufika ufuoni na wasafiri wataangamia. Anatuhimiza kuelewa kuwa hapa duniani sisi ni wasafiri. Maisha yetu ni mafupi. Kwa hivyo, tujue namna ya kuishi. Tukiishi vyema, hatima yetu pia itakuwa njema. Ni maisha kama haya ndiyo yenye neema, baraka, ufanisi na tumaini.

Mtunzi anaonyesha ya kwamba katika ulimwengu wa leo, kuna changamoto nyingi. Changamoto hizi zimechangiwa na usasa ambao umewafanya wanajamii kugongana. Usasa huu umejitokeza kama mwamba imara ambao umekuwa kikwazo katika jamii.

Miongoni mwa mambo yanayotokana na usasa kwa mujibu wa mtunzi ni utovu wa maadili. Kwa sababu hii, mtunzi anaonyesha kuwa watu hawana uhakika katika maisha yao. Wao wanaishi maisha nusunusu. Anatumia vipande vya mtumbwi kueleza hili.Kwa hali hii, watu wanaishi kwa majonzi kwa sababu ya mivutano ya kijamii, ukosefu wa amani, heshima na utu. Anasema kuwa:

Kunywa vikombe vya majonzi
Na kula ukoko wa mateso
Kati ya vilio vya maskini
Na ngumi za matajiri.

Jambo linalojitokeza hapa ni kwamba zamani hakukuwa na utabaka ambao upo katika jamii ya sasa. Kuna tabaka la matajiri na maskini. Katika hali hii, walio maskini wanateseka kwa sababu ya kudhulumiwa, kukandamizwa, kuonewa na kubebeshwa mizigo ya kila aina na matajriri. Wito wa mtunzi katika shairi hili ni kwamba kuwe na mageuzi maalum ili watu waishi kwa uadilifu. Kwa njia hii kutakuwa na heshima, amani, upendo na kuelewana.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni hali ya watu kujitambua na kujua kuwa yafaa waishi maisha adilifu na kutumia nguvu zao kwa busara wakiwa vijana. Pia, kuishi bila utabaka kwani mwishowe sote tutarudi kwa Mungu, tuwe matajiri au maskini.

### 5.3 Shairi: 'Wimbo wa Unyago'

Katika shairi hili, Kezilahabi angependa msomaji atambue ulimwengu wake. Angependa msomaji kujichunguza na kujielewa ili aishi vyema. Ili Hayo Kuafikiwa, ni muhimu

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kuangalia mwanda mzima wa maisha. Mtunzi angependa wasomaji wahoji na wachunguze nafsi zao, mazingira yao, ujitambuzi nafsi wao, ulimwengu wao na hata maisha yao wenyewe. Shairi hili ni wimbo wa unyago kwa ambavyo ni nasaha. Mtunzi anatoa ushauri wake kuhusu namna ya kuishi. Wito wake ni kwamba watu waishi vyema na kufaulu maishani.

Anawasisitizia vijana kuishi maisha yao na wazee waishi yao. Ili watu wote waweze kuishi vizuri, kuna vitu ambavyo vijana wafaa kuepukana navyo, kama vile ukabila. Kwa mujibu wa mtunzi, ukabila ni utumwa na humfanya mtu asiishi vizuri. Anawashauri wasichana waolewe kulingana na mapenzi yao bali si kushurutishwa.

Ametumia msemo 'Achaguaye embe bichi, ajua lini litaiva.' Ametumia msemo huu kuonyesha kuwa ni muhimu watu wapewe nafasi ya kujichagulia na kujiamulia mambo. Jambo hili katika muktadha wa maisha ya jamii ni muhimu pale ambapo maamuzi yanahusu masuala ya ndoa. Mshairi anatahadharisha dhidi ya watu wanaonena mambo mengi katika jamii. Kwake, watu kama hao huwa wanafiki na wadanganyifu. Ametumia mfano wa 'Akuandikiaye barua ndefu hana la kusema'.

Anaendelea kushauri kwamba watu ambao ni wajuzi wa kusema wanaweza kuwateka nyara wenzao. Hii ndiyo maana akatumia msemo wa 'Mbwa kuwekwa utumwani kwa kifupa kiso mnofu.' Maishani, tunaweza kutekwa nyara kwa kuwa wapumbavu kwa kushawishiwa, hususan kupitia maneno matamu. Kwa hivyo, tuwe waangalifu.

Kezilahabi anasema ya kwamba, ili jamii ipate kuendelea, kuna umuhimu wa kupanga uzazi. Anasema:

Ee mama mwenye rutuba

Zaa, zaa kwa mpangilio

Si kufyatua matofali.

Wito ni kwamba watu wazae idadi ya watoto ambayo wataweza kuwalea na wazingatie afya zao zisiangamizwe. Anaonyesha ya kwamba, watu wanakuwa watumwa kwa kuzaa bila mpango.Wasipokuwa na mipangilio mizuri maishani, wanajinyima uhuru wa kufurahia maishana kuwa watumwa wa hali mbalimbali, hasa mateso.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni wosia kuwa yafaa watu wajidadisi kama watembeaji wanaoielewa njia yao. Kila mtu awe kijana au mzee apewe nafasi yake katika maisha na uhuru wa kuchagua bila kushurutishwa. Zaidi sana ni muhimu kupanga uzazi kwa kuwapata watoto ambao mtu ana uwezo wa kuwalea.

**5.4. Shairi: 'Makaburini'**

Kezilahabi anaelezea masaibu yanayowakumba watoto yatima. Kwa mfano, mtunzi anaonyesha ya kwamba, dadake mhusika (mvulana) husingiziwa umalaya. Anakemewa bila sababu kwa ajili ya kuonewa na kuchukiwa. Kwa upande mwingine, mvulana naye anakemewa na kutukanwa kwa kuambiwa ya kwamba ameambaa tabia ya ulevi kama babake. Pia, msichana anaambiwa kwamba nibahili na mchoyo kama mamake. Anasema:

Kila siku tu mlizamu wa sababu

Tu wadudu ndani ya kokwa

Kipoteacho 'ukome wizi wa babako.'

Kwa mwenzangu, 'umalaya wa mamako ukome.'

Tena kwangu 'ulevi wa baba'

Huo ndio urithi mliotuachia.

Ubeti huu ni taswira kamili ya mateso wapitiayo watoto yatima katika jamii ya sasa. Kama wadudu ndani ya kokwa, wale wanaoishi nao huwatesa. Kwa mfano, kitu kipoteapo yatima ndio wanaosingiziwa. Hali hizi ngumu huwasukuma yatima kujuta na kujaribu kusemezana na wazazi wao walio makaburini. Mvulana anauliza kama huo ndio urithi walioachiwa, wa mateso na majuto duniani.

Katika ubeti wa pili anakariri kuwa wanaitwa majina 'Maskini na yatima ambayo ni kweli'. Anatumia mbinu rejeshi kushadidia kauli kwamba wazazi walikuwa mfano bora wa kuigwa lakini sasayatima hawa wanauza kwenye baa. Kuwanawisha wateja mikono waliokula mbuzi, ng'ombe na kitimato. Ni kinaya kwamba, wanapoyafanya haya yote, wenyewe hawana chakula.

Mhusika yatima anakumbuka ya kwamba mali hii ilikuwa ya wazazi wake. Anamalizia kwa kusema kuwa 'Twachoma utajiri kuzalisha utajiri'. Hii inmaanisha kuwa, wamepokonywa utajiri wao na kutumiwa kufanya kazi kwa utajiri huo ili kumnufaisha dhalimu ambaye ni ami yao.

Anatumia taswira kupitia mbinu rejeshi kuwa waliokuwa nao darasa moja ni wasomi ilhali wao wamevalishwa sare 'Milimani baa'. Hii ni kinaya kwa kuwa yatima hawa wanateseka kwa kutoenda shuleni jinsi wenzao waliosoma nao walivyosoma. Anawazungumzia wazazi wao makaburini kwa kuwaeleza ya kwamba wao (yatima) ni watumishi wa 'Ba mkubwa'. Mtunzi anasema utajiri wa 'ba mkubwa'ulitokana na

kuwapokonya yatima mali waloachiwa na wazazi wao. Istoshe, amewafanya watumishi wake. Aidha, ni 'Mkali-chui'. Istiari hii inadhihirisha kwamba 'Ba mkubwa' ni mkali na dhalimu anayewatesa na kuwanyanyasa yatima.

Mtunzi anatumia mbinu ya utabiri kuonyesha kuwa siku za mbeleni watapata mateso mengi zaidi. Anasema:

Kesho tutakuwa vitambaa
Vya kusafisha mikono chooni
Na tutafuliwa kila wiki
Ndani ya karai kutu la machozi yetu
Kesho kutwa tutatupwa vidazo jalalani
Baba, baba, mama. Ndisi.

Hii inaonyesha jinsi yatima hawa wataendelea kuteseka hata zaidi kwa mikono ya mtu ambaye angefaa kuwajenga na kuwakuza ili wawe na maisha mema kama wenzao.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni hali katika jamii ambapo yatima wanateseka sana kwa mikono ya jamaa zao ambao wanafaa kuwa vielelezo. Watoto hao wanateseka kwa kufanywa wafanyakazi wa kazi duni kama vile kuuza kwa baa badala ya kupewa elimu.

**5.5 Shairi: 'Hoja'**

Katika shairi hili, mtunzi anajaribu kubainisha falsafa yake kuhusu maisha. Anadhihirisha ya kwamba unyanyasaji umekithiri katika jamii. Watu hawajali hisia za wenzao. Anatuchorea taswira ya namna wanyonge wanavyoangamizwa. Ni kinaya kwamba wanyonge wanadhulumiwa na dhalimu anaona kuwa hiyo ni haki yake.

Anaonyesha ya kwamba, tabia za wanadamu zinafananishwa na za wanyama kwa kukosa utu. Anashutumu ya kwamba, tabia za wanyama zinawafaa wanyama na sio binadamu. Binadamu akikosa utu na kutenda matendo yasiyofaa ni jambo linalofaa kumshughulisha kila mwanadamu katika jamii. Mienendo kama hiyo haipaswi kuruhusiwa katika jamii ili watu wapate maendeleo. Mienendo isiyofaa inakera na haina uadilifu.

Katika aya ya kwanza anatuchorea taswira ya mbuga la wanyama ambapo simba dume anamfukuza pundamilia, anamrukia juu na kumng'ata shingoni. Hali kadhalika, punda milia anaanguka chini kwa ukemi, simba anamrarua kuanzia tumboni, hivyo anakuwa mlo kwa ubabe wa simba. Vilevile, nyani wanatazama wakibweka kwa kuwawanaona kitendo hicho ni uzuri wa sanaa ya Muumba. Hata hivyo, tanzia ni kuwa nyani mwenyewe anauawa baada ya muda mfupi. Mtunzi anaona si hoja kwa kuwa ni wanyama.

Kezilahabi anasema:

> Lakini
> Nikakumbuka habari nilizosoma
> Nikiwa ndani ya daladala:
> Jana jioni kijana mmoja
> Jinale limehifadhiwa
> Alimbaka msichana
> Wa miaka kumi na sita.
> Dhuluma ya ubabe huweza kuharibu
> Haiba-hukla ya utu kwa muda mfupi…

Anatumia mbinu rejeshi kueleza aliyoyasoma akiwa ndani ya daladala. Habari aliyopata ni kuwa kijana mmoja ambaye jina lake limehifadhiwa alimbaka msichana wa miaka kumi na sita. Dhuluma hii ya kimapenzi inatokana na ubabe wake, jinsi tulivyoona ubabe wa simba. Ubabe huu huleta madhara kwa wanajamii. Anamalizia kwa kusema kuwa, raha na ukiukaji wa utu kwa muda mfupi husababisha adhabu ili kurekebisha tabia hii isiyojali utu. Mtunzi anasema kuwa anakereka. Anawashauri wanadamu wajirekebishe mapema.

Mazingira yaliyoibua utunzi huu ni masuala nyeti ambayo yanatokea katika jamii kutokana na usasa. Maovu kama vile ubakaji, unyanyasaji, ukandamizaji na uoenevu hasa kwa wanyonge unaendelea na hakuna anayejali. Hata dhalimu mwenyewe anaona kuwa ni haki yake kuwadhulumu wanyonge.

**5.6 Shairi: 'Namagondo iii'**

Katika shairi hili, Kezilahabi anaongea kuhusu mabadiliko katika kijiji chake. Anasema haya kama mtu anayekielewa kijiji chake vyema. Alizaliwa na kukulia pale kijijini. Hili linadhihirika anaposema:

> Najua hapa nilivuta pumzi ya kwanza
> Na labda ya mwisho nitaitoa hapa
> Roho yangu itakuwa imechakaza viatu
> Penye miiba, tope, moto na mazulia.

Katika dondoo hili, anaeleza kuwa ataenda kotekote nahata kuishi hadi kuzeeka. 'Miiba' inaashiria maisha machungu ambayo ameyapitia akiwa katika safari yake ya kutafuta maisha hapa ulimwenguni. 'Matope' yanaashiria matatizo ya maisha, huku 'Moto'

unaashiria yale machungu anayoyapitia binadamu katika maisha yake. 'Mazulia' nayo ni ishara ya maisha mazuri ambayo mtunzi ameishi.

Mshairi anasema kuwa ataishi maisha hadi siku yake ya kifo na atakuwa ameishi maisha yake mazuri. Atapokeza wengine mbinu ya kutafuta maisha naye ayaage kwa heri. Miti ni taashira ya maisha ya mashambani na anasema kuwa bado ana nafasi yake kule kijijini.

Kwa kusema kuwa 'Wahenga naja bila kalamu'. Anaashiria kuja bila kuwajulisha watu. Anaomba apewe nafasi yake katika maisha haya ya mzunguko. Anafuraia maisha ya mashambani hasa ya ukulima na kutilia mkazo umuhimu wa maisha ya nyumbani licha ya mabadiliko yatokeayo. Anajivunia maisha ya kwao nyumbani na kusema kazi mtu afanyayo ni muhimu hasa ya nyumbani. Mtunzi kama msomi amesafiri kotekote na licha ya haya, amegundua kuwa nyumbani ndimo mna utulivu. Anashauri watu kuwa maisha ni kama safari ndefu na utulivu upo tu kwenyu nyumbani.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni uelewa wa jamii alimozaliwa mtunzi. Anaielewa jamii yake na hasa kijiji chake alikozaliwa na kukulia. Mtu husafiri akaenda sehemu mbalimbali za ulimwengu kwa shughuli za kimasomo au kikazi lakini mwishowe mtu hurudi nyumbani ambapo alizaliwa ili kukamilisha safari yake ya maisha.

### 5.7 Shairi: 'Msamaha'

Kezilahabi anabainisha umuhimu wa msamaha katika maendeleo ya jamii. Jambo hili halina manufaa tu katika familia bali pia katika taifa nzima. Familia ndiyo msingi wa taifa. Familia inapokaa vizuri, taifa pia huwa na amani.

Kezilahabi anaongea kumhusu mhusika ambaye ametambua makosa yake na sasa anaomba msamaha. Pale ambapo kuna msamaha, watu hupata maridhiano, amani, na utangamano. Kulingana na mtunzi, mhusika alimkosea sana mkewe. Alimdhuru na vilevile kumsababishia madhara makubwa. Jambo hili linatokana na sababu ya kwamba hata watoto walishuhudia nao majirani wakasikia. Mtunzi anaashiria kwamba kosa hili lilitendeka hadharani. Lilikuwa na kumwaibisha mkewe na kuumbua utu wake.

Taswira ya uso kuvimba ni tokeo la mikono yake chafu inaashiria mume alitenda kitendo cha kinyama cha kumpiga mkewe. Mume anakiri ya kwamba hakushawishiwa na pombe wala hasira bali ni yeye mwenyewe. Hatua hii inaonyesha uponyaji unaweza kupatikana katika ndoa na jamii kwa jumla iwapo wanaohusika watatambua makosa yao. Wawe jasiri wa wakubali na kuwajibika ipasavyo. Kuomba msamaha si ishara ya udhaifu bali ni kitendo cha busara.

Katika kutambua makosa na kunyenyekea, jamii hupata uponyaji, maridhiano na maendeleo.

Mtunzi anasema:

> Najua nimekosa sana. Naomba msamaha.
> Watoto waliona, majirani walisikia.
> Uso wako ulivimba
> Tokeo la mikono yangu hii michafu.

Ingawa shairi hili limelenga msamaha katika kiwango cha familia, linaweza pia kuashiria msamaha katika kiwango cha taifa. Hasa pale ambapo wanajamii wametengana kwa misingi mbalimbali. Kwa mfano, chuki za kikabila zinazochochewa na viongozi, uonevu

na upendeleo unaosababisha baadhi ya wanajamii kutengwa katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya taifa. Ufisadi unaoambatana na maongozi mabaya ya kuibia umma, tamaa na ubinafsi. Katika hali kama hii, ni muhimu wale wahusika kuomba msamaha hadharani ili taifa lipate uponyaji, uelewano, maridhiano na utangamano. Hatua hii inaweza kuchangia amani, upendo na kuondoa kutenga baadhi ya wanajamii katika shughuli za kitaifa. Matokeo yake yatakuwa uzalendo na umoja.

Mazingira yaliyoibua shairi hili ni kutaka kuleta amani na uelewano kutokana na kuomba msamaha kama hatua muhimu na busara katika jamii yoyote.

### 5.8 Muhtasari

Sura hii iliangazia masuala ya kijamii hasa yanayoikumba jamii ya sasa. Mambo haya ni kama vile kukengeuka, unyanyasaji, ubakaji na hata umuhimu wa kuomba msamaha. Mambo haya yamemulikwa na mtunzi. Kama mwanajamii, anayaangazia masuala nyeti yanayoikumba jamii hii. Anatoa wosia kuwa ili tuishi vyema yafaa kuishi na kutenda wema kama bado tungali hai.

Sura iliyofuata iliangalia hitimisho, matokeo ya utafiti, changamoto za utafiti na mapendekezo ya utafiti zaidi.

# SURA YA SITA

## Hitimisho, Matokeo na Mapendekezo ya Utafiti

### 6.1 Muhtasari

Utafiti huu ulibaini aina ya maudhui yaliyowasilishwa na mtunzi wa *Dhifa,* namna maudhui hayo yalivyowasilishwa na jinsi mazingira ya kihistoria na kijamii yaliibua maudhui ya diwani ya *Dhifa* (2008).

Uteuzi wa diwani ya *Dhifa* ulichochewa na wazo kwamba diwani hii imesheheni mashairi yaliyotungwa kutathmini iwapo malengo ya Azimio la Arusha yalitimia nchini Tanzania. Azimio hili lilitarajiwa kuwa jua la nchi hii kwa kuleta haki, usawa na ujamaa kwa kuondoa athari za kikoloni. Istoshe, diwani hii inamulika masuala muhimu ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yanayoikumba jamii ya mtunzi katika kipindi cha utunzi.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura sita. Sura ya kwanza ilijadili masuala ya kikaida kwa mujibu wa kazi yautafiti. Mambo hayo ni: Utangulizi wa utafiti ambao unauwekea utafiti huu msingi kwa kuonyesha namna fasihi, ushairi ukiwemo humulika masuala yanayotendeka katika jamii na kuonyesha athari ya mazingira katika uwasilishaji wa maudhui ya kazi yoyote ya kifasihi. Pia, kuonyeha namna mtunzi kama mwanajamii huathiriwa na mazingira alimokulia na kuzungukwa nayo na jinsi athari hizo zinavyojitokeza katika kazi za mtunzi teule.

Isitoshe, sura hii ilijadili swala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti na sababu za kuchagua mada ambazo tulitaja hapo awali katika sura hii. Pia, sura hii ilijadili upeo na mipaka ya utafiti ambapo tumeeleza kwamba utafiti huu ulishughulikia mashairi ishirini

na moja. Vilevile, ilijadili yaliyoandikwa kuhusu mada ili kuonyesha nafasi na mchango wa kazi zilizotajwa kwa utafiti huu na katika taaluma ya utafiti wa mashairi.

Sura ya kwanza vilevile ilijadili nadharia iliyotumiwa kuongoza utafiti huu ambayo ni nadharia ya uhistoria mpya. Utafiti uliangazia waasisi wa nadharia hii na pia kuonyesha mihimili muhimu ya nadharia hii iliyoufaa utafiti. Kadhalika, sura hii ilijadili mbinu za utafiti ambapo mbinu kuu ilikuwa usomaji wa maktabani. Kitengo kingine kilichojadiliwa katika sura hii ni sampuli na uteuzi wa sampuli. Utafiti huu ulitumia mbinu kusudio kuteua mashairi ishirini na moja yenye maudhui ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo yalichanganuliwa. Mbinu za kukusanya data zilizojadiliwa katika sura hii ni kusoma na kuchanganua mashairi teule pamoja na utoaji wa mifano mwafaka katika mashairi husika. Data ilikusanywa kutokana na mashairi hayo teule na kisha kuwasilishwa kwa njia ya kimaelezo.

Sura ya pili iliangalia mazingira ya mtunzi kwa lengo la kuelewa msingi, muktadha na chimbuko la maudhui ya diwani teule na namna mazingira yake yalivyouathiri utunzi wake. Pia, iliangalia vipindi tofauti vya kihistoria katika nchi ya Tanzania. Hivi ni kabla ya uhuru, baada ya uhuru hasa baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha kwa matarajio kwamba ulinganishi wa vipindi hivi katika maisha ya Watanzania ungetuwezesha kueleza maudhui na dhamira ya mtunzi na hivyo kutuwezesha kueleza athari ya mazingira ya kijamii na kihistoria katika uwasilishaji wa maudhui ya *Dhifa.*

Sura ya tatu ilijadili maudhui ya kisiasa. Kezilahabi anaongea kuhusu hali ya kisiasa nchini Tanzania na harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Mashairi katika sura hii

yanatathmini kufaulu kwa Azimio la Arusha na hali ya uongozi nchini Tanzania na mataifa changa ya bara la Afrika. Mfumo wa uongozi unaendelea kuathiri maendeleo na hata kudhulumu umma bila kujali.

Katika sura ya nne, utafiti ulichanganua maudhui ya kiuchumi. Kezilahabi anadhihirisha ya kwamba, utunzi huakisi uyakinifu na uhalisia wa mazingira ya mtunzi kwa kuzingatia matukio ya kihistoria ya wakati wake. Sura hii ilibainisha kwamba Kezilahabi kama mtunzi anaielewa jamii yake na anajitokeza kama mwanafalsafa anayezungumzia ujenzi wa jamii mpya kiuchumi hasa baada ya uhuru.

Mtunzi anaelekeza silaha zake dhidi ya mfumo wa kibepari ambao ndio adui wa mataifa changa ya Kiafrika. Anachambua hali halisi ya Tanzania baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha. Mashairi yaliyochaghuliwa yanaonyesha athari za mfumo wa kibepari kwamba mfumo wa kikoloni umekita mizizi kwa jamii ya sasa na kuathiri uchumi wa nchi ambao umezorota kutokana na uongozi wa nchi ambao unatoa mwongozo usiotegemewa wala kujali umma.

Sura ya tano ya utafiti iliangazia maudhui ya kijamii katika nchi ya Tanzania kwa kumulika masuala ya kijamii yanayoikumba jamii ya sasa. Masuala haya ni kama mabadiliko yanayompata mtu aliyekuwa katika hali duni anapobadilika na kuanza kuwadhulumu wale alioishi na kushiriki nao kwa kuwafanya wamuabudu. Pia, masuala kama dhuluma kwa wanyonge yanajitokeza na wadhalimu wanaona ni haki yao kuwanyanyasa wanyonge. Unyanyasaji huo unadhihirika kupitia kwa matajiri kuwatesa wanyonge, watu kutesa yatima, ubakaji na hata kutojali mazingira.

Watu walio na nguvu hutumia ubeberu wao kuwatesa maskini katika jamii kwa kuwa mfumo wa udhalimu hauwapi wanyonge sauti ya kujitetea. Wao ni kuonekana tu bali si kunena. Masuala ya kuchumbiana na ndoa pia yanajitokeza wazi katika sura hii kwa kuwapa vijana haki ya kujichaghulia maisha ya ndoa bila kushurutishwa. Pia, kuna masuala yanayohusiana na msamaha ambapo mtunzi anaonyesha umuhimu wa kuomba msamaha hasa katika kuleta umoja na uponyaji katika jamii. Kuwa, msamaha ni hatua muhimu sana katika kuleta umoja bali si ishara ya udhaifu.

Katika sura ya sita ambayo ndiyo ya mwisho, utafiti uliangazia muhtasari wa kila sura na matokeo ya utafiti kwa kina, huku kila lengo likichunguzwa na kukadiriwa iwapo lilitimizwa au la. Sura hii pia iliangazia mchango wa kazi hii katika ushairi wa Kiswahili na kubainisha kwamba utafiti umeshadidia tafiti za awali na utawafaa wanafunzi shuleni, wasomi vyuoni, watafiti wa ushairi na wakuza mitaala hasa inayohusiana na athari ya mazingira katika uwasilishaji wa maudhui ya ushairi wa Kiswahili. Vilevile, sura hii ilijadili changamoto za utafiti na mapendekezo ya utafiti zaidi.

## 6.2 Matokeo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yalikuwa, kubainisha maudhui yaliyowasilishwa na mtunzi wa *Dhifa,* kueleza namna maudhui hayo yalivyowasilishwa na kubainisha mazingira ya kihistoria na kijamii yaliyoibua maudhui teule.

Kuhusu lengo la kwanza lililokuwa kubainisha maudhui yaliyowasilishwa na mtunzi wa *Dhifa.* Utafiti ulipata ya kwamba, maudhui yaliyoshughulikiwa ni pamoja na maudhui ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kuhusu maudhui ya kisiasa, utafiti ulionyesha ya kwamba

malengo ya uhuru husus an baada ya Azimio la Arusha hayakutekelezwa kwa sababu ya ubinafsi, na utekelezaji ambao ulitetereka. Ukoloni mkongwe uliendelea katika umbo la ukoloni mamboleo na kudhihirika miaka mingi baada ya uhuru na Azimio la Arusha. Mtunzi anabainisha ya kwamba, ili suluhisho mwafaka kupatikana, wananchi hawana budi kuzinduka na kutekeleza majukumu yao vilivyo. Wanapaswa kuhamasishwa vilivyo ili kuleta mapinduzi yenye maana. Jambo hili kulingana na mtunzi linahitaji mapambano makali.

Kuhusu maudhui ya kiuchumi, utafiti ulipata ya kwamba, hata baada ya Azimio la Arusha, jamii ya Watanzania ilibakia ya kitabaka. Kulikuwa na wachache hasa viongozi na vikaragosi vyao kwa kuongozwa na tamaa. Waliwanyanyasa walio wengi kwa sababu ya ukiritimba, unyonyaji na udhalimu. Kwa jinsi hiyo, walio wachache walifurahia matunda ya uhuru wakakimbilia makombo yaliyoachwa na wakoloni na kujinufaisha kibinafsi. Vilevile, walihodhi nyenzo za uzalishaji mali na kuendeleza ukiritimba. Kwa hivyo, utafiti ulipata ya kwamba, ingawa maazimio ya Arusha yalikuwa mazuri, ya kuondoa utabaka kiuchumi, unyonyaji na ukandamizaji. Utekelezaji haukufaulu kwa hivyo, hali ya wengi hasa wakulima na wafugaji iliendelea kuwa duni kwa sababu ya kunyanyaswa na mfumo wa ubepari. Hali ya walio wengi itaweza kubadilika tu pale ambapo watajitokeza na kupigania haki zao kwa dhati.

Kuhusu maudhui ya kijamii, utafiti ulipata ya kwamba watu wanapopanda cheo, hujisahau kwa haraka. Kwa mfano musika ambaye ni Monika, maisha yake ya awali yalikuwa duni, lakini baada ya kuoleka na waziri maisha yake yalibadilika na mienendo yake pia. Kutokana na haya, alianza kuwadharau na kuwaambia watu alioshiriki nao hapo

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

awali katika hali yake ya uduni wamshangilie kwa kumpigia makofi kila apitapo. Pia, tulipata kuwa watu hasa vijana wanapaswa kupewa uhuru wa kuamua kuhusu mambo hasa ya ndoa bila kushurutishwa na jamii. Kuna umuhimu wa kuomba msamaha katika kuleta usawa na uponyaji katika jamii.

Kuhusu athari ya mazingira ya kihistoria na kijamii katika uwasilishaji wa maudhui, utafiti ulipata ya kwamba, mazingira ya kihistoria na kijamii huathiri utunzi wa msanii kifani na kimaudhui pamoja namwelekeo. Utafiti uliangazia Tanzania wakati wa ukoloni baada ya uhuru na baada ya Azimio la Arusha. Ulinganishi wa vipindi hivi tofauti katika historia ya Watanzania ulituwezesha kueleza maudhui, dhamira na fani alizotumia mtunzi. Kuhusu wakati wa ukoloni, utafiti ulipata ya kwamba wakoloni polepole walitumia hila ili kuwafanya Waafrika wapuuze na kudunisha utamaduni wao wa Kiafrika.

Kwa upande mwingine, waliwafanya Waafrika kuutukuza utamaduni wao wa kikoloni hivyo kuzamisha mirija ya kuendelea kuwategemea. Aidha, Waafrika waligawanywa kitabaka na kikabila. Wachache waliowaunga mikono walinufaika na utawala wa kikoloni. Viongozi wa Afrika walioteuliwa katika utawala wa kikoloni walikuja kuwa vifaa vya utawala wa kikoloni. Hivyo, uchumi wa kikoloni uliwaathiri Waafrika kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, ulihimiza ubinafsi ulioambatana na unyonyaji usiojali utu. Aidha, kulikuwa na ubepari ambao uliambatana na ulimbikizi wa mali kwa manufaa ya wachache.

Utafiti pia ulipata ya kwamba, kabla na baada ya Azimio la Arusha nchini Tanzania, ilikuwa muhimu kwamba Tanzania iwe na sera mpya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni ili malengo yake ya kupigania uhuru yatimizwe. Hata hivyo, sera za Tanzania huru kabla na baada ya Azimio hazikufaulu kutokana na sababu za nje na ndani ya nchi. Kwa mfano, kulikuwepo na nguvu katika medani ya biashara ya kimataifa ambapo serikali ilishindwa kuleta maendeleo yaliyotarajiwa. Kwa hivyo, bei ya mazao iliporomoka kwa ghafla katika soko la kimataifa.

Kwa upande mwingine, viongozi wa Kiafrika walikimbilia makombo yaliyoachwa na wakoloni na kudidimiza malengo ya uhuru na ya Azimio la Arusha kwa sababu ya mfumo wa ukoloni mamboleo. Utafiti vilevile ulipata ya kwamba, mashairi yaliyotungwa hasa baada ya Azimio la Arusha yalifungamana na hali ya mazingira kwa mujibu wa wakati kwa ambavyo yalikuwa ya kutathmini na kuhakiki kufaulu kwa malengo ya Azimio la Arusha. Kutathmini huko kumebainika katika nyanja zote za maisha ya jamii, hivyo, mtunzi amejitokeza kama mwangalizi, mwalimu na vilevile macho ya jamii. Utafiti ulionyesha kuwa anaweza kukejeli, kutahadharisha, kukashifu, kuelimisha na vilevile kuzindua jamii ili kujenga jamii iliyobora zaidi.

Utafiti ulibainisha ya kwamba, nadharia ya Uhistoria Mpya ilikuwa na mihimili mwafaka iliyoongoza utafiti huu. Kwa mfano, ilionyesha ya kwamba, muktadha ambamo kazi za kifasihi hutungiwa husaidia kuelewa mazingira yanayochipuza utunzi fulani. Aidha, mihimili yake ilisaidia kuelewa mabadiliko ambayo yametokea katika jamii ya Watanzania kutokea wakati wa ukoloni hadi sasa. Vilevile, suala la mwingiliano matini

hususan matukio ya kiyakinifu ya kihistoria yamesaidia kuelewa athari ya mazingira ya kihistoria na kijamii katika uwasilishaji wa maudhui ya diwani ya *Dhifa.*

### 6.3 Changamoto za Utafiti

Utafiiti huu ulikumbwa na changamoto kadha. Changamoto kuu ilikuwa pale ambapo tulichanganua maudhui ya kisiasa na kiuchumi. Mashairi yaliingiliana sana kiwango cha kutoweza kuyatofautisha vizuri. Vilevile, kulikuwa na ugumu wa kufasiri mashairi ya kifalsafa yanayojikita katika falsafa ya mtunzi binafsi.

### 6.4 Umuhimu wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu utawafaa wasomi wa fasihi, hasa ushairi, wahakiki, watafiti wa mashairi na wakuza mitaala. Hii ni kwa sababu ni kupitia kwa maudhui na namna yalivyowasilishwa ndipo hadhira na wasomaji hupata lengo na dhamira ya mtunzi. Watafiti watasaidika kwa kusoma kazi hii na kuuwekea utafiti wao msingi. Wakuza mitaala watafaidika kwa kuteua vipengele vinavyohusiana na uchambuzi wa maudhui ya ushairi wa Kiswahili.

Watunzi wa ushairi watafaidika kwa kuelewa namna mazingira ya kihistoria na kijamii huathiri utunzi wa mashairi, kando na falsafa ya mtunzi mwenyewe.

### 6.5 Mapendekezo

Utafiti huu ulidhamiria kubainisha athari ya mazingira ya kihistoria, kiuchumi na kijamii katika uwasilishaji wa maudhui ya *Dhifa*. Hata hivyo, utafiti huu ulibaini maudhui ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na namna yalivyojitokeza katika diwani teule. Utafiti huu ulijikita katika mazingira ya nchi ya Tanzania, utafiti zaidi wa aina hii unaweza kufanywa kuhusu mazingira ya Kenya kwa kuzingatia kipindi cha ukoloni na awamu mbalimbali za uongozi.

## MAREJELEO

Abdalla, A. (1972). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.

Adagala, K. (1981). *Petals of Blood: A Study of Women Question and Imperialism.* Karatasi ya Semina ya Wakufunzi. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Anene, J. na Brown, G. (1966). *Africa in thee 19th and 20th Centuries:* A handbook for Teachers and Students. Ibadan University Press.

Apondi, R. (2014). *Usawiri wa Katiba Mpya ya Kenya. (2010) katika Mashairi ya Uongozi ya Kithaka Wa Mberia.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Babusa, H. (2005). *Vigezo Badala Kuhusu Uainishaji wa Mashairi ya Kiswahili.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Boesen, J. na Wengine. (1977). *Socialization from Above.* Uppsala: Scandinavian Institute of African Studies.

Brett, E. (1973). *Colonialism and Under-development in East Africa*. Nairobi: H.E.B.

Chacha, N. (1987). Ushairi wa Abdilatif Abdalla: *Sauti ya Dhiki*.Dar es Salaam. Dar es Salaam University Press.

Ndwiga, P. (2013). *Mtindo katika Mashairi ya Diwani ya Karne Mpya*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Fanon, F. (1963). *The Wretched of the Earth*. Paris: Presence Africainne.

Faucault, M. (1997). *The Order of Things.* London: Routeledge and Kegan Limited.

Gakuo, J. (2014). *Changamoto za Uchanganuzi na Ufasiri wa Ushairi katika Shule za Upili Nchini Kenya.* Tasnifu ya Ph.D. Nairobi. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Gicuku, M. (2011). *Usawiri wa Maudhui ya Ndoa katika Ushairi wa* Euphrase Kezilahabina Kithaka wa Mberia. Tasnifu ya M. A. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Greenblatt, S. (1980). *Renaissance Self-Fashioning.* Chicago: University of Chicago Press.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi.* Nairobi: Heinmann Education Books.

Kezilahabi, E. (2008). *Dhifa.* Nairobi: Vide-Muwa.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi.* H.E.B. Nairobi.

Kezilahabi, E. (1988). *Karibu Ndani.* Dar es Salaam.

Khatib, M. (1975). *'Washairi wa Kiswahili Wanavyoliona Azimio la Arusha'*katika Kiswahili, Juzuu 45/2. Jarida la TUKI, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

King'ei, K. (2000). *Miale ya Uzalendo.* Nairobi: Phoenix Publishers.

King'ei, K. na Kemoli, A. (2001). *Taaluma za Ushairi.* Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

King'ei, K. na Kisovi, N. (2005). *Misingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kombo, K.na Tromp, A. (2006). *Proposal and Thesis Writing. An Introduction.* Nairobi: Pauline Publishers.

Madumulla, J. (1988). *Riwaya ya Kiswahili Tanzania*, katika MULIKA no. 20. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Massamba, D. (2003). *Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili*. Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili iii. Fasihi. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Dar es Salaam.

Masinde, E. (1992). *Mashairi Huru: Uchambuzi wa Dhamira na Mtindo.* Tasnifu ya M.A. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Masinde, E. (2002). *Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui.* Tasnifu ya Uzamifu. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mlacha, S. (1984). '*Riwaya za Visiwani (1970-1980) na ujenzi wa jamii mpya*' katika Mulika na. 16. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Matteru, M. (1975). *Sauti ya Dhiki* katika Mulika na. ya 7. uk. 24-32.

Mmbaga, N. (1978). *Dhima ya Ushairi katika Kuhifadhi Historia ya Jamii.* MULIKA na.14. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mulokozi, M. na Kahigi, K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mulokozi, M. na Sengo. T. (1994). '*Kauli Zilizotelewa katika Kongamano la Kiswahili.'* Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mulokozi, M. na Kahigi, K. (1995). *Malenga wa Bara*. Tanzania. Dar es Salaam Press.

Mutiiria, G. (2014). *Mchango wa Kimaudhui Watunzi wa Kike katika Ushairi wa Kiswahili.* Tasnifu ya M.A.Nairobi. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundations.

Ngugi wa Thiong'o (1977). *Home Coming*. Nairobi: H.E. B.

Ogot, B. (1974). *A Survey of East African History*. New Edition. Nairobi: Longman.

Ojenge, H. (2014). *Masuala Ibukizi katika Mashairi –Huru ya Kiswahili.* Tasnifu ya M.A. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Orodho, A. (2005). *Elements of Education and Social Science Research Methods*. Nairobi: Masola Publishers.

Raymond, W. (1977). *Marxicism and Literature*. U.S.A: Oxford University Press.

Rodney, W. (1972). *How Europe Underdeveloped Africa*. Dar es Salaam. Tanzania Publishing Press.

Sengo, T. (1973). *Dhima ya Fasihi katika Maendeleo ya Jamii*. Jarida la Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili. Vol.43/2. Dar es Salaam.

Senkoro, M. (1988). *Ushairi, Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Topan, F. (1977). *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*: Oxford University Press. Nairobi. (Mhariri)

Wambiri, G. na Muthee, D. (2010). *Research Monotoring and Evaluation in ECDE programmes.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi. Phoenix Publishers.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia.* Nairobi. Focus Publications Ltd.

Wamitila, K. (2008). *Kanzi ya Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Wafula, R. (1992) *'Nadharia kama Mwongozo wa Utunzi na Uhakiki katika Fasihi'*, Karatasi ya Semina, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wellek, R. na Warren, A. (1949). *Theory of Literature*. London: Pengune Books, Harmondsworth.

## Kiambatisho: Mashairi Teule.

### 1. NJIA TULOPITISHWA

Sasa wakokota tongotongo nzito
Machoni mwa mswaki kuukuu
Na kusafisha meno ya njano
Kisha wacheka gizani kwa mawi yatokeayo
Na kujigonga kwenye kichuguu
Walichokiumba na kuukimbia mchwa
Ulao kila kitu kilichoko
Mlima watoa cheche hafifu kileleni
Zisotosha kuonyesha njia.

Nzige waloanguliwa jangwani
Sasa walala juu ya majani.
Na yadaiwa mito na visima vimekauka.
Watetezi wapiga madebe shinda.
Ni ndege waoga tu washtukao.
Kesho tutakula nini, swali la watoto.
Sasa tufe hivihivi, la watu wazima.

Njia tulopitishwa yasikitisha.
Twasubiri mvua ya haki
Tukisawazishe kwa majembe makali
Na kukandika nyumba mpya

Na kuchoma moto malkia wa askari.

Penye haki vichuguu na milima hulala.

Ingawa hatuna machozi ya moto

Yatayofuta aibu hii tukufu

Bendera ya haki itapepea daima

Daima tutakuwa na kuwako.

Mbele ya umoja thabiti

Milima na vichuguu hulala.

**2. MAFURIKO**

Nitaandika wimbo juu ya mbawa za nzi

Utoe muziki arukapo wausikie walio wengi

Ushairi wa jalalani utaimbwa

Juu ya vidonda vya wakulima

Na usaha ulio jasho lao.

Nitaandika juu ya mbawa za wadudu

Wote warukao

Juu ya mistari ya pundamilia

Na maskio makubwa ya tembo.

Juu ya kuta vyooni, maofisini, madarasani,

Juu ya paa za nyumba, kuta za Ikulu,

Na juu ya khanga na tisheti.

Nitaandika wimbo huu:

Mafuriko ya mwaka huu

Yatishia nyumba kongwe bondeni.

Waliomo wameanza kuihama

Na miti ya umeme imeanguka.

Palipokuwa na mwanga, sasa giza.

Mafuriko ya mwaka huu!

Mti mkongwe umelalia upande

Wa nyumba zetu hafifu

Upepo mkali uvumapo hatulali.

Kila kukicha twatazama mizizi yake

Na mkao wake, na kuta hafifu za nyumba.

Lazima ukatwe kuanzia matawi hadi shina

Mafuriko ya mwaka huu yaashiria…

Tutabaki kuwasimulia wajukuu:

Mwaka ule wa mafuriko

Miti mingi mikongwe ilianguka.

Mafuriko ya mwaka huu!

Wengi wataumbuka.

## 3. JIBWA

Jibwa likitoka jikoni

Ulimi lajilamba

Piga limekwiba piga:

Jibwa likishika hatamu

Haliwezi kuacha utamu.

Jibwa likianza kula mayai

Jua wizi limefuzu

Kesho litakula kitovu

Cha mtoto wako pekee.

Jibwa jizi fisi.

Jibwa liloshika hatamu

Adabu yake kiburi,

Cheche halitafukuza.

Litalala kivulini

Wewe wachumia juani.

Jibwa liloshika hatamu

Litatumia kila hila,

Kila vitisho na unyama

Litakacho likipate

Na meno nje litatoa

Kwa kivuli kipitacho

Dawa ya jibwa shoka.

Subiri litapolala,

Na ndoto za kwiba likiota

Piga kichwa piga.

Life,

Life bila ukemi

Majirani wasichungulie.

Kisha kamba shingoni

Funga

Haraka haraka liburuze

Jalalani

Petroli

Mwagia, choma.

Jibwa jizi laana.

Kichaa likipata

Usimsubiri daktari.

Piga kichwa piga

Piga kwa bunduki, piga.

Washairi msigune.

Jibwa jizi mwalijua

Ni sisi twalifuga.

**4. MADOMO MAPANA**

Nitafukuzwa mbinguni

Kwa ushairi wangu mbaya

Lakini hata motoni nitaimba:

Wanasema

Wanasiasa ni kama jizi

Lililosukuma moto pembeni

Na kunyonya ziwa la mama

Wakati amelala usingizi usiku.

Wanasema.

Mwanasiasa afapo

Tumejikomboa na domo

Moja pana lizibwalo na mchanga

Na kilima cha sementi ngumu

Lisisikike tena hadharani.

Wanasema pia

Kusema haki

Kwa kawaida

Wanasiasa hatuwapendi.

Kupigia kura ni hasira ya mkizi

Ni basi tu. Ni Ah!

Ah!

Wanamalizia

Nchi mmeifilisi waachieni walimu

Wakajenge taifa jipya.

Kama hamwezi kuona mbali

Bure kuweka mkono usoni,

Bure kukuna kichwa

Kama hamwezi kufikiri.

Ng'ombe amekamuliwa na Wazungu

Waarabu, Wahindi na Wao

Sasa anatoa damu.

Vilivyobaki ni chai ya rangi

Na madomo mapana zaidi

Yaliyo bado hai.

Kuimba nimeimba.

**5. MARAHABA**

Kama sote tulitoka kisiwa kimoja

Cha Mungu mmoja Mfadhili

Basi sote yatupasa huko

Malalamiko yetu kuwasilisha.

Na

Yaelekea kadiri tunavyozeeka

Na matatizo ya maisha kuongezeka

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Twazidi kuyakumbuka makasia
Tuliyotundika ukutani ujanani
Na jasho lililowanisha miili yetu
Basi
Tuzibe matundu ya mtumbwi wetu
Na tupige makasia, tuelekee
Kwenye kisiwa cha uzima wa milele
Kama hapa duniani tu wasafiri.
Na
Tukifika, sote tuseme kwa sauti moja
Shikamoo Baba!

Lakini ghafla twajigonga kikondoo
Kwenye mwamba thabiti wa usasa
Usemao hawezi kujibu Marahaba.
Na
Kwa kutokuwa na hakika
Twaogelea juu ya vipande vya mtumbwi
Na kurudi kwa mioyo mizito duniani
Ambako twakaribishwa
Kunywa vikombe vya majonzi
Na kula ukoko wa mateso
Kati ya vilio vya maskini
Na ngumi za matajiri.

Ghafla kutoka mahali pasipojulikana

Twaskia ngurumo kubwa:

Marahaba.

**6. MKE WA WAZIRI**

**(WIMBO WA HARUSI)**

Wewe Monika

Ulitoka kwetu bila ushanga kiunoni

Kama kumbikumbi asi mbawa.

Ulipofika mjini ukaolewa na waziri

Sasa wataka tusimame barabarani

Kukupungia matawi mabichi.

Upitapo wainua kipua juu,

Chogo limechongoka kama senene

Aendaye kwenye harusi ya mende

Na kutusanifu kwa mawani meusi

Kama nyani achezaye sarakasi.

Unajua kuchekesha.

Sikiliza Monika.
Sisi tumezoea vituko vya wakubwa
Huyo mumeo anatoka kijiji jirani
Tulimwona akilambwa na mbwa
Alipomaliza kujisaidia
Na alikimbia siku ya tohara.
Sasa naye avuta kidevu, shingo upande
Kama beberu, tayari kupigana.
Wewe Monika
Twende ufukweni kuogolea
Tuone hiyo cheni ya dhahabu.
Mnajua kuchekesha.

Monika sikiliza.
Sisi wanawake wa shamba
Twajua mambo mawili
Kulima na kupalilia
Kuvuna twavunia wengine.
We Monika!
Kile kikwapa chako kimekwisha?
Na kisigino hakichani chandarua?
Wapi zile nywele za kipilipili?

We Monika!

Sasa unazo ngapi?

**7. WIMBO WA UNYAGO**

Ishi kijana ishi, ishi maisha yako.

Wazee waliishi yao

Sasa yamebaki kwako.

Ukabila ni utumwa

Olewa msichana olewa

Olewa chaguo lako

Hiari ni haki asilia

Achaguaye embe bichi

Ajua lini litaiva.

Chunga lugha ya ulaghai:

Usikubali kuitwa kipenzi

Hiyo ki ni ki ya kitoto;

Asifuye macho yako

Ataka kuyafumba;

Asifuye miguu yako

Ataka usitembee;

Asifuye meno yako

Ataka ucheke kijinga.

Akuandikiaye barua ndefu
Ashindwa kusema ukweli;
Na kadi maneno ya wengine.
Akupigiae simu kila siku
Hana la kusema bali haloo;

Asemaye mumeo hafai
Nyumbani kwake pia hafai
Mbwa aliwekwa utumwani
Kwa kifupa kiso mnofu.

Ee mama mwenye rutuba
Zaa, zaa kwa mpangilio,
Si kufyatua matofali.
Zaa ukichunga afya yako.
Tawi lenye matunda mengi
Huvunjwa na upepo wa tufani.
Kumbuka
Kuku aliwekwa utumwani
Kwa wingi wa vifaranga vyake
Akashindwa kujenga kiota.

**8. ALALAYE**

Mafuriko yaliyotokea

Yametosa matumaini ya wakulima

Na wafanyakazi baharini.

Wazamiaji wameshindwa kuyaona.

Wakulima sasa wabeba majembe yao begani

Na kurudi nyumbani vichwa chini.

Nyuma ndege watua

Na kula mbegu mpya walizosia.

Kimya wasota wakiimba kimoyomoyo:

Tumeona ngozi ya ng'ombe imewambwa

Wafikiri hatujui nyama ilikokwenda.

Tumeona mifupa ya kuku jalalani

Wadhani hatujui nani kafaidi.

Tumeona vyombo vikisafishwa jikoni

Wahisi hatujui nani kala.

Wanasema asiyekuwepo lake halipo

Alalaye usimwamshe.

Tunasema:

Kila mwanchi alikuwepo na yupo

Lake lazima liwepo

Alalaye huamka mapema.

**9. DHIFA**

Ni chakula cha mchana.

Walanchi wameshafika:

Wazungu, Wahindi, Waarabu

Weshateka sehemu zao.

Chakula ki mezani.

Ni dhifa.

Puani mwa Bwana Mkubwa

Kamasi jeupe lachungulia.

Waonao hawaoni,

Ila nzi atuae pale

Siyo tu kuliona

Bali kulila kabisa.

Kwa mbwembwe achezesha mbawaze.

Mawaziri wenye kula

Wabunge wapewa magari

Waandishi walosajiliwa

Watangazaji wenye yale yale

Wakereketwa wasokereka,

Kimya wamekaa.

Mpambe maskini nyuma amekaa.

Wacheza ngoma wakulima

Warukaruka jukwaani.

Pale pale bila papara

Nzi akunja kiunoche

Kwa shibe anya kabisa.

Ni dhifa.

Wapiga picha mso kibali pigeni

Mpaaambe pia aonekane

Na nnnzi .

Na kamaaasi.

Ni dhifa hii.

Moja, mbili tatu!

Vizazi tazamaneni.

Picha ya wakati huu

Ndiyo hii.

**10. BONDE**

Hapo zamani za kale palikuwa na giza

Halafu kutoka mlima Kilimanjaro jua likachomoza

Kwa tabasamu likang'ara juu ya nchi.

Pakawa na mwanga.

Halafu kutoka mlimani maneno makubwa

Yalijiviringisha kwa nguvu za wazo

Yakiangusha miti na nyumba za waliojua kusema.

Pakawa na ukimya.

Waliobaki waliandamana bila hadhari

Kutazama mawe yalikoishia.

Wakatumbukia kwenye bonde la fikra:

Pakawa na giza

Pakawa na mwanga

Pakawa na fikra.

Wakasema:

Sasa twaimba nyimbo za matunda ya mwanga

Na fikra pevu, tukifukia mashimo

Yaliyoachwa wazi.

**11. NAMAGONDO III**

Najua hapa nilivuta pumzi ya kwanza

Na labda ya mwisho nitaitoa hapa.

Roho yangu itakuwa imechakaza viatu

Vilivyokanyaga pengi:

Penye miiba, tope, moto na mazulia

Hadi siku nitapomkuta mgeni mwizi avisubiri.

Chai yangu nitakwisha kunywa

Kikombe changu kukikabidhi

Na kusema: kwaheri Nabili

Kwaheri miti; ndugu na marafiki

Na watoto kwaheri.

Kijinafasi changu nilishaomba.

Wahenga naja bila kalamu;

Nipeni nafasi kwenye duara.

Nyuma udongo utabusu mashavu yangu

Hadi nipate ile tabasamu ya milele.

**12. ULINGONI**

Wacheza ngoma sasa wamechusha.

Wacheza matako nje wala hawapendezi.

Mbwembwe zao sasa ujahili

Na hakuna awashangiliaye.

Wamebaki kuwashika watazamaji

Wacheze nao katikati ya duara.

Wafikiri wanajua:

Hawataki uwanjani kutoka.

Bila kubadilisha uwanja

Mwondoko ni uleule.

Kilichobaki ni kuanzisha kiufundi

Mduara mpya wenye mzingo mpana.

Watazamaji watahama polepole

Na vichwa vyao watatingisha

Kufuatisha mdundo mpya,

Wenyewe kwa hiari wakiingia ulingoni.

**13. CHA WATU**

Wazee wa uhuru wamepoteza miwani

Watoto wawasomea kinyumenyume

Na kuongezea yasiyokuwemo.

Ujumbe wa wenye fikra

Haufiki palipokusudiwa.

Udenda wao umedondokea chakula

Wageni wa watoto wasita kukila.

Wazee wamekula minofu yote

Sasa wajaribu hata mifupa.

Udenda wachirizika kwenye viwiko.

Watu lazima wajipikie chao.

**14. ZIMWI**

Zimwi limemeza watoto wote kijijini,

Sasa lenda likitagaa kuelekea ziwani.

Wanakijiji wafuatisha nyayo

Wakihesabu matumaini na kupima hatari.

Nyumbani wanawake vilio wameanza

Wakikumbuka uchungu walioupata.

Zimwi litujualo limetula likatwisha.

Mchangani limekunguwaa kivulini

Likiota pa kujisaidia.

Nzi watambaa wakinyonya udenda.

Watoto ndani wahesabu mali

Wakifikiria pa kutoboa.

**15. MASKINI 2**

Maskini amechinja maelfu ya sisimizi

Chajio cha mwisho.

Lakini bila kutafunwa

Ndani na nje wakurupuka

Na vipande vya mwiliwe

Mdomowe ukiwa wazi.

Alikufa juzi kwa njaa.

Kila mpita njia atupia jani bichi

Kuepuka laana.

Kesho atazikwa na halmashauri ya jiji

Bila jina.

**16. MAENDELEO SI NDWELE**

Mama Afrika atoka jiko-benki na mwiko

Akipiga kelele, "Panya!"

Chakula hakipikiki kikaiva

Watoto wagongana wao kwa wao

Katika msako na kutoana meno

Baba atoka chumbani na bunduki akiyumba

Akiimba wimbo wa Taifa la Afrika

Alioutunga ndotoni.

Panya anapita dirisha lilo wazi, nje.

Mtoto bubu awatazama na kucheka

Kitoto kichanga kinalia

Naye bundi anamshika panya gizani.

Maendeleo yameipiga chenga Afrika.

**17. UKWELI-KOKO**

Nimekuja kusema uwongo

Sikuja kusema ukweli.

Kwani mkigundua kuna ukweli

Katika uwongo mtapenda ushairi wangu.

Lakini mkigundua uwongo

Katika ushairi ulodai ukweli mtanichukia.

Niacheni niimbe:

Watawala Afrika ni wapenda demokrasia

Na fikra zao sahihi zadumu.

Umaskini ni wa kujitakia

Wafanyakazi wote wavivu kupindukia

Wavuna wapandacho

Ardhi, madini na nafaka ni mali ya umma.

Kiingereza na Kifaransa ni funguo za maisha.

Lugha za Kiafrika ni lugha za mitaani

Nimeimba. Ni mimi ukweli-koko.

**18. MSAMAHA**

Najua nimekukosea sana. Naomba msamaha.

Watoto waliona, majirani walisikia.

Uso wako ulovimba

Tokeo la mikono yangu hii michafu

Si pombe, si hasira, ni mimi.

Mama, nilikukosea sana

Naomba msamaha.

**19. MASKINI 3**

Mimi ni maskini wa kutupa

Nanyonywa na njaa yamalizia

Wakati nimekondeana kama siafu

Nitaingia ndani ya sikio la tajiri

Ukali mumumo nitang'ata

Sikio lilokataa kusikia kilio changu

Karne hadi karne kama ndege

Kiziwi nikinywa maji ya mvua

Yaliyobaki juu ya jani la mti

Wa utajiri utiririkao kama mto

Uyoyomao maziwani na baharini

Akaunti watu wasojua kuamka asubuhi

Na mpini uwekao sahihi ya ukata

Wasema sieleweki sitegemeki

Mimi mtetwa.

**20. MAKABURINI**

Baba, Mama. Twaitwa mzigo

Tangu mlipotuacha. Ajali tata ya gari.

Kila siku tu mlizamu wa sababu

Tu wadudu ndani ya kokwa.

Wasioweza kutekeleza "wauona mzigo huu".

Kipoteacho "ukome wizi wa baba yako!"

Kwa mwenzangu "umalaya wa mamako ukome!"

Tena kwangu "ulevi wa baba"

Kwake "ubahili na uchoyo wa mama".

Huo ndio urithi mliotuachia.

Watuitao maskini yatima watwambia ukweli.

Mlikuwa mfano wa kuigwa.

Baba, Mama. Ni sisi wanenu. Pacha.

Twauza *Bar.*

Twanawisha mikono wateja

Walokwisha kula mbuzi, ng'ombe, kitimoto.

Vyote hivi na *Bar,* vilikuwa vyenu. Twaskia tu.

Twachoma utajiri kuzalisha utajiri.

Tulokuwa nao darasa moja, sasa wasomi.

Sisi tumevalishwa sare. "Mlimani Bar".

Baba, Mama. Ni sisi

Watumishi wa Bamkubwa. Mkali-chui.

Kesho tutakuwa vitambaa

Vya kusafishia mikono chooni

Na tutafuliwa kila wiki

Ndani ya karai-kutu la machozi yetu.

Kesho k`utwa tutatupwa vidaso jalalani.

Baba, Mama. Ndisi.

**21. HOJA**

Asubuhi

Nikiwa ndani ya gari la utalii

Hiki ndicho nilichoona:

Simba dume akimfukuza pundamilia

Juu anamrukia amng'ata shingoni

Na chini aanguka kwa ukemi.

Simba aanzia tumboni kumrarua

Mlowe wa haki ya ubabe.

Nyani mtini wabwekabweka.

Uzuri wa sanaa ya Muumba

Wateketezwa kwa muda mfupi.

Si hoja.

Lakini

Nikakumbuka habari nilizosoma

Nikiwa ndani ya daladala:

Jana jioni kijana mmoja

Jinale limehifadhiwa

Alimbaka msichana

Wa miaka kumi na sita.

Dhuluma ya ubabe huweza kuharibu

Haiba-hulka ya utu kwa muda mfupi

Na adhabu, laini.

Ni hoja

Ni bado asubuhi.

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY